# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Tano




Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tano



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 555

Jina la Chapisho: Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano
Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania
Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania
ISBN: 978-9987-09-330-4

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tano katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 1 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018

Toleo la Pili 2021

ISBN: 978 - 9987 - 09 - 330 - 4

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar-es-Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170 / +255 735 041 168
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 2 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi** ......................................................................................iv

**Shukurani** .......................................................................................v

**Sura ya Kwanza**
Kujipenda na kuwapenda watu wengine ..............................................1

**Sura ya Pili**
Kujivunia shule na kuipenda nchi yetu ...............................................12

**Sura ya Tatu**
Muundo wa uongozi serikalini ..........................................................31

**Sura ya Nne**
Kujijali na kuwajali watu wengine .....................................................49

**Sura ya Tano**
Kuithamini jamii .............................................................................64

**Sura ya Sita**
Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi.................................................75

**Sura ya Saba**
Kusimamia majukumu ......................................................................86

**Sura ya Nane**
Kuwa mvumilivu...............................................................................97

**Sura ya Tisa**
Kufikia malengo ..............................................................................108

**Sura ya Kumi**
Kuwa mwadilifu...............................................................................122

**Sura ya Kumi na Moja**
Demokrasia ....................................................................................140

**Sura ya Kumi na Mbili**
Kudumisha amani............................................................................155

**Sura ya Kumi na Tatu**
Kushirikiana na mataifa mengine .....................................................175



URAIA NA MAADILI STD V .indd 3 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha tatu katika mfululizo wa vitabu vya Uraia na Maadili kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa darasa la tano. Kitabu kimeandaliwa kulingana na muhtasari wa Uraia na Maadili wa mwaka 2016.

Kitabu kimezingatia mwenendo na matarajio ya nchi yetu ya Tanzania katika kukujengea uwezo wa kujipenda na kuwapenda watu wengine, kujivunia shule yako, pamoja na kuipenda nchi yako. Pia, utajifunza muundo wa uongozi serikalini, kujijali na kuwajali watu wengine, kuithamini jamii, kulinda rasilimali na maslahi ya nchi. Aidha, utajifunza namna ya kusimamia majukumu na mambo yanayoonesha tabia ya uvumilivu. Vilevile, maudhui ya kitabu hiki yatakujenga kufikia malengo, tabia ya uadilifu, kusimamia misingi ya demokrasia na kujenga ari ya kudumisha amani katika nchi. Kadhalika, maudhui ya kitabu hiki yatakuwezesha kutambua ushirikiano wa Tanzania na mataifa mengine.

Kitabu hiki kina sura kumi na tatu na kila sura imeundwa na vipengele kadhaa. Aidha, baadhi ya matini ya sura za kitabu hiki yamejengwa kwa visa, habari, mazungumzo, nyimbo, mashairi, ngonjera, michoro na picha.

Kila sura ina mazoezi na kazi ya kufanya. Vilevile, ufafanuzi wa msamiati umetolewa mwishoni mwa kila sura ili kukusaidia kuelewa kwa urahisi zaidi umahiri unaohusika.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 4 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa Kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

| | |
|---|---|
| **Waandishi**: | Musa T. Mwalutanile, Prof. Willy L. Komba, Dkt. Aldof S. Mihanjo, Isaya M. Msanga, Debora W. Mbogoso, Christina C. Malima na Lucy C. Kimbi. |
| **Wahariri:** | Ambrose Mghanga (BAKITA), Chediel R. Nyirenda (Mwenyekiti wa jopo) na Jopo la wahariri. |
| **Msanifu:** | Benjamin Majengo |
| **Wachoraji:** | Alama Art and Media Production Limited |
| **Mratibu:** | Musa T. Mwalutanile |

Pia, TET inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 5 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kujipenda na kuwapenda watu wengine

Ulipokuwa darasa la nne ulijifunza matendo ya kujipenda na kuwapenda watu wengine. Katika sura hii, utajifunza matendo yenye kuonesha upendo kwa watu wenye mahitaji maalumu, kuheshimu jinsi na kuvaa mavazi yenye staha katika miktadha mbalimbali kulingana na utamaduni wa mtanzania.

### Kuwapenda watu wenye mahitaji maalumu

Je, umewahi kusikia mtu akisema kuwa inakupasa kuwapenda wenzako? Je, upendo ni nini? Upendo ni tabia na matendo ya kutojiumiza au kutowaumiza watu wengine kwa makusudi, kimwili, kiroho au kisaikolojia. Mara nyingi, huwa tunasema kuwa upendo halisi hauna mipaka. Kwa kutambua hilo, inatupasa kujipenda na kuwapenda watu wengine bila ubaguzi. Watu wenye mahitaji maalumu wanahitaji upendo zaidi kwa sababu ya hali zao. Hivyo, inatupasa tusifanye matendo ya kuwaumiza. Mifano ya watu wenye mahitaji maalumu ni wazee, watu wasioona, watu wenye uoni hafifu, watu wenye ulemavu wa ngozi, watu wenye ulemavu wa akili na wenye ulemavu wa viungo vingine vya mwili. Mifano mingine ni watoto yatima na watu masikini.

### Chunguza picha hii, kisha jibu maswali yanayofuata.



*Kielelezo namba 1: Wanafunzi wakishirikiana kusoma bila kuwabagua wenye ulemavu*



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 1 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Ni wanafunzi gani katika picha hii wana mahitaji maalumu?
2. Je, wanafunzi hao wanahitaji msaada gani?
3. Kuna faida zipi za kuchangamana au kushirikiana na wenzako wenye mahitaji maalumu?
4. Utatenda matendo gani kwa wanafunzi wenzako wenye ulemavu wa kutoona au uoni hafifu?
5. Unaweza kufanya mambo gani mengine ili wanafunzi wenye mahitaji maalumu wasijisikie wapweke?

**Kazi ya kufanya**

Jadili na wanafunzi wenzako kuhusu watu mbalimbali wenye mahitaji maalumu na jinsi ya kuwasaidia. Orodhesha mahitaji hayo na msaada wanaohitaji kwenye daftari lako na kumpa mwalimu.

## Kutenda matendo yenye kuheshimu jinsi nyingine

Je, umewahi kusikia katika maisha yako neno jinsi? Mara nyingi watu hushindwa kutofautisha neno jinsi na jinsia. Wewe unafikiri maneno hayo yana maana moja? Ipo tofauti kati ya maneno jinsi na jinsia. Neno jinsi lina maana ya tofauti za kimaumbile zilizopo kati ya mwanaume na mwanamke. Tofauti za kijinsi na majukumu yake hayabadiliki kwa sababu ni ya kimaumbile.

## Angalia jedwali lifuatalo linalotofautisha jinsi

| Mwanamke | Mwanaume |
|---|---|
| Anaweza kupata mimba | Anaweza kusababisha mimba |
| Hupata hedhi | Hapati hedhi |
| Ananyonyesha mtoto | Hanyonyeshi mtoto |

*Jedwali namba 1: Tofauti kati ya jinsi*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jinsia ni uhusiano uliopo kati ya mwanamke na mwanaume ulioundwa na jamii husika. Jinsia inahusu mgawanyo wa majukumu kati ya wanawake na wanaume katika jamii. Japokuwa wanawake na wanaume wanatofautiana kimaumbile, wanaweza kushirikiana majukumu mbalimbali. Kwa mfano, wote wanaweza kuwa viongozi bora na pia wote wanaweza kufanya kazi za kitaalamu. Tofauti za kijinsia zinaweza kubadilishwa kulingana na uelewa wa haki za binadamu. Yapo matendo mengi yanayoonesha kuheshimu jinsi na kujali jinsia.

## Hebu tafakari matendo yafuatayo:

(i) Mwanafunzi wa kike akimwelekeza mwanafunzi wa kiume kukokotoa maswali ya hisabati.

(ii) Mwanafunzi wa kiume na wa kike wakiosha vyombo pamoja.

(iii) Mwanafunzi wa kiume akimtua mwanafunzi wa kike ndoo ya maji kichwani.

(iv) Mwanafunzi wa kiume akikataa kuketi katika dawati moja na wanafunzi wa kike.

(v) Wanafunzi wakigombana na kutumia lugha ya matusi kwa kutaja viungo vya maumbile ya kijinsi.

Je, ni matendo gani kati ya hayo ambayo hayaheshimu jinsi nyingine?

Matendo ya kudhalilisha kijinsi yanaonesha kuvunjiana heshima. Matendo kama haya yanapotokea, unapaswa kuyakemea na kutoa taarifa kwa walimu, wazazi, au walezi.

## Matendo yanayoonesha usawa wa kijinsia:

(i) Kutoa elimu sawa kwa mtoto wa kike na wa kiume

(ii) Kutambua kuwa mwanaume na mwanamke wote ni binadamu

(iii) Kutobaguana katika kutekeleza majukumu mbalimbali nyumbani na shuleni

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 3 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha hizi, kisha tafakari matendo haya.**

1




2



*Kielelezo namba 2: Matendo yanayozingatia usawa wa kijinsia*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 4 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika ukuaji wako utapitia hatua mbalimbali. Katika kila hatua unawajibika kujitambua, kujua majukumu yako, kujiheshimu na kuwaheshimu wenzako wa jinsi nyingine. Kwa mfano, kuna hatua ya kuanza kupata hedhi kwa watoto wa kike na kubalehe kwa watoto wa kiume. Hiki ni kipindi cha kupevuka kimwili, kiakili na kimawazo. Mabadiliko haya husababisha hisia ambazo zinaweza kuathiri mwenendo na haiba yako. Hivyo, ni vyema kufikiri kabla ya kusema au kutenda. Maneno unayozungumza yasiwaudhi wenzako wa jinsi tofauti. Pia, matendo unayotenda yasisababishe wao kuumia au kujiona wanyonge.

Inafaa kujenga uhusiano chanya kati ya wasichana na wavulana kwa kutambua mipaka ya uhusiano huo na umuhimu wa kuthamini utu wa mwingine. Kwa mfano, siyo vizuri kumcheka mwenzako kutokana na kubalehe na kupata hedhi. Vilevile, si vizuri kutumia lugha za matusi au kumgusa mvulana au msichana viungo vyake vya maumbile ya kijinsi na kumbagua. Mara zote, pale ambapo unabalehe au kupata hedhi mambo yanayoendana na jinsi yako yanaanza kubainika katika mwili. Kwa mfano, msichana anaweza kutoka chunusi usoni, kupata hedhi, kuota matiti na kupata mimba. Mvulana kwa upande wake anaweza kutoka chunusi usoni, sauti inaweza kuwa nzito, anaweza kuota ndoto nyevu na huweza kusababisha mimba.

Ili kuepuka madhara, kila jinsi iwajibike kujitunza kwa kutambua kuwa wakati huo siyo wa uhusiano wa kimapenzi. Hivyo basi, katika kipindi cha balehe unatakiwa kujijengea uwezo wa kudhibiti hisia zako. Ili kuepuka vitendo vinavyoweza kusababisha madhara, ni vyema kujiepusha na mazingira hatarishi kama vile, kupita vichochoroni peke yako au matembezi yasiyo ya lazima ya usiku. Pia, wasichana wajiepushe na kupenda kupokea zawadi kutoka kwa wavulana au wanaume.

**Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Ana alikuwa msichana mwenye uwezo mkubwa sana darasani. Alikuwa mchangamfu, akishiriki kikamilifu kwenye michezo na ngoma mbalimbali shuleni. Alikuwa na marafiki aliokuwa akicheza nao. Alipofika darasa la tano alibadilika ghafla. Siku moja, nguo yake ilionekana imechafuka. Wenzake darasani walimcheka na wavulana wakaanza kumbeza kwa miluzi. Mvulana mmoja alimbinyia jicho.*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 5 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Ana alianza kusononeka. Uchangamfu ulipungua na hakuwa anashiriki tena vizuri kwenye michezo. Alianza kujitenga na kutokushirikiana na wenzake katika kujifunza.*

**Zoezi la 2**

1. Mwanzoni Ana alikuwa mtoto wa aina gani shuleni?
2. Ana alipata mabadiliko gani?
3. Ana alifanyiwa vitendo gani ambavyo vilikiuka haki zake za kijinsi?
4. Una ushauri gani kwa wanafunzi wenzako wenye tabia kama ya wale waliomzomea na kumcheka Ana?
5. Kuna tofauti gani kati ya neno jinsi na jinsia?
6. Taja matendo ambayo ukitendewa utakuwa umedhalilishwa kijinsia.
7. Orodhesha matendo yanayofanyika shuleni kuonesha usawa wa kijinsia.
8. Taja matendo yanayoonesha kuheshimu jinsi nyingine.
9. Orodhesha matendo ya nyumbani yasiyoonesha usawa wa kijinsia.
10. Tofautisha kati ya udhalilishaji wa kijinsi na udhalilishaji wa kijinsia.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi kuhusu shughuli unazoweza kushiriki nyumbani kwenu bila kujali jinsi na jinsia. Andika shughuli hizo kwenye daftari lako, kisha liwasilishe kwa mwalimu.

## Kuvaa mavazi yenye staha katika miktadha mbalimbali

Je, ni mavazi gani huwa unayavaa mara nyingi? Mavazi tunayovaa huwa yanabeba au yana tafsiri namna tulivyo. Mavazi yenye staha yanaonesha tabia ya kujiheshimu na kujithamini. Je, unafikiri ni mavazi gani huonesha staha? Pamoja na majibu ambayo unaweza kuwa nayo, kwa kawaida



URAIA NA MAADILI STD V .indd 6 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mavazi yenye staha kwa wasichana ni sketi ndefu isiyobana, gauni refu lisilobana, blauzi isiyoonesha matiti wala kitovu, suruali ambayo ni ndefu na isiyobana. Kwa upande mwingine, mavazi yenye staha kwa wavulana ni kama vile suruali ambazo hazibani maungo ya mwili wala zisizochanwa, au kuvaliwa chini ya kiuno.

Uvaaji wa mavazi yenye staha huendana na miktadha. Kwa mfano, sehemu za ibada zina aina yake ya mavazi, shuleni huvaliwa sare zenye staha, michezoni huvaliwa mavazi ya aina yake kwa ajili ya michezo.

Baadhi ya nguo huvaliwa na jinsi zote kama vile; suruali, kaptura na koti. Lakini mtoto wa kiume havai gauni wala sketi. Hali kadhalika, hali ya hewa huainisha aina ya mavazi yafaayo kuvaliwa. Kuna mavazi yanayotakiwa kuvaliwa wakati wa joto na yale yanayovaliwa wakati wa baridi. Mavazi yavaliwayo wakati wa baridi ni koti, sweta, mashati ya mikono mirefu na suti.

Mavazi yanayovaliwa wakati wa joto ni kama vile, kaptura, magauni na mashati yenye mikono mifupi. Pia, baadhi ya watu huvaa mavazi kama magauni mapana, baibui, misuli na kanzu kwa mikoa yenye joto kama Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Hata hivyo, tuepuke kisingizio cha hali ya hewa kwa lengo la kuvaa mavazi yasiyo na staha.

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**




*Kielelezo namba 3: Mavazi ya staha na yasiyo ya staha*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 7 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

1. Picha zipi zinaonesha mavazi ya staha?
2. Ni picha zipi zinaonesha mavazi yasiyo ya staha?
3. Utamshauri nini mwenzako anayependa kuvaa mavazi yaliyopo kwenye picha namba 2?

**Kazi ya kufanya**

Chunguza mavazi yasiyo ya staha yanayovaliwa na watu katika jamii unayoishi kisha, bainisha kwa kuandika kwenye daftari lako maeneo ambayo mavazi hayo huvaliwa.

## Mavazi ya utamaduni

Mavazi ya kiutamaduni ni mavazi ambayo hubeba utambulisho wa jamii fulani. Mavazi hayo hutambulisha mila na desturi za kabila fulani. Kuna baadhi ya mavazi ambayo huonesha tamaduni mbalimbali. Mavazi hayo ni kama lubega hasa kwa watu wa jamii ya kimasai; kanzu, msuli, koti na baraghashia hasa kwa jamii ya watu wa pwani. Vilevile, yapo mavazi maalumu yanayovaliwa na viongozi wa kimila kama vile watemi na machifu. Kwa mfano, machifu wa makabila ya Wangoni na Wahehe huvaa migolole. Pia, kuna mavazi maalumu wakati wa kucheza ngoma za kiasili. Mfano, kaptura nyeupe na shati jeupe huvaliwa na watu wa kabila la Wanyasa kwenye ngoma ya mganda na nguo ya kaniki huvaliwa kwenye ngoma za asili za Kigogo.

Kutokana na utandawazi, Tanzania imekuwa ni soko la mavazi yanayotoka kwenye tamaduni za nchi mbalimbali. Pamoja na matokeo ya utandawazi ambayo hayaepukiki, tunawajibika kuchagua mavazi yasiyotudhalilisha wala kushusha heshima yetu na ya nchi yetu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 8 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1



2



*Kielelezo namba 4: Watu waliovalia mavazi ya utamaduni*

**Zoezi la 4**

1. Taja mavazi ya asili ya kabila lako.
2. Unadhani ni watu wa jamii gani huvaa vazi lililooneshwa kwenye picha namba 2 katika kielelezo namba 4 wanapocheza ngoma za asili?
3. Taja faida mbili za mavazi ya asili.
4. Taja athari mbili za kimavazi zitokanazo na utandawazi katika jamii yako.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 9 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wenzako kuhusu mavazi yasiyo ya staha ambayo yanavaliwa katika jamii yenu na jinsi mtakavyowashauri watu waache kuvaa mavazi hayo. Andika ushauri mliokubaliana katika daftari lako, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Zoezi la 5

Andika **Kweli** au **Si Kweli** kwa maswali yafuatayo:

1. Upendo halisi ni kujipenda mwenyewe. ___________
2. Watu wenye ulemavu wana mahitaji maalumu. ______
3. Moja ya mahitaji ya kwanza ya mtu ni upendo. ____
4. Majukumu ya kijinsi hubadilika. __________
5. Majukumu ya kijinsia hubadilika kutokana na mtazamo wa jamii husika. ___________
6. Watoto wa jinsi zote wanapaswa kujiheshimu na kuheshimiwa. __________
7. Wanaume wote hawashiriki kabisa kupika chakula nyumbani. _____________
8. Mavazi ya heshima yanaonesha tabia ya kupitwa na wakati na ushamba. ____________
9. Mavazi mengine huvaliwa na wanawake na wanaume. ____________
10. Vazi la lubega halivaliwi na Wamasai. ____________

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 10 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Balehe | mabadiliko ya kimwili ya mtoto wa kiume na wa kike kuingia utu uzima |
| Haiba | tabia nzuri na mwenendo wa kupendeza unaowafanya wengine wawe na mvuto wa heshima kwako |
| Hedhi | damu inayomtoka msichana au mwanamke kila mwezi |
| Kaniki | aina ya kitambaa cheusi cha nguo ya pamba, huvaliwa na wanawake badala ya kanga au kitenge |
| Kudhibiti | kuweka kitu chini ya mamlaka au kutawala kitu barabara |
| Mgolole | shuka ndefu inayovaliwa na baadhi ya viongozi wa kimila |
| Muktadha | mazingira ambamo tukio au jambo hutendeka |
| Staha | heshima na adabu |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 11 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Kujivunia shule na kuipenda nchi yetu

Katika sura ya kwanza, ulijifunza matendo yenye kuonesha upendo kwa watu wenye mahitaji maalumu, kuheshimu jinsi na kuvaa mavazi yenye staha. Katika sura hii, utajifunza mambo yanayoiletea shule sifa nzuri. Pia, utajifunza umuhimu wa kuenzi tunu za taifa letu ambazo ni tamaduni, mila na desturi zetu. Vilevile, utajifunza alama za utambulisho wa taifa letu pamoja na sikukuu za kitaifa.

### Kuipenda na kujivunia shule yetu

Hebu jiulize, je, unaipenda shule yako? Je, unajivunia shule yako? Unajivunia vitu gani katika shule yako?

Sifa nzuri za shule zinajumuisha tabia njema za wanafunzi na walimu, majengo safi na mazingira yanayovutia. Hivyo, sifa nzuri ya shule inatokana na shule kuwa na mazingira yanayotunzwa kwa kupandwa miti ya vivuli, miti ya matunda pamoja na maua.

Vilevile, sifa nzuri ya shule huchangiwa na wanafunzi kuwa nadhifu kwa kutunza sare zao na vifaa wanavyotumia katika mchakato wa kujifunza. Wanashirikiana kutunza rasilimali na samani za shule kama vile majengo, madawati, viti, vitabu na madaftari yao. Hali kadhalika, wanafunzi wanajituma na kuwajibika ipasavyo. Uwepo wa mambo yote haya husababisha ufaulu mzuri na kujenga sifa nzuri ya shule.

Sifa mbaya za shule zinajumuisha tabia zilizopo shuleni ambazo hazikubaliki miongoni mwa jamii inayoizunguka. Sifa mbaya ya shule inachangiwa na mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu na mazingira machafu.

Pia, kuna vitendo vya utovu wa nidhamu kwa baadhi ya wanafunzi, kama vile kutovaa sare ya shule kikamilifu, kushindwa kufua sare zao na kuchana madaftari na vitabu. Vilevile, baadhi ya wanafunzi wana tabia ya utoro, uvivu na kuchelewa kufika shuleni. Hali hii huchangia

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 12 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

sifa ya shule kuwa mbaya. Aidha, matendo ya baadhi ya walimu kuonesha tabia za uvunjifu wa taratibu na sheria za kazi. Mfano wa vitendo hivyo ni ugomvi baina ya walimu, walimu na wanafunzi, walimu kutotumia lugha yenye staha wawapo mazingira ya shule au katika jamii. Mambo yote haya yanaweza kusababisha shule kuwa na sifa mbaya.

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1



2



*Kielelezo namba 1: Utunzaji wa mazingira shuleni*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Unaona nini katika picha namba 1 na 2?
2. Elezea mazingira ya shule katika picha namba 1.
3. Linganisha mazingira ya shule iliyopo kwenye picha namba 1 na ya shule yako.
4. Orodhesha vitendo vya wanafunzi unavyovifahamu vinavyoweza kuifanya shule yenu iwe kwenye hali kama ilivyo kwenye picha namba 1.
5. Je, wanafunzi waliopo kwenye picha namba 2 wameshika nini?
6. Taja tabia za wanafunzi zinazochangia kuchafua mazingira ya shule yako.
7. Taja sifa nzuri zinazobainisha shule yako.
8. Ungepewa nafasi ya kushiriki michezo inayoiletea shule yako sifa nzuri, ungeshiriki mchezo au michezo ipi?
9. Wewe na wanafunzi wenzako, pamoja na walimu, mnatakiwa kutenda matendo gani ya ziada ili shule yenu iwe na sifa nzuri? (Tofautisha matendo ya wanafunzi na yale ya walimu).

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na mwalimu wa mazingira shuleni kwako kuhusu changamoto zinazowakabili katika kutunza mazingira ya shule yenu na jinsi ya kuzitatua. Andika mapendekezo yaliyotokana na majadiliano hayo kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Nembo ya shule yetu

Je, unafahamu maana ya neno nembo? Nembo ni alama maalumu inayotambulisha kitu fulani. Nembo ya shule ni alama inayoitambulisha shule inayohusika. Kwa kawaida nembo ya shule hujumuisha kauli mbiu ya shule, shughuli mbalimbali za shule kama vile shughuli za kitaaluma, elimu ya kujitegemea na mazingira ya shule.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 14 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Je, shule yako ina nembo inayoitambulisha? Je, nini kauli mbiu ya shule yako? Ili kuifahamu vizuri nembo ya shule yako mwalimu atakuonesha na pia atakuongoza kuichora.

## Kufanya shughuli mbalimbali za kujitolea shuleni

Je, umewahi kufanya kazi za kujitolea shuleni kwako? Ulijisikiaje ulipofanya hivyo? Ilikuwa shughuli gani? Kujitolea ni tabia ya kufanya jambo kwa hiari bila kushurutishwa na pasipo kujali maslahi binafsi. Kwa mfano, unaweza kujitolea kupanda miti na maua katika mazingira ya shule au kuanzisha bustani za mboga. Pia, unaweza kuanzisha na kushiriki katika klabu mbalimbali kwa mfano skauti, klabu ya mazingira, klabu ya UKIMWI, klabu ya kutoa elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa na klabu ya elimu kwa mlipa kodi. Aidha, unaweza kushiriki katika shughuli ya kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, madarasa na vyoo vya shule.

Pia, unaweza kushiriki katika shughuli mbalimbali shuleni hasa za elimu ya kujitegemea ili kuleta maendeleo katika shule na kuongeza kipato. Baadhi ya shughuli hizo ni kilimo na ufugaji, kuanzisha vitalu vya kuotesha miche ya miti na kujiunga na masomo ya ziada ya ufundi stadi endapo shule yako ina masomo hayo.

**Zoezi la 2**

1. Eleza umuhimu wa nembo ya shule.
2. Bainisha mambo ya msingi yaliyomo kwenye nembo ya shule yako.
3. Je, umewahi kufanya shughuli za kujitolea shuleni kwako au katika jamii? Zitaje.
4. Baada ya kusoma kipengele cha shughuli za kujitolea shuleni, unafikiri unaweza kuanzisha au kujiunga katika shughuli zipi?

**Kazi ya Kufanya**

Chora nembo ya shule yako katika daftari lako, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 15 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Tunu za nchi yetu

Tunu ni mambo yote ya thamani ambayo watu hujionea fahari kuwa nayo. Je, tunu za nchi ya Tanzania ni zipi? Tunu za nchi yetu ya Tanzania ni lugha yetu ya Kiswahili, umoja, mshikamano, uzalendo, uwajibikaji, upendo, heshima na utu. Sisi sote yatupasa kuipenda na kujivunia nchi yetu kwa kuzienzi tunu zinazoitambulisha. Vilevile, ni muhimu kuheshimu mila na desturi zetu na kudumisha tamaduni zetu kama sehemu ya tunu za taifa.

## Mila na desturi za Kitanzania

Je, umewahi kusikia mtu akikuambia tudumishe mila na desturi zetu? Ulielewa kuwa anamaanisha nini? Mila na desturi ni namna tulivyozoea kufanya mambo katika jamii yetu tangu zamani. Mila na desturi vinaweza kutafsiriwa kama ni mapokeo ambayo jamii hurithishana kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mila na desturi hujenga au kuunda utamaduni ambao ndio utambulisho wa jamii hiyo. Nchini Tanzania kuna mila na desturi mbalimbali ambazo hubeba utambulisho wa jamii mbalimbali. Kuna mila na desturi zinazofaa na zisizofaa, kama ilivyobainishwa katika Jedwali namba 1.

Ili kuimarisha utamaduni wa taifa, inatupasa kudumisha mila na desturi zinazofaa na kutokomeza mila na desturi zisizofaa ambazo ni kikwazo kwa maendeleo ya familia, jamii na hata taifa kwa ujumla.

**Tafakari maneno yaliyopo kwenye jedwali hili, kisha jibu maswali yanayofuata.**

| Mila na desturi zinazofaa | Mila na desturi zisizofaa |
|---|---|
| Zinahamasisha watu wote kufanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano. | Zinahamasisha wanawake kubeba majukumu ya kutunza familia, wakati wanaume hawawajibiki ipasavyo. |
| Vijana kwenda jandoni na kupewa mafunzo na majukumu. Pia, kuwafundisha kuhusu mapokeo mema ya tamaduni zao ili kujenga ari ya uwajibikaji ndani ya jamii. | Baadhi ya makabila, hukeketa wasichana na kuwacheza ngoma zisizo na maadili mfano kumcheza mwali na vigodoro. |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 16 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| Zinahamasisha wanafamilia wa jinsi zote kushirikiana kufanya kazi za nyumbani na za kujiongezea kipato katika familia. | Zinahamasisha uvivu na ubaguzi wa jinsi moja kutoshiriki kufanya kazi za nyumbani. Mfano, mtoto wa kiume kutoshiriki kazi kama kuosha vyombo na kupika. |
| Mgawanyo wa kazi unaozingatia usawa wa kijinsia. | Mgawanyo wa kazi usiozingatia usawa wa kijinsia. Kwa mfano, kumtumikisha mwanamke kufanya kazi nyingi kuliko mwanaume. |
| Haki za watoto zinaheshimiwa | Watoto hawana haki. |

*Jedwali namba 1: Mila na desturi zinazofaa na zisizofaa*

**Zoezi la 3**

1. Orodhesha mila na desturi nyingine zisizofaa unazozifahamu mbali na hizo zilizotajwa katika jedwali la 1.
2. Orodhesha mila na desturi zinazofaa zilizopo katika jamii yako.
3. Taja ngoma nyingine zinazodhalilisha jamii kijinsi na kijinsia katika maeneo unayoishi.
4. Orodhesha mambo yanayoweza kufanywa ili kurekebisha kila desturi zisizofaa kwenye jedwali la 1.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako juu ya mambo matatu yanayofanywa hapo shuleni yanayoakisi mila na desturi zinazofaa. Orodhesha kwenye daftari lako, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kudumisha utamaduni wa taifa

Umewahi kusikia neno utamaduni? Je, umewahi kuwaza maana ya neno hili? Tunaweza kuutafsiri utamaduni kuwa ni mwenendo wa maisha

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

unaohusisha asili, mila, desturi, jadi, au itikadi inayotawala katika jamii fulani. Pia, ni mtindo wa jumla wa maisha ya jamii fulani. Hivyo, kudumisha utamaduni wa taifa ni kuzingatia mila na desturi zinazofaa, pamoja na mambo mengine yote yanayojenga umoja katika jamii na taifa.

## Umuhimu wa utamaduni

Utamaduni ndio unaobeba utambulisho wa taifa letu. Pia, utamaduni unajenga moyo wa kujiamini na kujithamini. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili hulitambulisha taifa la Tanzania. Wasanii wanapokwenda nje ya nchi hulitambulisha taifa letu kwa sanaa wanayoipeleka huko. Vilevile, utamaduni hujenga umoja, upendo, ushirikiano, kuthaminiana na kuheshimiana.

Utamaduni hudumisha mila na desturi za jamii kwa kupitia mafunzo mbalimbali ya vijana, kwa mfano mafunzo ya jando na unyago katika jamii fulani kulingana na wakati. Mafunzo hayo huwawezesha kuishi maisha yanayokubalika katika jamii husika. Pia, utamaduni huhimiza kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, ili kupanua fursa za ajira. Kazi za sanaa kama vile maigizo, muziki, michezo, ngoma na kuchonga vinyago huimarisha kipato cha mtu binafsi, jamii na taifa.

Aidha, kwa kupitia utamaduni tunapata burudani katika miktadha mbalimbali; mfano, nyimbo na ngoma za asili zinapochezwa. Nyimbo na ngoma za asili pia hutumiwa na makabila mbalimbali kama kichocheo cha kuhamasisha kufanya kazi kwa bidii, kujenga tabia nzuri na nidhamu katika maisha. Kwa mfano, kabila la Wasukuma hupiga ngoma wakati wa kulima ili kuhamasisha ari ya kufanya kazi.

Tunaweza kudumisha utamaduni wetu kwa njia mbalimbali. Njia mojawapo ni kwa kushiriki katika mambo ya sanaa na ngoma za asili. Njia nyingine ni kutumia lugha zetu za asili, kuitumia na kuienzi lugha ya Kiswahili katika matukio mbalimbali mfano, shughuli za kiserikali na za kijamii. Aidha, tunatakiwa kujivunia, kutumia na kuyaenzi mavazi yetu ya asili, kudumisha mila na desturi zinazofaa, kutumia na kuvitangaza vyakula vyetu vya asili. Pia, tunatakiwa tuzienzi mila na desturi zetu hasa zile zinazoimarisha uhusiano mwema. Vilevile, ni muhimu kuidumisha heshima na uhusiano kwa kuzingatia taratibu za kusalimiana katika jamii. Kwa mfano, kwa kawaida mtu mwenye umri mdogo ndiye anayepaswa kuanza kumsalimia mtu mwenye umri mkubwa. Utamaduni ni kielelezo cha uhai wa jamii yetu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1



2



*Kielelezo namba 2: Vitendo vya kudumisha utamaduni*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 19 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. Je, unaona nini kwenye picha namba 2 iliyopo katika kielelezo namba 2?
2. Taja vitu unavyoviona kwenye picha namba 1
3. Orodhesha faida zitakazoletwa na vitendo vilivyooneshwa katika picha unazoziona.
4. Taja vitu walivyoshika watu waliopo katika picha namba 2 katika kielelezo namba 2.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi kuhusu ala za muziki wa asili zinazotumika katika jamii yenu, kisha chora ala hizo na uziwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Alama za taifa

Ulipokuwa darasa la nne ulijifunza matendo ya kuipenda nchi yetu kama vile kuonesha heshima kwa wimbo wa taifa na bendera ya taifa, pamoja na kuthamini fedha ya Tanzania. Katika sura hii, utajifunza kwa undani zaidi matumizi ya alama hizi za taifa. Aidha, utajifunza matumizi ya bendera ya taifa, wimbo wa taifa, mnyama wa taifa (twiga), nembo ya taifa, fedha ya taifa, bendera ya rais, mwenge wa uhuru, katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ramani ya Tanzania.

## Matumizi ya alama za taifa

Je, ulishajiuliza umuhimu wa alama za taifa? Alama hizi hutumika wakati fulani, kwenye mazingira fulani na kwa lengo fulani. Hebu tuyabaini matumizi ya alama za taifa la Tanzania.

## Bendera ya taifa

Bendera ya taifa inaitambulisha nchi ya Tanzania miongoni mwa mataifa mengine. Bendera yetu ya taifa hupepea katika nchi zote ambako Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 20 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

imefungua ofisi za ubalozi. Pia, viongozi na baadhi ya Watanzania wanaposafiri nje ya nchi kwa lengo la kuiwakilisha Tanzania, hubeba bendera yetu ya taifa.

Bendera ya taifa hutambulisha pia vyombo vya usafiri vinavyosajiliwa Tanzania. Vyombo hivyo ni meli, ndege, magari na pikipiki. Vilevile, bendera ya taifa hutambulisha ofisi au taasisi za serikali kama vile shule, ofisi ya kijiji, kata, wilaya na mkoa, majengo ya mahakama na ofisi za wizara mbalimbali.

Pia, bendera ya taifa hutumika kuonesha majonzi pale inapotokea msiba au janga la kitaifa. Mifano ya majonzi hayo ni kama vile kifo cha baba wa taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ajali ya MV Bukoba iliyotokea tarehe 21 mwezi wa 5 mwaka 1996 na Kivuko cha MV Nyerere iliyotokea tarehe 20 mwezi wa 9 mwaka 2018 katika Ziwa Viktoria ambapo meli na kivuko hicho vilizama na kusababisha vifo vya watu wengi. Katika maombolezo ya matukio kama hayo bendera ya taifa hupepea nusu mlingoti.

## Wimbo wa taifa

Kwa kiasi kikubwa matumizi ya wimbo wa taifa yanafanana na yale ya bendera ya taifa. Wimbo wa taifa huimbwa wakati viongozi wa nchi wanapotembelea nchi nyingine. Pia, huimbwa wakati vikundi vya utamaduni na michezo wanapocheza michezo ya kimataifa ndani na nje ya nchi. Pia, wimbo wa taifa huimbwa kabla ya tangazo la msiba wa kiongozi mkuu wa nchi, kama vile Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Hali kadhalika, kabla ya rais kufanya uzinduzi wa jambo muhimu linalogusa maslahi mapana ya taifa, huimbwa wimbo wa taifa. Mfano wa matukio hayo ni uzinduzi wa meli mpya au ndege mpya. Aidha, wimbo wa taifa huimbwa katika taasisi mbalimbali kama vile, shuleni na katika vikosi vya majeshi yetu ili kukuza uzalendo. Vilevile, wimbo wa taifa huimbwa katika matukio muhimu ya kitaifa, kama vile sikukuu za kitaifa na hafla zinazohusisha viongozi wakuu wa serikali.

## Mnyama wa taifa

Je, unamfahamu mnyama wa taifa? Anaitwa nani ? Na ulimwona wapi? Mnyama wa taifa la Tanzania anaitwa twiga. Mnyama huyu hutumika kama alama kificho katika fedha ya noti ya Tanzania. Pia, hutumika pamoja na alama ya bendera ya taifa kutambulisha ndege inayomilikiwa na Serikali



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, alama ya twiga hutumika kama kielelezo cha utajiri wa maliasili iliyopo Tanzania.




*Kielelezo namba 3: Alama ya twiga katika ndege ya Tanzania*

## Nembo ya taifa la Tanzania

Je, umewahi kuiona nembo ya taifa? Ina vitu gani? Uliiona wapi? Nembo ya taifa ina jumla ya alama 13 ambazo ni: mwanamke na mwanaume, mwenge wa uhuru, pembe za ndovu, mlima Kilimanjaro, mawimbi ya bahari, bendera ya taifa, mkuki, mazao ya pamba na karafuu, jembe na shoka, ukanda wenye maneno uhuru na umoja, rangi ya njano na nyekundu. Nembo ya taifa inatumika kuonesha umiliki wa mali na nyaraka za Serikali ya Tanzania. Alama hiyo huonekana katika vitabu na machapisho mbalimbali ya serikali, hati za kusafiria nje ya nchi na mavazi ya viongozi wa juu wa kijeshi. Pia, hutumika katika mawasiliano rasmi ya kiserikali kama vile barua za kiserikali na matamko ya kiserikali. Nembo ya taifa la Tanzania hutumika pia kama muhuri wa Rais.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 22 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Fedha ya Tanzania

Alama nyingine ya kitaifa ni fedha ya Tanzania. Fedha ya Tanzania inaitwa shilingi. Fedha hutumika kwa namna mbili. Hutumika kuitambulisha Tanzania kama nchi huru. Pia, hutumika kuthamanisha vitu na mali. Fedha ya Tanzania iko katika sura mbili: noti na sarafu.

## Bendera ya Rais

Alama hii hutumika kutambulisha mamlaka rasmi ya Rais katika shughuli rasmi ambazo rais anahudhuria ndani au nje ya nchi. Vilevile, hutumika katika chombo cha usafiri anachokitumia Rais.

## Mwenge wa uhuru

Mwenge wa uhuru uliwashwa kwa mara ya kwanza juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro siku ambayo Tanganyika ilipata uhuru tarehe 9 mwezi wa 12 mwaka 1961. Mwenge huu wa uhuru hutumika kukumbuka na kuitambulisha Tanzania kama nchi huru. Hutumika pia kuonesha mshikamano wa kitaifa. Mwenge wa uhuru hutumika katika matukio ya kuzindua baadhi ya miradi ya maendeleo nchini pindi unapokimbizwa kwenye maeneo husika. Vilevile, mwenge wa uhuru hutumika kuhamasisha na kudumisha uzalendo kwa Watanzania. Wakati wa kukimbiza mwenge wa uhuru, kuna wimbo maalumu unaoimbwa ili kuwakumbusha Watanzania jukumu lao la kuulinda uhuru wao. Mbio za mwenge hufanyika mara moja kila mwaka kuzunguka nchi nzima.




*Kielelezo namba 4: Uzinduzi wa miradi ya maendeleo wakati wa mbio za mwenge wa uhuru.*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Hebu imba, kisha tafakari maudhui ya wimbo huu wa "Kuwasha mwenge."

### Kuwasha mwenge

"Sisi tumekwisha kuwasha Mwenge,

Tumekwisha kuwasha Mwenge,

Na kuuweka juu ya mlima,

Mlima Kilimanjaro.

*Kuwasha Mwenge,*

*Kuwasha Mwenge,*

*Na kuuweka Kilimanjaro.*

Umulike hata nje ya mipaka yetu, ulete tumaini,

Pale ambapo hakuna matumaini,

Upendo mahali ambapo pana chuki,

Na heshima ambapo pamejaa dharau."

## Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Je, umewahi kuiona katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Je, umewahi kuisoma? Katiba ni sheria, kanuni na taratibu zinazotumika kuendesha shughuli za nchi, chama au kikundi cha watu wenye malengo yanayofanana. Tanzania tunatumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo ni sheria mama inayoainisha misingi mikuu ya kisiasa na kuonesha muundo, madaraka na majukumu ya serikali. Katiba huonesha pia haki na wajibu wa raia wa Tanzania.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni alama mojawapo miongoni mwa alama zinazolitambulisha taifa letu. Katiba hutumika kuhifadhi na kulinda sheria zote zinazotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inaeleza bayana mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili mikuu mitatu ya dola ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Katiba hutumika wakati viongozi wanapoapishwa baada ya kuteuliwa na kuchaguliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Wanaapishwa na katiba ili kuitetea na kuilinda katiba hiyo. Vilevile, katiba hueleza bayana

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

madaraka na mipaka ya viongozi ili kuepusha migogoro na matumizi mabaya ya madaraka. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huhifadhi sheria zinazotetea maslahi na haki za binadamu.

## Ramani ya Tanzania

Alama hii hutumika kutambulisha na kuonesha mipaka ya nchi yetu na nchi nyingine zilizo jirani yetu. Upande wa mashariki,Tanzania inapakana na Bahari ya Hindi, upande wa magharibi inapakana na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Rwanda. Upande wa kaskazini Tanzania imepakana na nchi za Kenya na Uganda. Upande wa kusini inapakana na nchi za Malawi, Msumbiji na Zambia.

### Zoezi la 5

1. Tanzania ina alama ngapi za taifa? Zitaje.
2. Nembo ya taifa ina alama ngapi? Zitaje.
3. Bainisha aina mbili za fedha ya Tanzania.
4. Taja faida ya mwenge wa uhuru nchini Tanzania.
5. Orodhesha tunu za taifa la Tanzania.
6. Eleza manufaa ya katiba ya nchi kwa Watanzania.
7. Ni mambo gani ya uzalendo kwa Mtanzania yanayo hamasishwa kwenye wimbo wa “kuwasha mwenge”?

### Kazi ya Kufanya

Andika wimbo wa taifa la Tanzania, kisha orodhesha tunu zilizotajwa katika wimbo huo.

## Sikukuu za kitaifa

Je, unazifahamu sikukuu gani za kitaifa? Kama mwanafunzi umewahi kushiriki sikukuu gani za kitaifa? Sikukuu za kitaifa ni zile siku ambazo zinaadhimishwa kitaifa kila mwaka, ili kukumbuka matukio muhimu ya



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kitaifa. Ifuatayo ni orodha ya sikukuu zinazoadhimishwa kitaifa nchini Tanzania:

| Tarehe | Sikukuu |
|---|---|
| 1 Januari | Mwaka Mpya |
| 12 Januari | Kumbukumbu ya siku ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| 07 Aprili | Kumbukumbu ya kifo cha Rais wa kwanza wa Zanzibar (Sheikh Abeid Aman Karume) |
| 26 Aprili | Muungano wa Tanganyika na Zanzibar |
| 01 Mei | Siku ya wafanyakazi duniani |
| 07 Julai | Maonesho ya biashara ya kimataifa |
| 08 Agosti | Siku ya wakulima Tanzania |
| 14 Oktoba | Kumbukumbu ya kifo cha Rais wa kwanza wa Tanzania (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere) |
| 09 Disemba | Uhuru wa Tanganyika |

*Jedwali namba 2: Sikukuu za Kitaifa*

Pia, kuna sikukuu nyingine za dini ya Wakristo kama vile Krismas, Ijumaa Kuu, Pasaka na Jumatatu ya Pasaka. Vilevile, kuna sikukuu za Waislamu, mfano Eid - El Fitri, Eid - El Haji na Maulid.

## Umuhimu wa sikukuu za kitaifa

Sikukuu za kitaifa hutumika kuenzi matukio ya kitaifa na kudumisha ujumbe ulio katika matukio hayo. Sikukuu za kitaifa, hutoa fursa kwa viongozi kueleza mafanikio na changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi. Wakati wa maadhimisho ya sikukuu hizo, viongozi hutumia nafasi hizo kuchanganua na kufafanua mambo ya kitaifa na kutafakari mwelekeo wa nchi. Pia, hutoa elimu mbalimbali kwa wananchi kuhusu mambo yanayohusu maendeleo ya nchi yao. Kwa mfano, wakati wa sherehe za wakulima ambazo huadhimishwa tarehe 8 mwezi wa 8 kila mwaka, viongozi wetu wa kitaifa huwahamasisha wakulima kutembelea maonesho mbalimbali yatakayo wasaidia wakulima kupata mbinu na njia za kisasa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 26 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

za kuboresha kilimo na ufugaji. Vilevile, sikukuu hizi huwasaidia wananchi kupata fursa ya kuwasiliana na viongozi wao. Aidha, kwa kupitia sikukuu hizi wananchi hupata fursa ya kusherehekea mafanikio na kutafakari changamoto mbalimbali. Mfano, katika sikukuu ya Mei Mosi wafanyakazi hutoa dukuduku zao kuhusu changamoto zinazowakabili.

## Zoezi la 6

1. Eleza umuhimu wa kuadhimisha sikukuu zifuatazo:
   (a) Mapinduzi ya Zanzibar
   (b) Muungano wa Tanganyika na Zanzibar
   (c) Uhuru wa Tanganyika
2. Ni faida gani wafanyakazi wanapata kwa kusherehekea Sikukuu ya Wafanyakazi?
3. Sikukuu ya Wakulima ina faida zipi kwa taifa letu?

## Kazi ya Kufanya

Andika taarifa fupi kuhusu jinsi ulivyoshiriki katika moja ya sikukuu za kitaifa na kisha wasilisha daftari lako kwa mwalimu wa somo.

## Zoezi la 7

**Chagua jibu sahihi kwa kuandika herufi ya jibu katika kisanduku.**

1. Ni ishara gani inayoonesha kwamba taifa limepatwa na msiba mkubwa?
   (a) bendera zote kupepea nusu mlingoti
   (b) bendera ya taifa kupepea nusu mlingoti
   (c) bendera ya taifa kutopandishwa kabisa siku ya tukio

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Vyombo vya usafiri kama vile meli na ndege huwa na alama ya bendera ya taifa la Tanzania. Hii humaanisha:
   (a) vinatoka Tanzania au ni mali ya Tanzania
   (b) vinatumika Tanzania tu
   (c) hutumiwa na watanzania tu wanapokuwa nje ya Tanzania.

3. Alama ambayo hutumika kuonesha umiliki wa mali na nyaraka za serikali tu ni:
   (a) picha ya makamu wa Rais
   (b) bendera ya taifa
   (c) nembo ya taifa

4. Chimbuko la sheria zote nchini Tanzania ni:
   (a) fedha ya Tanzania
   (b) katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania
   (c) vyama vya siasa

5. Ni siku ambazo viongozi hupata fursa kueleza mafanikio na changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi:
   (a) siku za kukimbizwa mwenge wa uhuru tu
   (b) sikukuu ya Mapinduzi ya Zanzibar tu
   (c) sikukuu za kitaifa

6. Umuhimu wa bendera ya Rais ni:
   (a) kutembelea katika ziara mbalimbali tu
   (b) kuonesha mamlaka ya Rais
   (c) kuhamasisha mwenge wa uhuru

7. Rangi ya bluu iliyopo katika bendera ya taifa huwakilisha:
   (a) watanzania
   (b) madini
   (c) maji ambayo ni mito, maziwa na bahari nchini Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Wimbo wa taifa huimbwa kwenye matukio yapi kati ya haya?
   (a) kwenye matukio muhimu ya kitaifa, taasisi mbalimbali na timu ya taifa inapocheza na timu nyingine ya nje ya nchi yetu.
   (b) wakati shughuli mahakamani zinapoanza
   (c) wakati Rais anahutubia tu

9. Mwenge wa uhuru uliwashwa kwa mara ya kwanza lini?
   (a) 9/12/1962
   (b) 9/12/1961
   (c) 26/4/1964

10. Baadhi ya alama zipatikanazo kwenye fedha ya Tanzania ni.
   (a) twiga, tembo, nembo ya taifa na sura ya rais
   (b) nembo, nyumbu na kifaru
   (c) mwenge, twiga na sokwe

11. Maana ya utamaduni ni:
   (a) ushabiki wa kitu au jambo unalolipenda
   (b) mtindo wa jumla wa maisha ya watu katika jamii au taifa fulani
   (c) shughuli za asili zinazofanywa na watu.

12. Mambo yanayoifanya shule kuwa na sifa nzuri ni:
   (a) kupiga bendi ya shule vizuri ili wanafuzi wa shule za jirani watamani kuhamia
   (b) mazingira safi, unadhifu wa wanafunzi, matokeo mazuri katika mitihani na nidhamu nzuri
   (c) kuwahi kwenda shuleni na kuwahi kurudi nyumbani tu

13. Mifano ya vikundi vinavyoweza kuundwa shuleni ni kama:
   (a) skauti, klabu za mazingira, klabu ya TAKUKURU, klabu za masomo
   (b) upatu, ushirika na vyama vya siasa
   (c) skauti, singeli na ngoma za asili

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 29 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

14. Umoja, uzalendo, ushirikiano, upendo, heshima, utu ni mifano ya tunu za taifa letu, hivyo yatupasa:
    (a) kuziandika na kuzisoma kila mara
    (b) kuwahamasisha wananchi wote wapate kuzisoma
    (c) kuzithamini na kuzienzi

15. Zipi kati ya hizi ni mila zisizofaa katika jamii?
    (a) kufanya kazi kwa ushirikiano
    (b) kuwakeketa wasichana
    (c) kuhamasisha wanaume na wanawake kushirikiana kufanya kazi za nyumbani ili kujiongezea kipato

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Dola | chombo chenye mamlaka ya kuendesha utawala au siasa ya nchi |
| Dukuduku | machungu, wasiwasi au mfundo unaomsonga mtu moyoni |
| Dumisha | kuendeleza jambo |
| Katiba | jumla ya kanuni, taratibu au sheria ambazo huwezesha serikali itawale au chama au kampuni iendeshe shughuli zake |
| Maslahi | manufaa au faida aipatayo mtu baada ya kufanya kazi, biashara au kumaliza tendo lolote |
| Mhimili | nguzo, kitu kinachozuia kingine kisianguke |
| Minajili | kwa ajili ya |
| Thamini | kukipa kitu hadhi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Muundo wa uongozi serikalini

Ulipokuwa darasa la nne ulijifunza muundo wa serikali ya kijiji na mtaa. Katika sura hii, utajifunza muundo wa uongozi wa serikali ngazi ya kata, wilaya na mkoa. Pia, utajifunza mgawanyo wa kazi, wajibu, pamoja na umuhimu wa kuwa na muundo wa uongozi serikalini.

### Dhana ya uongozi serikalini

Uongozi serikalini ni mamlaka yaliyoundwa kisheria iliyomo kwenye katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yenye madaraka kamili ya kujiendesha. Uongozi serikalini unaanzia ngazi ya chini kabisa ya kitongoji mpaka ngazi ya kitaifa. Pia, uongozi ni chombo cha juu chenye kutoa sera na maamuzi muhimu ya maendeleo.

### Muundo wa utawala kata

Viongozi wa kata wanaongoza wananchi katika ngazi ya kata husika.

**Diwani:** Ndiye kiongozi anayechaguliwa na wananchi. Huchaguliwa wakati wa uchaguzi mkuu wa rais na wabunge kila baada ya miaka mitano. Huyu ndiye kiongozi mkuu wa kisiasa katika kata na ni mwenyekiti wa vikao mbalimbali vinavyoendeshwa katika kata.

**Ofisa mtendaji wa kata:** Ni mtendaji mkuu wa shughuli zote za kata. Ni mwajiriwa wa serikali. Huwa ni katibu wa vikao vyote vya kata. Kipindi cha uchaguzi husimamia shughuli zote za uchaguzi katika kata yake. Pia, ni mwakilishi wa mkurugenzi katika kata na msimamizi wa huduma za jamii katika kata.

Katika muundo wa utawala katika kata, wenyeviti wa vijiji na maofisa watendaji wa mitaa au vijiji ni miongoni mwa viongozi wanaounda wanaounda utawala wa kata.

Kwa hiyo, kuna aina kuu nne za viongozi katika kata:

1. Diwani wa kata na diwani wa viti maalumu
2. Ofisa mtendaji wa kata
3. Wakuu wa idara, mfano biashara, elimu na kilimo
4. Wenyeviti wa vijiji au mitaa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 31 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Muundo wa utawala katika kata




*Kielelezo namba 1: Muundo wa utawala ngazi ya kata*

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 1**

1. Taja idara za utawala katika kata.
2. Nani kiongozi mkuu wa idara zote hizi?
3. Ofisa mtendaji wa kata anafanya kazi chini ya kiongozi gani?
4. Je, katika muundo wa utawala katika kata, ni viongozi gani wako katika ngazi ya chini kabisa ya madaraka?
5. Eleza kwa ufupi majukumu makuu ya uongozi wa kata.
6. Nini tofauti ya uongozi na utawala?



URAIA NA MAADILI STD V .indd 32 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu tofauti ya muundo wa uongozi wa serikali ya kijiji au mtaa na ule wa kata.

## Kazi na wajibu wa viongozi wa kata

Je, neno wajibu lina maana gani? Wajibu ni kazi au jambo ambalo linamlazimu mtu kulitimiza na hakuna hiari katika kulifanya. Kwa ujumla, wajibu na utendaji kazi mzuri wa viongozi wa kata, ni muhimu kwa sababu husaidia kuwahamasisha wananchi kushiriki katika maendeleo ya kata yao. Husimamia na kutekeleza sera na mipango utawala wa kata katika ngazi ya vitongoji, vijiji au mitaa. Ni wajibu wa viongozi wa kata kusaidia kutafuta mbinu za kutatua changamoto za wananchi katika kata zao. Pia, kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali kutoka mamlaka za juu serikalini.

## Soma utambulisho huu wa viongozi wa kata, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Diwani wa kata:** Mimi ni diwani kiongozi mkuu wa kisiasa katika kata. Ni mwakilishi mkuu wa wananchi katika ngazi ya wilaya. Pia, ni mwenyekiti wa vikao mbalimbali vinavyoendeshwa katika kata. Vilevile, ninashirikiana na ofisa mtendaji wa kata, kusimamia majukumu na miradi mbalimbali ya maendeleo ya kata yangu. Zaidi ya hayo, ninamshauri Mbunge kuhusu masuala ya maendeleo ya kata yangu. Pia, ni mjumbe wa baraza la madiwani katika halmashauri au manispaa inayohusika.

**Diwani viti maalumu:** Mimi pia ni diwani. Ninachaguliwa na mkutano mkuu wa chama changu cha siasa. Ni mjumbe wa vikao vya kamati ya maendeleo katika kata yangu. Ninashirikiana na diwani wa kuchaguliwa katika kutekeleza majukumu yangu. Pia, ni mjumbe wa baraza la madiwani katika halmashauri au manispaa inayohusika.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 33 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ofisa mtendaji wa kata:** Mimi ni ofisa mtendaji wa kata. Ninasimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika kata. Pia, ni katibu wa vikao vyote vya kata. Ninamwakilisha mkurugenzi wa halmashauri au manispaa katika kata. Vilevile, ninasimamia amani na usalama wa raia na mali zao katika kata nikisaidiwa na vyombo vya dola.

**Ofisa elimu kata:** Mimi ni ofisa elimu kata. Ninashughulikia masuala yote ya elimu ya msingi, sekondari na elimu ya watu wazima. Mimi ni kiungo kati ya shule zilizopo katika kata na idara ya elimu katika halmashauri ya wilaya au manispaa. Ninatekeleza maagizo na taratibu zinazohusu elimu kutoka mamlaka za juu za serikali katika kata.

**Ofisa maendeleo jamii wa kata:** Mimi ni ofisa maendeleo jamii wa kata. Kwanza, ninahamasisha, ninaratibu na kusimamia maendeleo katika kata. Pia, ninaelimisha jamii dhidi ya mila na desturi potofu zinazoweza kukwamisha maendeleo ya jamii. Tena, ninawaelimisha wananchi umuhimu wa lishe bora na utunzaji wa mazingira katika kata.

Pili, ninahamasisha kuhusu usawa wa jinsia na maendeleo. Tatu, ninashirikiana na jamii kuibua miradi ya maendeleo, kuiratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango katika kata. Mwisho, ninamwakilisha ofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri ya wilaya au manispaa katika kata. Kwa hiyo, mimi ni kiungo kati ya kata na halmashauri ya wilaya katika masuala ya maendeleo ya jamii.

**Ofisa kilimo na mifugo wa kata:** Mimi ni mwajiriwa wa halmashauri ya wilaya.Pia, ninajulikana kama ofisa ugani. Majukumu yangu ni kuhakikisha kuwa taratibu za kilimo na ufugaji bora zinazingatiwa katika kata.

**Ofisa maliasili wa kata:** Mimi ni ofisa maliasili wa kata. Ni msimamizi mkuu wa maliasili katika kata. Ninashirikiana na wananchi kupambana na waharibifu wa mazingira kwa kuwaelimisha umuhimu wa kutunza mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ofisa afya wa kata:** Mimi ni ofisa afya wa kata. Ninawaelimisha wananchi jinsi ya kujikinga na magonjwa na umuhimu wa chanjo kwa watoto. Pia, naelimisha wananchi umuhimu wa kuwa na afya bora kwa kuzingatia usafi wa mazingira katika kata.

## Zoezi la 2

1. Taja wakuu wa idara katika ngazi ya kata.
2. Je, ofisa afya wa kata ana kazi gani?
3. Nani ni kiongozi wa kisiasa katika kata?
4. Nani husimamia na kuratibu shughuli za maendeleo katika kata?
5. Je, kazi za ofisa elimu kata ni zipi?
6. Tunapiga vita mila na desturi potofu katika jamii. Je, ni ofisa yupi katika ngazi ya kata anayeweza kutusaidia kupiga vita mila na desturi potofu?
7. Je, ofisa ugani wa kata ana kazi zipi?

## Kazi ya Kufanya

Andika kwenye daftari lako tofauti kati ya diwani wa kata na diwani wa viti maalumu katika kata yako. Baada ya kumaliza wasilisha daftari lako kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 35 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Muundo wa uongozi wa wilaya

Muundo wa uongozi katika wilaya umegawanyika katika sehemu kuu mbili: serikali ya wilaya na halmashauri ya wilaya. Serikali ya wilaya inawakilisha serikali kuu na halmashauri ya wilaya inawakilisha serikali za mitaa.

Serikali ya wilaya inajumuisha mkuu wa wilaya, katibu tawala wa wilaya na maofisa tarafa. Mkuu wa wilaya na Katibu tawala wa wilaya huteuliwa na Rais.

**Muundo wa serikali ya wilaya**




*Kielelezo namba 2: Muundo wa serikali ya wilaya*

### Mkuu wa wilaya

Mkuu wa wilaya ni kiongozi mkuu wa wilaya. Humsaidia mkuu wa mkoa katika kuzisimamia halmashauri za wilaya. Mkuu wa wilaya ni kiongozi wa wilaya kwa upande wa serikali kuu katika wilaya yake. Huteuliwa na Rais na kuapishwa na mkuu wa mkoa husika kwa niaba ya Rais.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Majukumu ya mkuu wa wilaya ni pamoja na kuhakikisha kuwa kuna utulivu na usalama katika wilaya. Mkuu wa wilaya ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama katika wilaya na ni mjumbe wa kamati ya ushauri ya mkoa. Mkuu wa wilaya pia, ni mwenyekiti wa kamati mbalimbali zinazoundwa ndani ya wilaya. Hufungisha ndoa za serikali na vilevile, huziwezesha na kuzisaidia serikali za mitaa ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Mkuu wa wilaya huchunguza uhalali wa matendo au uamuzi wa serikali za mitaa zilizoko wilayani kwake ili kuhakikisha kuwa maslahi ya wananchi na taifa yanazingatiwa katika mipango na utoaji wa uamuzi.

## Kamati ya ushauri ya wilaya

Hii ni kamati ya juu katika wilaya inayojadili na kufanya uamuzi kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo katika wilaya. Vikao vya kamati hiyo ni vya kisheria na hufanyika mara mbili kwa mwaka. Kamati hii inaundwa na wajumbe kama vile mkuu wa wilaya, ambaye ni mwenyekiti wa kamati, katibu tawala wa wilaya ambaye ni katibu wa kamati, wabunge wote katika wilaya, wenyeviti wote wa halmashauri, viongozi wa vyama vya siasa katika wilaya, wataalamu wote wa idara katika wilaya na kamati ya ulinzi na usalama katika wilaya.

## Katibu tawala wa wilaya

Katibu tawala wa wilaya ni mteule wa Rais. Moja ya kazi zake ni kumshauri mkuu wa wilaya kuhusu ulinzi na usalama pamoja na utekelezaji wa majukumu ya sherehe na dhifa za kitaifa. Pia, humshauri mkuu wa wilaya kusikiliza malalamiko ya wananchi, masuala yanayohusu uwekaji wa mazingira bora ya kuziwezesha halmashauri za wilaya kutekeleza majukumu yake. Yeye ni kiongozi mkuu wa utawala katika ngazi ya wilaya. Ni msajili wa vizazi, vifo na ndoa za kiserikali. Vilevile, hushiriki kuandaa makadirio ya mapato na matumizi ya wilaya, hushughulikia masuala ya itifaki wilayani na kuratibu harakati za kupambana na dharura za maafa wilayani.

## Ofisa tarafa

Ofisa tarafa ni kiongozi anayesimamia majukumu ya serikali kuu na serikali za mitaa katika tarafa yake. Huwajibika katika sehemu mbili, serikali kuu, yaani kwa katibu tawala wa wilaya; na serikali za mitaa, yaani kwa mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya. Majukumu ya ofisa tarafa ni pamoja na kusimamia utendaji wa maofisa watendaji wa kata, vijiji, vitongoji na mitaa katika tarafa yake. Pia, huwasaidia wakurugenzi wa mamlaka wa



URAIA NA MAADILI STD V .indd 37 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

serikali za mitaa katika kusimamia utekelezaji wa maendeleo katika tarafa yake. Vilevile, ofisa tarafa hushiriki na kutoa ushauri kuhusu upangaji wa mipango ya maendeleo katika tarafa yake. Huyu ni mwajiriwa wa serikali ya wilaya husika.

### Uongozi wa halmashauri ya wilaya au manispaa

Halmashauri za wilaya, miji au manispaa zinahusika na kubuni na kupanga mipango ya maendeleo katika maeneo yao. Halmashauri hizo hufanya maandalizi ya utekelezaji wa miradi kuanzia miradi ya kijiji, kata na wilaya husika. Kamati ya maendeleo ya wilaya inaunganisha mipango yote ya maendeleo katika wilaya.

### Baraza la madiwani la halmashauri

Baraza la madiwani ndicho chombo cha juu cha uongozi katika halmashauri ya wilaya au manispaa. Baraza hili huundwa na madiwani wa kuchaguliwa kutoka kila kata na pia madiwani wa kuteuliwa ambao ni wajumbe wa vikao vya baraza la madiwani. Kikao cha baraza la madiwani cha halmashauri ya wilaya au manispaa huongozwa na mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya. Kiongozi huyu hupatikana kwa kuchaguliwa kutoka miongoni mwa madiwani wa kata mbalimbali zinazounda halmashauri husika. Mkurugenzi mtendaji wa wilaya ndiye katibu wa vikao vya baraza la madiwani.

Baraza la madiwani hutunga sheria ndogondogo kulingana na mazingira ya halmashauri inayohusika. Pia, husimamia mapato na matumizi ya fedha za halmashauri ya wilaya au manispaa. Vilevile, huhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma muhimu za jamii kama vile afya, umeme, maji, barabara na elimu. Hali kadhalika, baraza hili humshauri mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya au manispaa katika mambo mbalimbali ya maendeleo kwenye wilaya. Ni kiungo muhimu cha kuchochea maendeleo ya wananchi katika tarafa, kata, vijiji na vitongoji au mitaa wanayoongoza.

Muundo wa uongozi wa halmashauri ya wilaya au manispaa umegawanyika katika makundi makuu matatu: Baraza la madiwani, Mkurugenzi mtendaji wa wilaya, Idara na vitengo mbalimbali vya wataalamu katika halmashauri husika. Katika muundo wa uongozi huu, kuna jumla ya vitengo sita na idara 13 kama zilivyoainishwa katika kielelezo namba 3. Kwa mujibu wa taratibu na sheria za serikali za mitaa, idara na vitengo vyote vilivyoanishwa katika muundo huu, vina mamlaka zinazolingana. Kwa maneno mengine ni kwamba, watumishi wote hawa huwajibika kwa mkurugenzi mtendaji wa wilaya au manispaa.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 38 17/08/2021 11:18

## Muundo wa halmashauri ya wilaya au manispaa




*Kielelezo namba 3: Muundo wa uongozi wa halmashauri ya wilaya*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



URAIA NA MAADILI STD V .indd 39
17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya

Ni kiongozi mkuu wa halmashauri mwenye dhamana ya kisiasa. Dhamana hii humfanya kuwa kioo ndani na nje ya halmashauri yake. Majukumu ya mwenyekiti wa halmashauri ni pamoja na kuwa mwenyekiti wa baraza la madiwani na kamati ya kudumu ya fedha na mipango au utawala. Yeye, ni mtia saini na lakiri au muhuri katika nyaraka zote rasmi za halmashauri. Pia, hudhibiti na kuongoza mikutano ya baraza la madiwani, ili liweze kufanya uamuzi wenye maslahi kwa wananchi wote wa halmashauri. Vilevile, hutenda haki kwa madiwani wote bila kujali itikadi za kisiasa, dini, rangi au kabila.

Mwenyekiti wa halmashauri anatakiwa kupewa ofisi ambayo ataitumia kukutana na wananchi wote wenye shida, kero na maoni ya kuboresha utendaji wa halmashauri. Anatakiwa kukutana na wananchi mara mbili kwa wiki. Ratiba ya siku mbili ni lazima iwe wazi na ifahamike kwa wananchi wote. Aidha, mwenyekiti wa halmashauri akitaka kutembelea halmashauri yake katika harakati za kuhimiza maendeleo, atalazimika kufanya kazi hiyo katika siku hizo mbili tu zilizoruhusiwa kisheria na siyo vinginevyo.

## Mkurugenzi wa halmashauri

Mkurugenzi wa halmashauri ndiye mtendaji mkuu na ofisa masuuli wa halmashauri. Anawajibika kuhakikisha kuwa majukumu na kazi zote za halmashauri zinatekelezwa kwa mujibu wa sheria na kwa kuzingatia maelekezo na mipango ya halmashauri inayohusika.

Mkurugenzi wa halmashauri ni katibu wa vikao vya baraza la madiwani. Huweka saini nyaraka mbalimbali za halmashauri, kama vile mikataba kwa niaba ya wananchi wa halmashauri inayohusika, iwe ni kwa ajili ya uwekezaji ama miradi mbalimbali ya maendeleo. Hupokea na kusikiliza matatizo, changamoto, au malalamiko ya wananchi kwenye halmashauri husika. Ana wajibu wa kuzipatia majibu ya kina changamoto hizo, kwa kuwaagiza wasaidizi wake kuhakikisha kuwa matatizo ya wananchi yanapata ufumbuzi wa haraka. Huitisha na kuendesha mikutano ya menejimenti, ambapo mambo mbalimbali ya halmashauri yatajadiliwa na kutolewa uamuzi. Mkurugenzi pia ni ofisa uhusiano na msemaji mkuu wa uamuzi wa halmashauri. Anawajibika kuutetea uamuzi na maazimio ya halmashauri. Iwapo atapotosha maazimio hayo ni yeye atakayechukuliwa hatua. Ni mwenyekiti wa tume ya uchaguzi katika majimbo yaliyopo chini ya halmashauri yake. Yeye huhusika na kuratibu zoezi zima la uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu katika halmashauri yake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi na wajibu wa wakuu wa idara**

Wakuu wa idara katika ngazi ya halmashauri huajiriwa na halmashauri inayohusika. Katika ngazi ya wilaya, wakuu hao ni pamoja na Ofisa elimu wa wilaya, Ofisa maendeleo ya jamii, Ofisa kilimo na mifugo, Ofisa maliasili, Ofisa biashara na Ofisa afya. Hawa ni wataalamu ambao kazi zao kubwa ni kusimamia shughuli zinazohusiana na kada zao. Humshauri mkurugenzi wa halmashauri na huwajibika kwa mkurugenzi juu ya masuala yote ya maeneo yao ya utendaji.

**Ofisa elimu wa wilaya:** Ofisa elimu wa wilaya hushughulikia masuala yote ya elimu ya msingi, sekondari na elimu ya watu wazima katika halmashauri yake. Pia, ni kiunganishi kati ya shule za wilaya yake na idara ya elimu katika mkoa. Jukumu lake lingine ni kutekeleza maagizo na taratibu zinazohusu elimu pamoja na kusimamia maslahi na wajibu wa watumishi wote walio chini yake au waliopo katika kada ya elimu.

**Ofisa maendeleo ya jamii wa wilaya:** Husimamia na kuratibu mipango ya maendeleo ya jamii katika wilaya ili kufikia malengo waliyojiwekea. Huratibu shughuli za maendeleo ya jamii zikiwemo za wanawake na watoto kwa kuzingatia jinsia. Pia, huwezesha jamii kushiriki katika kubuni, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini mipango na kujua miradi yao ya maendeleo. Ofisa maendeleo ya jamii wa wilaya anaratibu shughuli za kupambana na magonjwa, mfano, UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu.

**Ofisa kilimo na mifugo wa wilaya:** Huhakikisha kilimo na ufugaji bora vinatiliwa mkazo katika wilaya zao. Hudhibiti visumbufu vya mimea na mazao ili kuwasaidia wakulima katika wilaya yake kulima kilimo chenye tija. Vilevile, huendesha mafunzo ya wataalamu wa kilimo na ufugaji, pamoja na kufanya ukaguzi wa ubora na matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo na ufugaji. Huwajibika pia kuelekeza njia za kilimo na ufugaji bora wenye tija.

**Ofisa maliasili wa wilaya:** Ni msimamizi wa maliasili wa wilaya. Husimamia utunzaji wa maliasili kama vile misitu, wanyama na mazingira kwa ujumla. Pia, hupambana na wahalifu wa mazingira katika wilaya yake na kuwaelimisha wananchi juu ya utunzaji mzuri wa mazingira katika wilaya yao.

**Ofisa biashara wa wilaya:** Anasimamia na kubuni miradi ya biashara katika wilaya yake. Yeye anawaelimisha wananchi jinsi ya kuanzisha biashara na kuendesha vyama vya ushirika. Pia, ana jukumu la kuwashauri na kuwahamasisha wananchi wenye uwezo wa kuanzisha viwanda vidogovidogo vitakavyoweza kuajiri watu wengine ndani na nje

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 41 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya wilaya yake. Yeye ndiye mwenye dhamana ya kuwaelimisha wananchi na wafanyabiashara kwa ujumla umuhimu wa kuwa na leseni za kufanya biashara na kulipa kodi stahiki.

**Ofisa afya wa wilaya:** Ana jukumu la kuwaelimisha wananchi jinsi ya kujikinga na magonjwa na kuhusu afya ya jamii pamoja na chanjo kwa watoto. Vilevile, ana wajibu wa kuelimisha wananchi faida za usafi wa mazingira kwa afya bora. Pia, husimamia sheria na kanuni za afya katika wilaya.

**Zoezi la 4**

1. Wakuu wa idara katika halmashauri wana umuhimu gani?
2. Ni kiongozi gani ana wajibu wa kusajili vizazi na vifo katika ngazi ya wilaya?
3. Taja majukumu ya mkuu wa wilaya

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako kuhusu majukumu ya kitengo cha TEHAMA katika wilaya. Andika kwenye daftari lako na liwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Muundo wa serikali ya mkoa

Serikali ya mkoa ni chombo cha utekelezaji cha serikali za mitaa na serikali kuu katika mkoa husika. Kupitia kamati ya maendeleo ya mkoa, serikali inaeleza na kutafsiri sera na maagizo mengine ya taifa. Serikali ya mkoa huongozwa na mkuu wa mkoa. Muundo wa serikali ya mkoa unajumuisha mkuu wa mkoa, katibu tawala wa mkoa, wakuu wa vitengo kama vile TEHAMA, fedha na mahesabu, usimamizi wa manunuzi na huduma za kisheria.

Pia, kuna idara zinazosimamia majukumu mbalimbali kama vile mipango na uratibu, afya na ustawi wa jamii (ambayo inahusisha hospitali ya mkoa), uchumi na sekta za uzalishaji na idara ya elimu. Idara nyingine ni utawala na usimamizi wa rasilimali watu, huduma za maji, miundombinu na usimamizi wa mamlaka ya serikali za mitaa.

FOR ONLINE USE ONLY

## Muundo wa uongozi wa serikali ya mkoa




*Kielelezo namba 4: Muundo wa uongozi wa serikali ya mkoa*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



URAIA NA MAADILI STD V .indd 43
17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Soma majigambo yafuatayo, kisha kamilisha zoezi linalofuata.

**Mkuu wa mkoa:** Mimi ni mteule wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamwakilisha yeye hapa mkoani. Ni msimamizi wa mambo yote hapa. Ninawaapisha wakuu wa wilaya kwa niaba yake. Vilevile, mimi ni mwenyikiti wa kamati ya ulinzi na usalama. Pia, mimi ni mwenyekiti wa kamati ya ushauri ya mkoa.

**Kamati ya ushauri ya mkoa:** Mimi ni kikao cha juu cha mkoa kinachojadili na kutoa uamuzi kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo katika mkoa. Kikao hiki kipo kisheria na hufanyika mara mbili kwa mwaka. Pia, nimeundwa na wajumbe kama vile mkuu wa mkoa ambaye ni mwenyekiti wa vikao vya kamati, katibu tawala wa mkoa ambaye ni katibu wa vikao vya kamati ya mkoa na wabunge wote katika mkoa na viongozi wa vyama vya siasa katika mkoa. Vilevile, kuna wakuu wa wilaya wote katika mkoa, mameya na wenyeviti wa halmashauri, wakurugenzi wa halmashauri, wataalamu wote wa idara katika ngazi ya mkoa na kamati ya ulinzi na usalama katika mkoa.

**Katibu tawala wa mkoa:** Mimi ninaratibu shughuli zote za utawala kwenye sekretarieti ya mkoa. Ni mshauri mkuu wa mkuu wa mkoa katika masuala ya sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za serikali za mitaa. Ninawajibika kwa fedha zote za serikali zinazoletwa mkoani na zile zinazokusanywa kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato. Pia, ninapokea na kuchambua takwimu na taarifa za utekelezaji zinazotoka kwenye halmashauri na mashirika mbalimbali.

**Mkaguzi wa ndani wa mkoa:** Mimi ni mtendaji mkuu katika kitengo cha ukaguzi wa ndani hapa mkoani. Ninasimamia ukaguzi wa fedha na mali za serikali za ngazi ya mkoa, nikishirikiana na wakaguzi wa nje ya mkoa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ninaandaa na kutoa taarifa za ukaguzi wa manunuzi na matumizi ya fedha za serikali hapa mkoani.

**Ofisa ugavi mkuu:** Kazi yangu ni kusimamia manunuzi yote yanayofanywa na ofisi ya mkuu wa mkoa. Ninanunua vifaa mbalimbali kama vile vipuri vya magari na kuandaa na kutoa taarifa ya ugavi wa vifaa mbalimbali katika serikali ya mkoa.

**Katibu tawala msaidizi-Afya:** Mimi ninasimamia sera ya afya na masuala yanayohusu afya na ustawi wa jamii katika mkoa. Ninashirikiana na waganga wakuu wa hospitali za wilaya. Ninamshauri mkuu wa mkoa katika masuala ya afya na ustawi wa jamii.

**Mhasibu wa mkoa:** Mimi ni msimamizi na mdhibiti mkuu wa masuala ya fedha za serikali mkoani. Vilevile, ninaandaa na kutoa taarifa za fedha za serikali.

**Katibu tawala msaidizi-Elimu:** Mimi ninaratibu masuala yote ya elimu katika mkoa, nikishirikiana na maofisa elimu wa wilaya. Vilevile, ni msimamzi mkuu wa mitihani ya taifa na elimu ya watu wazima katika mkoa.

**Kamanda wa polisi wa mkoa:** Mimi ninasimamia vikosi vya polisi kwa ajili ya usalama wa raia na mali zao kwa kushirikiana na vikosi vingine ya usalama katika mkoa.

## Umuhimu wa kuwa na muundo wa uongozi serikalini

Muundo wa uongozi serikalini unasaidia kujua wajibu wa viongozi. Unasaidia kujua nani anawajibika kwa nani. Pia, muundo unasaidia kurahisisha utekelezaji wa majukumu. Vilevile, unasaidia kuweka mipaka ya utendaji wa kazi miongoni mwa viongozi serikalini. Huwezesha kufanya tathmini ya malengo ya jumla katika sekta zote za umma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Orodhesha idara mbalimbali zilizopo katika uongozi ngazi ya mkoa.
2. Taja majukumu ya ofisa wa afya wa mkoa.
3. Eleza shughuli za maendeleo zinazofanywa katika ngazi ya mkoa.
4. Eleza kwa kifupi umuhimu wa muundo wa uongozi serikalini.
5. Taja majukumu ya mkuu wa mkoa.
6. Mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya na mkurugenzi wa halmashauri hupatikanaje?

## Kazi ya Kufanya

Jadilianeni na mwalimu wa somo kuhusu changamoto zilizopo katika mkoa wako. Je, ni kwa namna gani viongozi wa mkoa na wananchi wanashirikiana kuzitatua? Andika majibu kwenye daftari na wasilisha kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 6

**Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku.**

1. Msaidizi wa mkuu wa mkoa katika shughuli zake za utendaji ni nani?
   (a) katibu tawala msaidizi-Elimu
   (b) katibu tawala wa mkoa
   (c) mkuu wa idara ya utawala na utumishi mkoa
   (d) ofisa afya wa mkoa

2. Mwenyekiti wa halmashauri ngazi ya wilaya huongoza akina nani?
   (a) wenyeviti wa mtaa
   (b) makatibu tawala



URAIA NA MAADILI STD V .indd 46 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) madiwani wa halmashauri
(d) mtendaji wa kata

3. Katika ofisi ya kata, nani ni mtendaji mkuu?
(a) diwani
(b) ofisa mtendaji wa kata
(c) ofisa mazingira wa kata
(d) ofisa maendeleo wa kata

4. Mkurugenzi wa halmashauri anapatikanaje?
(a) kwa kupigiwa kura na madiwani
(b) kwa kuajiriwa na menejimenti ya utumishi wa umma
(c) kwa kuteuliwa na Rais
(d) kwa kupigiwa kura na wananchi katika halmashauri inayohusika

5. Katibu wa vikao vya baraza la madiwani ni nani?
(a) mwenyekiti wa halmashauri
(b) diwani wa viti maalumu
(c) katibu tawala
(d) mkurugenzi wa halmashauri

6. Wakuu wa idara katika halmashauri za wilaya huwajibika kwa nani?
(a) mkurugenzi wa halmashauri
(b) mkuu wa wilaya
(c) mkuu wa mkoa
(d) ofisa tawala wa wilaya

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

Andika neno **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi.

1. Mwenyekiti wa baraza la madiwani na kamati ya fedha na mipango ni mkurugenzi wa halmashauri. ______________
2. Jukumu la Katibu tawala msaidizi-Elimu ni kupambana na magonjwa mfano UKIMWI. _______________
3. Mkuu wa mkoa huteuliwa na Rais. _________________
4. Mkuu wa wilaya huapishwa na mkuu wa mkoa. ________
5. Katibu tawala wa wilaya ni mshauri mkuu wa Mkuu wa wilaya. _______________
6. Ofisa tarafa ana jukumu la kusimamia maofisa watendaji wa kata, vijiji na vitongoji. _______________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Diwani | ni mtu aliyechaguliwa na watu au kuteuliwa na mkutano mkuu wa chama cha siasa ili kuiwakilisha kata fulani |
| Itifaki | utaratibu maalumu wa kuwatambulisha viongozi unaotumiwa na maofisa wa serikali katika shughuli rasmi |
| Mkoa | eneo la utawala lenye wilaya kadhaa |
| Tarafa | sehemu ya kiutawala iliyo ndogo kuliko wilaya na ni kubwa kuliko kata |
| Wilaya | sehemu ya kiutawala katika mkoa ambayo ni ndogo kuliko mkoa lakini ni kubwa kuliko tarafa |
| Masuuli | kuwajibika kwa masuala yote yanayohusu uendeshaji, usimamizi na uidhinishaji wa fedha |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 48 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Kujijali na kuwajali watu wengine

Katika sura ya kwanza ulijifunza kujipenda na kuwapenda watu wengine, hasa watu wenye mahitaji maalumu, kuheshimu jinsi nyingine na kuvaa mavazi yenye staha. Katika sura hii, utajifunza kutambua na kuepuka vitendo visivyodumisha amani katika familia na shuleni. Pia, utajifunza kukemea na kutoa taarifa ya matendo yasiyokubalika. Vilevile, utajifunza kushiriki shughuli za maendeleo ya familia na kuleta uhusiano mzuri katika jamii. Aidha, utajifunza kukuza mahusiano bora na majirani zako na kushiriki katika kutatua matatizo.

### Matendo yasiyokubalika katika familia

Kuna matendo yasiyokubalika katika familia. Matendo hayo ni kama ubakaji, ulawiti, adhabu za kikatili, ajira za watoto, kufanyishwa kazi ngumu zaidi ya umri wa mtoto, kunyimwa mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi, malazi, kutosikilizwa na kunyanyaswa kijinsia.

Je, ni matendo gani yanayofanywa na wazazi au walezi katika familia yako ambayo hukiuka haki za watoto na kusababisha uvunjifu wa amani?

### Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Familia ya Bwana Soba walijaliwa kupata watoto wawili; wa kike na wa kiume. Mtoto wa kike aliitwa Aitu na mtoto wa kiume aliitwa Bosa. Aitu alikuwa na ulemavu wa macho. Bosa alikuwa anasoma darasa la tano, lakini Aitu hakupata fursa ya kupelekwa shule. Kitendo hicho kiliwaumiza sana Bosa na Aitu. Waliwaomba wazazi wao kumtafutia shule Aitu lakini Mzee Soba alikataa kabisa. Mama alijitahidi kumshawishi baba ili wamruhusu Aitu aende shule lakini alitukanwa na kudhihakiwa na hata kupigwa eti kwa sababu mwanamke hakuruhusiwa kutoa ushauri wowote kwa mwanaume. Hata hivyo Bosa alidhamiria kumsaidia dada yake.

Baada ya kuona ugomvi unaendelea baina ya wazazi wake, Bosa aliamua kuwashirikisha walimu wake mambo yanayoigusa familia yake. Walimu walimpongeza Bosa kwa kutoa taarifa na kuamua kumpa ushirikiano. Walimu waliwatembelea wazazi wa Bosa na kuwaelimisha umuhimu wa



URAIA NA MAADILI STD V .indd 49 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

elimu kwa watoto wote na kuwahamasisha kumpeleka Aitu kwenye shule za watoto wenye mahitaji maalumu.

Aitu alipoambiwa kuwa atakwenda shule, alifurahi sana. Aliwashukuru walimu, wazazi na kaka yake kwa kumsaidia yeye kwenda shuleni. Pia, aliahidi kusoma kwa bidii hadi kufikia ngazi ya chuo kikuu.

**Zoezi la 1**

1. Taja matendo yasiyokubalika katika familia yaliyobainishwa kwenye habari hii.
2. Ni tabia gani aliyoionesha Bosa kwenye habari hii ?
3. Je, tabia hiyo ya Bosa imeleta manufaa gani kwa Aitu, familia na jamii?
4. Katika jamii unamoishi watoto wenye ulemavu wanasaidiwaje kupata haki na mahitaji yao muhimu kama vile elimu, matibabu na malazi?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu matendo wanayofanyiwa wanafunzi ambayo hayakubaliki kisha andika kwenye daftari na kuliwasilisha kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kukemea matendo yasiyokubalika shuleni

Je, ni matendo gani yasiyofaa ambayo umewahi kufanyiwa shuleni kwako? Ulijisikiaje baada ya kufanyiwa matendo hayo? Baadhi ya matendo hayo ni kupewa adhabu za kuumiza, kulazimishwa kuingia kwenye uhusiano usiofaa, kama vile uhusiano wa kingono. Matendo mengine ni kudharauliwa, kudhihakiwa na kunyimwa msaada wa kimasomo au kimaisha.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 50 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

1. Umewahi kuona matendo gani ya kikatili yakifanyika shuleni au nyumbani?
2. Je, wewe ulishawahi kufanyiwa matendo ya ukatili? (Kama ndiyo, taja matendo hayo).
3. Unatoa ushauri gani kwa matendo ya ukatili uliyowahi kuyaona?
4. Je, utafanya nini ili kujiepusha kutendewa matendo kama haya ukiwa shuleni au nyumbani?

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu matendo maovu wanayofanyiwa wanafunzi. Orodhesha matendo hayo kwenye daftari lako kisha wasilisha daftari kwa mwalimu wa somo.

## Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Enna anasoma darasa la tano katika shule ya msingi Kokugu. Alikuwa anaishi na bibi yake ambaye ni mzee sana. Kabla ya kwenda shule, Enna anafanya kazi zote za nyumbani na kumwandalia bibi yake kifungua kinywa na chakula cha mchana. Hufanya hivyo kila siku hali inayomsababishia kuchelewa shuleni. Mara kwa mara mwalimu humwadhibu Enna. Anapojaribu kujieleza ili mwalimu ajue changamoto zinazomkabili, huwa hapewi nafasi. Enna huumia zaidi mara mwalimu anapomwambia ni mkorofi. Hunyanyaswa kijinsia kwa kuchapwa fimbo za makalioni na kutukanwa. Hali hiyo humfanya Enna kujisikia mnyonge mbele ya wenzake na kushuka kitaaluma. Wiki mbili zimepita bila Enna kufika shuleni kwa kuwa anaelemewa na kazi za nyumbani kwao. Hakuna mwalimu aliyefuatilia taarifa zake kwa kudhani Enna ni mwanafunzi mkorofi na jeuri.

Hata hivyo, leo asubuhi Enna amefika mapema shuleni. Mwalimu wa darasa amempongeza na kumuuliza: "Kwa nini siku za nyuma ulikuwa ukichelewa na hata kutofika shuleni?" Enna alimjibu mwalimu, "Leo nimewahi kwa kuwa jana shangazi yangu alifika nyumbani kunisaidia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

shughuli za kumhudumia bibi yangu." Mwalimu alisema, "Pole sana, kumbe siku zote ulikuwa unamhudumia bibi yako kabla ya kuja shuleni." Enna alijibu, "Ndiyo mwalimu."

**Zoezi la 3**

1. Je, Enna alikuwa na changamoto gani nyumbani?
2. Ni kwa nini Enna alishuka kitaaluma?
3. Taja vitendo vibaya ambavyo Enna alifanyiwa na mwalimu wake.
4. Unatoa ushauri gani kwa mwalimu wa Enna?
5. Je, utawasaidiaje wanafunzi wenye changamoto kama ya Enna shuleni kwako?
6. Una ushauri gani kwa watu walio na mazoea ya kutoa adhabu bila kusikiliza shida ya mwanafunzi?

**Kazi ya Kufanya**

Shirikiana na wenzako kuandaa igizo dhima litakaloonesha maovu yanayofanywa dhidi ya wanafunzi shuleni na katika jamii inayokuzunguka. Kisha, muigize wakati wa kipindi darasani.

## Kutoa taarifa ya vitendo visivyokubalika

Je, umewahi kutendewa na wenzako vitendo visivyo kubalika? Ni vitendo gani hivyo? Je, ulivizuiaje? Kuna vitendo vingi vinavyovuruga amani katika familia ambavyo havina budi kutolewa taarifa. Taarifa hizo zinaweza kutolewa katika taasisi zilizoanzishwa ili kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuishi kwa amani katika familia. Vilevile, taasisi hizi hupokea malalamiko au taarifa za vitendo vya unyanyasaji na hatarishi kwa familia kama vile dawati la jinsia. Unaweza kutoa taarifa ya matukio ya uhalifu kwenye dawati la jinsia lililopo kwenye kituo cha polisi kilicho karibu na kuwahamasisha wengine kufanya hivyo. Pia, unaweza kuwashawishi wenzako kujiunga na vikundi vinavyotetea haki za watoto. Vikundi hivyo vina nguvu na faida kubwa ya kuchochea amani katika jamii. Aidha,



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 52 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

shuleni kuna vitengo vya unasihi na ushauri nasaha. Tumia fursa hizo na uwashauri wengine kufanya hivyohivyo.

Wakati mwingine unaweza kuona woga kukemea vitendo visivyofaa. Badala yake unaweza kutoa maoni yako kwa kuyaandika na kuyaweka kwenye sanduku la maoni. Mbali na kujiunga na taasisi za kitaifa au kikanda zinazopinga ukatili wa wazazi au walezi, walimu na baadhi ya wanafunzi, unaweza pia kujiunga na klabu zinazojihusisha na suala hilo hapo shuleni. Serikali ya wanafunzi ni njia nyingine madhubuti ya kuimarisha demokrasia shuleni kwako. Kwa kufanya vikao vya mara kwa mara, kero mbalimbali za wanafunzi zinaweza kujadiliwa, kutolewa uamuzi na kuwasilishwa kwa uongozi wa shule kwa hatua zaidi. Inakupasa kutoa taarifa zozote za kweli ambazo zinaweza kuisaidia serikali hiyo kuchukua hatua katika kukemea vitendo viovu shuleni na nyumbani. Vilevile, saidiana na kushirikiana na walimu, wazazi au walezi kuhakikisha kuwa shuleni na nyumbani kwako kuna amani.

**Zoezi la 4**

1. Orodhesha vitendo vinavyohatarisha ustawi wa familia yako.
2. Je, utachukua hatua gani utakapotendewa vitendo vya unyanyasaji ndani ya familia?

**Kazi ya Kufanya**

Andika kisa au habari unayoijua ambayo inaibua vitendo visivyofaa, wanavyotendewa watoto shuleni na katika jamii.

## Kushiriki shughuli za maendeleo ya familia

Shughuli ni kazi halali kwa ustawi wa familia na jamii. Katika familia zipo shughuli mbalimbali, kwa mfano, kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara. Shughuli hizo hutusaidia kujikimu au kuongeza kipato cha familia. Je, katika familia yenu mnafanya shughuli gani zinazowaletea kipato?

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 53 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kufanya shughuli mbalimbali katika familia ni jambo muhimu katika maisha yetu ya kila siku. Shughuli hizi huongeza mtaji ambao hutuwezesha kufanya miradi mikubwa. Ukubwa wa kipato cha familia hutegemea shughuli tunazozifanya. Kwa kugawana majukumu katika shughuli tuzifanyazo tunaweza kuongeza kipato. Kwa mfano, baba wa familia anaweza kulima mazao ya chakula na biashara na mama akafuga kuku. Kutokana na kufuga kuku, familia huweza kujipatia nyama na mayai kwa matumizi ya nyumbani na hata kuuza ziada ili kujipatia fedha. Kupitia shughuli zifanywazo na baba na mama nyumbani, watoto hujifunza vilevile hupata ari ya kutenda shughuli hizo.

Familia inayojishughulisha huweza kuondoa umaskini na utegemezi. Hii ni kwa sababu familia huwa na uwezo wa kujipatia chakula na fedha za kutosha kukidhi mahitaji yake. Familia hiyo huwa na uwezo wa kuhudumia watoto wa familia, pamoja na watoto wa ndugu wenye uhitaji. Hii husaidia kupunguza uwepo wa watoto wa mitaani na wale wanaoishi kwenye mazingira magumu. Hili litawezekana kwa kuwa shughuli za kuzalisha mali hufanywa kikamilifu na familia nzima.

**Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Eliza ni mwanafunzi wa darasa la tano. Anaishi na wazazi wake pamoja na wadogo zake wawili. Baba yake Eliza ambaye ni Bwana Chapakazi ni mkulima hodari. Shamba la familia lina ekari nne ambazo Bwana Chapakazi analima mahindi, alizeti, maharage na karanga. Bwana Chapakazi huamka mapema sana na kwenda shambani kila siku. Mama yake Eliza naye huamka mapema na kuandaa kifungua kinywa kwa ajili ya familia. Eliza amezoea kuamka asubuhi na mapema, anachota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa siku nzima.*

*Tito ni mdogo wake Eliza, naye huingia darasani saa sita mchana. Akiamka asubuhi, hufagia uwanja, kisha huosha vyombo. Bwana Chapakazi hurudi nyumbani saa nne kupata kifungua kinywa na kujadili shughuli za siku na mama Eliza. Baadaye Bwana Chapakazi, hurudi tena shambani kuendelea na kazi zake. Mama Eliza huanza shughuli zake za bustani na kuwalisha kuku. Tito na Eliza wakirudi nyumbani hupumzika na kisha hupata chakula cha jioni. Vilevile, hulisha kuku na kuanza kujisomea na kufanya kazi walizopewa shuleni. Baadaye hujiandaa kwa siku inayofuata.*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 54 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Taja shughuli anazofanya Bwana Chapakazi.
2. Mama yake Eliza anajishughulisha na nini?
3. Eliza anashiriki vipi katika shughuli za familia?
4. Tito ambaye ni mdogo wake Eliza ana mchango gani kwa familia?
5. Je, wewe unashiriki vipi katika shughuli za familia yako?
6. Una ushauri gani kwa watoto wenzako ambao hawashiriki katika shughuli za nyumbani?
7. Orodhesha matendo utakayoanza au kuendelea kuyafanya katika familia yenu baada ya kusoma kisa hiki.

## Kazi ya Kufanya

Jadili na wenzako kuhusu shughuli za kiuchumi zinazofanywa katika jamii unayoishi, kisha orodhesha kwenye daftari lako shughuli ambazo familia yako inashiriki kuzifanya.

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2



*Kielelezo namba 1: Baadhi ya shughuli za kuleta maendeleo katika familia*

**Zoezi la 6**

1. Unaona nini kwenye picha namba 1 na namba 2?
2. Je, kuna njia gani nyingine ya kulima shamba?
3. Watoto wa familia hii wanashirikije kwenye ustawi wa familia yao?
4. Orodhesha shughuli unazozifanya wewe kwa ustawi wa familia yenu.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi kuhusu shughuli ambazo utapenda kuzifanya ili kujipatia kipato, baada ya kuhitimu elimu yako ya msingi. Andika shughuli hizo kwenye daftari na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii

Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii na kushirikiana nao katika shida na raha hukuza uhusiano mwema na majirani na jamii kwa ujumla.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 56 17/08/2021 11:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1




2




*Kielelezo namba 2: Vitendo vinavyoonesha uhusiano mzuri na majirani zetu*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 57 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 7**

1. Orodhesha vitendo unavyoviona kwenye picha namba 1 na namba 2.
2. Orodhesha vitendo vingine unavyovifahamu vinavyofanana na hivi vilivyoonekana kwenye picha namba 1 na namba 2 ulivyowahi kushuhudia katika jamii yako.
3. Bainisha faida za vitendo vya kuonesha uhusiano mwema wa aina hii katika jamii inayokuzunguka.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi wako kuhusu vitendo vinavyoweza kuiweka karibu familia yenu na jamii inayowazunguka. Orodhesha vitendo hivyo kwenye daftari lako, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Kukuza mahusiano bora na majirani

Ni vizuri kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii inayokuzunguka. Kuna mbinu mbalimbali za kukuza uhusiano mzuri na watu wengine. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na kutembeleana na kujuliana hali, kushirikiana na wenzako katika mambo mbalimbali kama vile masomo, michezo na kazi. Pia, watu wanashirikiana katika matukio mbalimbali kama misiba na harusi. Vilevile, kushiriki katika shughuli za maendeleo kama kuotesha miti, kusafisha mifereji ya maji na kuchimba barabara. Hali kadhalika, majirani wanaweza kushauriana na wenzao kwenye mambo mbalimbali yenye kuleta manufaa na kutatua migogoro ili kuleta amani.

## Kujiunga na vikundi mbalimbali

Moja ya vipengele muhimu vya kujijali na kuwajali wengine ni kushirikiana na wenzako kwa kujiunga katika vikundi mbalimbali vya kijamii. Kujiunga na vikundi mbalimbali hujenga umoja. Hii ni njia nzuri ya kujenga uhusiano mzuri katika jamii. Katiba ya nchi yetu inatoa fursa ya kuunda na kujiunga na vikundi ili kuimarisha uhuru, umoja, demokrasia na maendeleo. Uhuru



URAIA NA MAADILI STD V .indd 58 17/08/2021 11:19
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wa kujiunga na kushirikiana na wengine ni muhimu ili kujenga timu ya kuchochea maendeleo. Vilevile, kujiunga na vikundi mbalimbali hutoa fursa ya kujitambua kwani mtu hupata fursa ya kuonesha vipaji vyake. Je, wewe umeshajiunga na kikundi au klabu yoyote shuleni au katika jamii?

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1



2




*Kielelezo namba 3: Baadhi ya vikundi vinavyoweza kutumika kujenga umoja*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 59 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 8**

1. Taja vitendo unavyoviona kwenye picha namba 1 na 2.
2. Orodhesha vitendo vingine unavyovifahamu vinavyofanana na hivi vinavyoonekana kwenye picha namba 1 na namba 2 ambavyo vinahamasisha umoja katika jamii.
3. Orodhesha faida unazoweza kupata kwa kujiunga na klabu mbalimbali shuleni kwako.
4. Utamsaidiaje mwenzako asiyependa kushiriki katika vikundi mbalimbali?
5. Taja vikundi au klabu zilizoanzishwa katika shule yenu.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na mwalimu kuhusu namna mtakavyoanzisha au kuimarisha klabu mbalimbali shuleni kwenu.

## Kushiriki katika kutatua matatizo

Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii inayokuzunguka, ni pamoja na kusaidiana katika mambo mbalimbali, hususani kutatua shida na matatizo ya wenzetu. Katika maisha utakutana na watu mbalimbali wenye matatizo na watakaohitaji msaada wako. Watu hao wanaweza kuwa majirani zako, wanafunzi wenzako, wazazi wako, au jamii kwa ujumla. Mfano, mwanafunzi mwenzako akikosa mahitaji ya msingi kama daftari au kalamu, unaweza kumsaidia kwa kumpa daftari na kalamu au kuonesha njia ya kupata. Pia, tunaweza kumsaidia pale anapokuwa na matatizo mbalimbali kama ya kiafya au kufiwa. Vilevile, tunaweza kuzungumza na wazazi wetu ili kuwaalika wenzetu wenye matatizo waweze kuishi na familia zetu wakati wa likizo.

## Soma habari hii kwa makini, kisha jibu maswali yanayofuata.

Juma na Moses ni marafiki wakubwa. Wazazi wa Moses wanajiweza kiuchumi. Moses alikuwa anapata mahitaji yote muhimu kutoka kwa



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wazazi wake. Pia, alikaa karibu sana na shule yao. Juma ni mtoto yatima, hivyo aliishi na shangazi yake katika kijiji kilicho mbali kidogo na shule. Shangazi yake Juma hakuwa na uwezo mkubwa kiuchumi. Hivyo, Juma alikuwa hapati mahitaji ya msingi. Hata nauli ya kwenda shule siku zingine alikosa. Alitembea kwa miguu umbali mrefu kwenda shule na kurudi nyumbani. Mara kwa mara aliugua, hivyo hakuweza kufanya vizuri sana kwenye masomo. Alikuwa mtu mwenye huzuni muda wote. Moses alipoona Juma yuko katika majonzi na mawazo muda wote, alijaribu kumzoea na kumdadisi. Kutokana na ukaribu huo, aligundua matatizo ya Juma. Ugunduzi huo ulimfanya Moses awe karibu sana na Juma kwa lengo la kumsaidia. Pia, Moses aliwaeleza wazazi wake kuhusu tatizo la Juma. Moses alianza kushirikiana na Juma kwenye masomo. Alimsaidia vifaa mbalimbali kama daftari na kalamu. Hatimaye, alimkaribisha nyumbani kwao kwa ridhaa ya wazazi wake. Wazazi wa Moses waligharamia matibabu ya Juma mpaka alipopona kabisa.

Baada ya afya ya Juma kuwa nzuri, alisoma kwa bidii. Wote wawili walifanya vizuri sana kwenye mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi. Sasa hivi wapo chuo kikuu ambapo Moses anasomea fani ya udaktari wa mifugo na Juma anasomea fani ya uhasibu. Wanafanya vizuri sana katika masomo yao huko chuo kikuu.

**Zoezi la 9**

1. Juma alikuwa na matatizo yapi?
2. Je, Moses alimsaidiaje Juma kutatua matatizo?
3. Je, unawasaidiaje wanafunzi wenye matatizo kama ya Juma shuleni kwako?
4. Je, ni matatizo yapi mengine waliyonayo wanafunzi wenzako mbali ya hayo yaliyoainishwa kwenye habari hii?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi wako namna ya kumsaidia mwenzako aliye kwenye matatizo ya kushindwa kununua sare ya shule. Andika kwenye daftari namna ya kutatua tatizo hilo kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 61 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 10

**Andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku.**

1. Kujijali na kuwajali wenzako kunasaidia mwanafunzi:
   (a) kufanya mambo yanayokubalika katika jamii
   (b) kuogopwa
   (c) kutenda uovu
   (d) kuwa mkorofi

2. Kugombana na wenzako mara kwa mara unapokuwa shuleni au nyumbani ni tabia:
   (a) isiyokubalika
   (b) inayoonesha kujali wenzako
   (c) ya upendo
   (d) ya unyenyekevu au kishujaa.

3. Matendo yafuatayo yanakuza uhusiano na watu wengine:
   (a) kushirikiana, kuwasadia watu wenye mahitaji maalumu, kuheshimiana na kujiunga katika vikundi vya kusaidiana
   (b) kuonesha upendo, kuheshimiana, ugomvi na unafiki
   (c) kuwasaidia watu wenye mahitaji, kusema uongo, kushirikiana na kuheshimiana
   (d) kuwasaidia watu wote na kuwafanyia unafiki

4. Moja ya faida za kujiunga na klabu za masomo shuleni ni:
   (a) kukuza uelewa na uongo.
   (b) kukuza uelewa na kujiamini
   (c) kushindana kwa majibizano ya ujeuri.
   (d) kuwa maarufu na kuvunja haki za binadamu

5. Ni njia mojawapo ya kutomsaidia mwanafunzi mwenye matatizo:
   (a) kumshika mkono
   (b) kumkumbatia
   (c) kumshauri namna ya kutatua tatizo
   (d) kumtenga

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 62 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Namna bora ya kushirikiana na majirani zako unapokuwa nyumbani:
   (a) kuwakimbia wanapokuwa na shida
   (b) kutowapokea mizigo
   (c) kujumuika nao katika matukio ya shida na raha
   (d) kuwakwepa pale wanapoomba msaada

7. Unaposhuhudia vitendo vya ukatili uwapo shuleni unatoa taarifa:
   (a) mahakamani
   (b) polisi
   (c) kwa mwalimu wa ushauri nasaha
   (d) kwa mwenyekiti wa mtaa tu

8. Ni madhara ya vitendo vya kikatili katika familia:
   (a) vifo na kushirikiana
   (b) kuvuna mazao mengi
   (c) kuwafundisha na kuwapiga
   (d) kusambaratika kwa familia

9. Umuhimu wa kushiriki shughuli za kifamilia kwa wanafunzi:
   (a) kutopata ajira
   (b) kumjengea mwanafunzi ari ya kujitegemea
   (c) kutopenda kula chakula anachopika
   (d) kutowahi kufika nyumbani baada ya kutoka shuleni na matembezini

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Holela | ovyoovyo bila kufuata utaratibu au mpangilio |
| Kudadisi | kuhoji au kupeleleza jambo kwa lengo la kujua zaidi |
| Nasaha | mawaidha, mashauri au mwongozo mzuri katika jambo |
| Dhamiria | kusudia kutenda jambo |
| Unasihi | ushauri wa kitaalamu unaotolewa juu ya tatizo au changamoto fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kuithamini jamii

Ulipokuwa darasa la nne ulijifunza jinsi ya kuithamini jamii kwa kutafakari vitendo vya kujijali na kuwajali wengine, ikiwa ni pamoja na kutambua na kukemea matendo maovu wanayofanyiwa watoto. Katika sura hii, utajifunza zaidi jinsi ya kuithamini jamii kwa kutathmini hali ya uharibifu wa mazingira katika eneo unamoishi ili uweze kuelewa wewe mwenyewe pamoja na kuweza kuielimisha jamii yako juu ya athari za uharibifu wa mazingira.

### Kutunza mazingira

Je, umewahi kujiuliza mazingira ni nini? Mazingira hujumuisha maeneo tunayoishi na vitu vyote vinavyotuzunguka. Vitu hivi vinaweza kuwa vya asili kama vile milima, misitu, mito, maziwa, bahari na mabonde. Pia, vitu hivyo vinaweza kuwa ni vya kutengenezwa na binadamu kama vile majengo, barabara, magari, reli, viwanja vya ndege na mashamba.

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1





URAIA NA MAADILI STD V .indd 64 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2



*Kielelezo namba 1: Baadhi ya mazingira yanayotunzwa vizuri*

**Zoezi la 1**

1. Picha namba 1 na 2 zinaonesha vitu gani?
2. Tofautisha asili za vitu vinavyoonekana kwenye picha hizi.
3. Umewahi kuona vitu hivyo katika mazingira yako?
4. Eleza umuhimu wa vitu vilivyomo katika picha namba 1 katika maisha yetu.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako namna mtakavyoboresha mazingira ya shule ili yawe mazuri na safi. Orodhesha mikakati hiyo kwenye daftari lako kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira na athari zake

Uharibifu wa mazingira kwa sehemu kubwa hutokana na shughuli za binadamu. Ni sehemu ndogo tu hutokana na matukio ya asili. Shughuli za binadamu zinazochangia uharibifu wa mazingira ni kama vile, kilimo,



URAIA NA MAADILI STD V .indd 65 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ufugaji, uchimbaji madini na uzalishaji viwandani. Matukio ya asili yanayochangia uharibifu wa mazingira ni pamoja na mafuriko, milipuko ya volkano na upepo mkali.

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kata ya Honda iliyopo wilaya ya Zunga ilikuwa imekithiri kwa vitendo vya uharibifu wa mazingira. Wananchi wa kata hiyo walijihusisha na ukataji wa miti na kuchoma misitu. Wengi waliandaa mashamba kwa kuchoma moto misitu na hivyo kuzalisha moshi uongezao hewa ya ukaa katika uso wa dunia. Walitumia mkaa na kuni majumbani ambazo zimetokana na kukata misitu na kuchangia uchafuzi wa hali ya hewa. Yote haya yamesababisha kutokufuata taratibu sahihi za maliasili na ujenzi bora wa makazi yao.

Pia, walijihusisha na uchafuzi wa vyanzo vya maji kwa kufanya shughuli zisizofaa kama vile kuoga ndani ya mto, kulima kandokando ya mto, kuchunga na kunywesha mifugo kandokando ya mto, pamoja na kujisaidia ndani ya mto. Baadhi ya wananchi wa kata hiyo walifuga mifugo mingi bila kuzingatia utoshelevu wa maeneo ya malisho na maji. Vilevile, walitupa takataka ndani ya mto.

Aidha, wananchi wengine walijihusisha na uchimbaji holela wa mchanga na mawe kwa ajili ya ujenzi. Kwenye kata hiyo kulikuwa na viwanda vya kuchambua pamba na kukamua mafuta ambavyo viliongeza uchafuzi wa mazingira. Shughuli nyingine ambazo zilifanyika kwenye kata hii ni uchimbaji wa madini. Wachimbaji wadogowadogo waliacha wazi mashimo na uwezekano wa kutumia ardhi hiyo tena haukuwepo. Pembeni mwa machimbo hayo kulikuwa na mto mdogo uliokuwa ukitumiwa na wachimbaji hao kusafishia madini yaliyopatikana katika eneo hilo. Matokeo yake ni kwamba kemikali zenye sumu kama zebaki zilizotumika kusafisha madini ziliingia kwenye maji hayo.

Hivyo, hali hii ilisababisha uchafuzi wa maji hayo na kupelekea kuibuka kwa magonjwa ya ngozi, kufa kwa mifugo na viumbe hai walioishi kwenye mto huo. Madhara mengine waliyoyapata kutokana na uharibifu wa mazingira ni pamoja na ukosefu wa mvua na wakati mwingine mvua kunyesha kupita kiasi na kuongezeka kwa mmomonyoko wa udongo. Vilevile, walikosa chakula cha kutosha kutokana na mavuno haba, ukosefu wa maji kutokana na uharibifu wa vyanzo vyake, kutokea kwa jangwa na majanga mbalimbali ya asili kama vile mafuriko na ukame.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 2

1. Orodhesha vitendo vya uharibifu wa mazingira vilivyobainishwa kwenye habari hii.
2. Wakazi wa kata ya Honda watapata matatizo gani kutokana na vitendo vya kuchoma misitu moto wakati wa kuandaa mashamba?
3. Ni kwa namna gani viwanda huchangia uchafuzi wa mazingira katika jamii?
4. Shughuli za uchimbaji madini zinaathiri vipi mazingira?
5. Orodhesha athari za kutiririsha sumu za viwandani na migodini kwenye maji.
6. Baada ya kusoma habari hii, unapendekeza hatua gani zichukuliwe za kunusuru mazingira ya Kata ya Honda?
7. Taja athari zinazosababishwa na kufuga idadi kubwa ya mifugo katika eneo dogo?
8. Ni magonjwa yapi yanaweza kutokea kwa sababu ya uharibifu wa mazingira?

### Kazi ya Kufanya

Chunguza eneo unaloishi kama kuna shughuli za binadamu zinazosababisha uharibifu wa mazingira, kisha orodhesha shughuli hizo kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Matendo ya kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira

Jamii haina budi kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira ili kuyatunza na pia kunusuru maisha yetu. Kadri tunavyoharibu mazingira yetu ndivyo tunavyohatarisha maisha yetu.

Katika ngazi ya taifa, jukumu la kusimamia utunzaji wa mazingira lipo chini ya ofisi ya makamu wa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndani ya ofisi hii ya makamu wa rais, serikali pia imeunda wizara

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maalum inayoitwa Wizara ya nchi ofisi ya makamu wa rais muungano na mazingira. Chini ya wizara hii kuna baraza la taifa la hifadhi na usimamizi wa mazingira lenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa mazingira. Mtu yeyote atakayefanya vitendo vya uharibifu wa mazingira nchini Tanzania anaweza kushitakiwa na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria. Pia, katika ngazi ya taifa ipo Wizara ya maliasili na utalii ambayo ina vitengo vya maliasili sehemu mbalimbali nchini vyenye jukumu la kusimamia rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na kuandaa mbegu bora za miti, kufanya utafiti na kudhibiti ukataji miti ovyo.

Pamoja na hayo, katika ngazi ya serikali za mitaa kuna ofisa maendeleo anayehusika na uhamasishaji na utunzaji mazingira, akifanya kazi na ofisa maliasili anayesimamia wananchi kupambana na uharibifu wa mazingira. Pia, yapo mashirika mbali mbali yasiyo ya kiserikali yanayoshughulika na kuhamasisha utunzaji wa mazingira. Pia, vipo vikundi vya wanawake na vijana wanaofanya matendo ya kuhifadhi mazingira kama vile, kuandaa vitalu vya miche ya miti ya aina mbalimbali.

Je, katika shule yako ni nani anayesimamia udhibiti wa mazingira na kuhamasisha utunzaji wake? Je, umewahi kuona vitalu vya miche ya miti? Je, uliviona wapi? Je, wewe umewahi kuotesha mti?

**Zoezi la 3**

1. Pendekeza njia ambazo zinaweza kutumiwa kuepusha au kupunguza uharibifu wa mazingira.
2. Katika eneo unaloishi kuna matendo gani yanayofanyika ambayo unafikiri yanasaidia utunzaji wa mazingira yenu?

**Kazi ya Kufanya**

Jadili na wanafunzi wenzako namna mtakavyotunza vyanzo vya maji vya kijiji au mtaa wenu. Orodhesha matendo hayo kwenye daftari, kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 68 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Elimu ya mazingira kwa jamii

Ili kuweza kuyatunza mazingira yetu yatupasa kushiriki katika elimu ya mazingira ili kujifunza juu ya athari na faida ya utunzaji mazingira. Hivyo, ni muhimu kwa kila mmoja kushiriki kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira. Elimu itolewe juu ya athari za uharibifu wa mazingira na kufanya matendo yanayodhibiti uharibifu wa mazingira. Je, kwa namna gani tunaweza kuyatunza mazingira yetu?

**Chunguza picha, hizi kisha jibu maswali yanayofuata.**

1



2



*Kielelezo namba 2: Baadhi ya vitendo vinavyoonesha kuhifadhi mazingira*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 69 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Je, ni matendo gani uliyoyabaini kwenye picha namba 1 na 2 ambayo yanadhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira?
2. Je, utashiriki vipi katika kuboresha mazingira ya shuleni au nyumbani kwenu?

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu matendo ya kuhifadhi mazingira katika jamii yenu. Orodhesha matendo hayo kwenye daftari lako, kisha yawasilishe kwa mwalimu wa somo.

**Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Doto ni mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Jitegemee. Anaishi kijiji cha Mkuyuni, Kata ya Kilacha. Alipokuwa anajifunza kuhusu utunzaji wa mazingira alimkumbuka baba yake. Kila mara baba yake alikuwa anakata miti shambani mwao bila kupanda miti mingine. Kwa kuwa shamba lilikosa miti upepo ulipeperusha udongo wenye rutuba na kuacha udongo mbaya. Mazao yakaanza kupungua. Vilevile, takataka za nyumbani na shambani zilizagaa kwenye eneo lao. Baadhi ya takataka zilitoka kwao na nyingine, kama karatasi na mifuko ya nailoni zililetwa na upepo kutoka maeneo mengine. Eneo lao likakosa mvuto.*

*Doto akaamua kutumia elimu ya mazingira aliyoipata shuleni kuwafundisha wazazi na ndugu zake jinsi ya kuboresha mazingira yao. Alimfundisha baba yake faida za kuwa na miti shambani. Alimsisitiza kupanda mti kila anapokata mti. Alimweleza umuhimu wa kuchimba shimo la kuhifadhia takataka. Vilevile, aliwaelimisha ndugu zake umuhimu wa kuwa na mazingira mazuri kuzunguka nyumba yao. Wote walifurahia mafunzo yake. Wakaanza kuboresha mazingira ya eneo lao. Baba alianza kuchimba shimo la takataka. Akaanza kupanda miti kwenye shamba lao. Alianza kilimo cha matuta pia. Doto na ndugu zake walianza kuboresha mazingira ya nyumbani kwao pia. Walitenga sehemu ya bustani na sehemu za maua. Baada ya muda eneo lao lilianza kubadilika. Majirani walishangaa mabadiliko yaliyotokea na kuanza kujifunza namna ya kuboresha mazingira yao kutoka kwa familia ya Doto.*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Je, mazingira ya eneo la familia ya Doto yalikuwa na matatizo gani?
2. Ni matendo gani yalisababisha uharibifu wa mazingira yao?
3. Kwa kutumia elimu aliyojifunza darasani kuhusu mazingira, Doto alifanya nini kuokoa mazingira yao?
4. Licha ya familia yake,ni watu gani wengine walinufaika na elimu hiyo?
5. Ainisha matendo yanayofanyika kwenye eneo lenu ambayo yanaboresha mazingira.
6. Orodhesha hatua unazofikiri utazitumia kuelimisha jamii inayokuzunguka ili kuokoa mazingira yenu.

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wenzako namna mtakavyoboresha mazingira ya shuleni kwenu. Andika kazi kwenye daftari na kuwasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Shughuli za maendeleo ya jamii

Shughuli za maendeleo ni kazi mbalimbali zinazofanyika kwa ajili ya ustawi wa jamii. Baadhi ya shughuli hizo ni ujenzi wa shule, ujenzi wa zahanati, barabara, mifereji na mabomba ya maji. Shughuli za maendeleo ya jamii hufanywa na wanajamii wenyewe. Tukiwa kama sehemu ya jamii, inatupasa kushiriki katika shughuli za kijamii. Tunaweza kushiriki kwa namna mbalimbali. Aina ya kwanza ya ushiriki ni ile ya moja kwa moja. Kwa mfano, tunaweza kushirikiana na wengine katika kutunza na kuboresha mazingira kwa kuotesha miti, kufanya usafi na kuotesha maua na kuyatunza.

Tunaweza pia kushiriki kwa kuchimba mashimo ya takataka, mitaro ya maji machafu, kukata nyasi ili kuharibu mazalia ya wadudu waharibifu kama vile mbu. Aina ya pili ya kushiriki ni kuunda vikundi vya utunzaji mazingira au ujasiriamali. Ndani ya kikundi unaweza kushiriki kama mwanachama wa kawaida au mmoja wa viongozi wa kikundi. Aina ya tatu ya ushiriki ni kwa kutoa msaada au huduma kwa watu wenye mahitaji maalumu ili nao waweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za maendeleo ya kijamii.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 71 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha hizi, kisha fanya zoezi linalofuata.**

1



2




*Kielelezo namba 3: Kushiriki kufanya baadhi ya shughuli za kijamii*

**Zoezi la 6**

1. Katika picha hizi unaona matendo gani?
2. Je, unajifunza nini kutokana na picha hizi?
3. Je, ni matendo gani ambayo wewe unaweza kushiriki?
4. Unaposhiriki kwenye shughuli za maendeleo ya jamii unajenga tabia gani?



URAIA NA MAADILI STD V .indd 72 17/08/2021 11:19
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na mwanafunzi mwenzako kubainisha sehemu zinazohitaji msaada kwa ajili ya maendeleo ya ustawi wa kijamii kutokana na changamoto za mazingira. Pendekeza shughuli na mbinu ambazo mtaweza kuzifanya ili kuchangia katika sehemu mlizobainisha. Andika kazi hiyo katika daftari na uwasilishe darasani wakati wa kipindi.

## Zoezi la 7

**Sehemu A**

Andika **Kweli** au **Si Kweli** kwenye sentensi zifuatazo:

1. Kutupa takataka ovyo na kukata miti ovyo huchangia uharibifu wa mazingira. ____________
2. Kuchoma misitu ni njia mojawapo ya utunzaji wa mazingira. ____________
3. Ufukiaji wa mashimo baada ya uchimbaji wa mchanga au madini ni kitendo cha uboreshaji wa mazingira. _________
4. Ukichoma takataka ovyo karibu na msitu unatunza mazingira. ____________
5. Ujenzi wa shule, zahanati, barabara na mifereji ni baadhi ya shughuli za maendeleo ya jamii. ____________

**Sehemu B**

**Chagua jibu sahihi kwa kuandika herufi ya jibu katika kisanduku**

6. Unaposhiriki katika shughuli za maendeleo ya jamii unaleta:
   (a) mshikamano na uzalendo
   (b) shida kwa wananchi
   (c) mtandao wa ombaomba
   [ ]

7. Shughuli za kibinadamu ambazo huchangia uchafuzi wa vyanzo vya maji ni kama vile:
   (a) kufua nguo, kupanda miti kuzunguka eneo la vyanzo vya maji
   (b) kulima na kufua nguo kandokando ya mto
   (c) kutunza mazingira ya asili na kunywesha mifugo
   [ ]

8. Mamlaka inayohusika na usimamizi na utunzaji mazingira nchini huitwa:
   (a) mamlaka ya mapato ya Tanzania



URAIA NA MAADILI STD V .indd 73 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) wizara ya afya
(c) baraza la usimamizi wa mazingira la taifa

9. Ni vyema tukaboresha njia za uchimbaji wa madini ili kusaidia:
(a) uchimbaji wa madini kuwa endelevu na wenye ufanisi
(b) kutopata fedha za kutosha
(c) kukosa ajira kwa wingi

10. Ukataji wa miti ovyo na uchomaji wa misitu huweza kusababisha:
(a) ukame na baa la njaa
(b) mvua nyingi na kupata eneo kubwa la kulima
(c) kupata mavuno mengi

11. Shughuli za maendeleo ya jamii ni pamoja na:
(a) kuiba na kutapeli wenzako
(b) kuharibu mazingira
(c) kusafisha barabara, mitaro na mazingira

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Hewa ya ukaa | hewa yenye sumu ya kaboni inayotokana na uchafuzi wa mazingira |
| Kipato | mavuno au fedha anazopata mtu zikiwa ni malipo ya kazi aliyoifanya au faida ya mauzo ya kitu |
| Madhara | ni uharibifu au athari mbaya |
| Mgodi | ni mahali panapochimbwa madini kama vile makaa ya mawe, dhahabu au almasi |
| Mkakati | mpango maalumu unaoandaliwa kwa ustadi mkubwa ili utumike kama njia ya kufanikisha au kutatua tatizo fulani kwa lengo fulani |
| Mtabiri | mtu anayeeleza mambo kwa kubashiri yatakayotokea |
| Mtandao | mfumo unaowaunganisha watu katika kutenda jambo fulani |
| Mtaro | ni mfereji mkubwa na mrefu uliochimbwa kwa makusudi ya kupitishia kitu, kama vile maji machafu, bomba la maji au mfereji wa kumwagilia shamba |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 74 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi

Ulipokuwa darasa la nne ulijifunza tabia ya kujitolea katika jamii yako, kujenga tabia ya kuthamini rasilimali za jamii na kutimiza wajibu wako katika familia. Ulijifunza pia kushirikiana na wengine katika kutekeleza majukumu ya shuleni na nyumbani. Katika sura hii, utajifunza umuhimu wa kulinda rasilimali za nchi kama wajibu wa kila raia mwema. Aidha, utajifunza kubaini rasilimali za taifa, matumizi ya rasilimali za taifa, kutunza rasilimali za taifa, kushiriki katika utunzaji wa rasilimali zilizopo, pamoja na kukemea matumizi mabaya ya mali za umma.

Rasilimali ni jumla ya mali zote zilizopo kwa mtu binafsi, kikundi cha watu, mashirika ya umma au binafsi au taifa husika kwa mfano; ardhi, watu, misitu, milima na makumbusho ya kihistoria. Pia, zipo rasilimali zinazopatikana nyumbani, kama vile nyumba, mashamba, mabomba ya maji na umeme. Rasilimali ni muhimu kwa maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa. Hivyo, ni muhimu kuzitunza. Kuna njia mbalimbali za kulinda na kutunza rasilimali. Baadhi ya njia hizo ni kama zilivyoainishwa katika sehemu inayofuata.

### Njia za kutunza na kuhifadhi rasilimali za taifa

Kuna njia mbalimbali za kulinda na kutunza rasilimali za taifa dhidi ya uharibifu. Miongoni mwa njia hizo ni pamoja na kutoshiriki katika uharibifu wa rasilimali na kutoa taarifa za uharibifu wa rasilimali. Njia nyingine ni kutunza milima na mabonde kwa kuendeleza uoto wake wa asili. Mfano kutunza uoto wa Mlima Kilimanjaro na bonde la Olduvai, Rufiji, Kilombero, Ihefu na maporomoko ya Kihansi. Mifano mingine ya kuhifadhi rasilimali ni pamoja na kuhifadhi makumbusho ya kihistoria, kama vile, mapango ya Amboni yaliyopo Tanga na michoro ya Kondoa Irangi iliyopo Dodoma. Pia, kutokukata miti ovyo, kuhifadhi vyanzo vya maji, kuzuia uvuvi na uwindaji haramu wa wanyama pori.

Kuna vitendo vingi vinavyochangia uharibifu wa rasilimali katika mazingira yanayotuzunguka. Mifano ya vitendo hivyo ni pamoja na uharibifu wa



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 75 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ardhi na misitu, kwa kuchimba madini, kulima kwa njia zisizofaa na kuchoma misitu. Mifano mingine ni uharibifu wa rasilimali maji kwa uvuvi wa kutumia sumu au baruti, kutupa takataka na uoshaji wa madini.

**Angalia picha hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**



*Kielelezo namba 1: Baadhi ya matendo ya kutunza rasilimali za nchi*

**Zoezi la 1**

1. Orodhesha rasilimali unazoziona kwenye kielelezo namba 1.
2. Taja kitendo kinachofanyika kwenye kielelezo namba 1.
3. Taja faida tatu za kitendo kinachofanyika kwenye kielelezo namba 1.
4. Orodhesha vitendo vinavyosadia utunzaji wa rasilimali za nchi. Je, vitendo hivyo vinalipatia taifa letu faida zipi?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako namna mnavyoweza kulinda rasilimali za mtaa wenu. Andika mikakati yenu kwenye daftari na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matumizi ya rasilimali za taifa

Je, unayajua matumizi ya rasilimali za taifa? Umewahi kufaidika nazo? Rasilimali za taifa ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya nchi yoyote ile. Maendeleo ya nchi hupimwa kutokana na kiwango cha rasilimali walizonazo. Nchi yetu imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi sana kama vile madini, ardhi, misitu, maji, milima na mabonde, mbuga za wanyama na watu. Katika kipengele hiki tutaangalia matumizi ya rasilimali hizi na umuhimu wa kuzitunza.

### Madini

Madini ni mawe yenye thamani ambayo mara nyingi hupatikana chini ya ardhi. Madini ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote ile. Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimejaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali. Baadhi ya madini yanayopatikana kwa wingi nchini Tanzania ni dhahabu, tanzanite, almasi, makaa ya mawe, aluminiamu, chokaa, chuma, chumvi na potasiamu. Madini haya hutumika kama malighafi za kutengenezea vitu mbalimbali vya thamani kama vile mikufu, saa, pete na hereni. Pia, baadhi ya madini kwa mfano madini ya chokaa hutumika kutengenezea saruji, chaki na jipsamu. Vivyo hivyo, chuma cha pua hutumika kutengeneza zana za chuma zilizo imara kama vile zana za kilimo, vifaa vya ujenzi na baadhi ya vifaa vya nyumbani. Madini ya aluminiamu hutumika kutengeneza sufuria, madirisha na bati za kuezekea nyumba. Madini ya dhahabu hutumika pia kuthamanisha utajiri wa nchi, kama yatahifadhiwa katika benki kuu ya taifa.



*Kielelezo namba 2: Baadhi ya vifaa vilivyotengenezwa kwa madini ya chuma na kunakishiwa kwa madini ya dhahabu*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 77 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ardhi

Ardhi ni sehemu ya dunia isiyo na maji au ni sehemu ya nchi kavu ya dunia. Ni moja ya rasilimali muhimu katika nchi yoyote ile ikiwemo Tanzania. Ardhi inajumuisha vitu vyote vilivyoota juu yake na vitu vyote vilivyopo chini ya ardhi. Ardhi ina matumizi mengi yakiwemo ya kilimo na ujenzi wa makazi ya binadamu na viwanda. Pia, hutumika kwa hifadhi ya wanyama na viumbe hai wengine. Vilevile, ardhi hutumika katika kuhimili uoto wa asili na maji na pia huchuja maji kwa njia ya asili kama vile maji ya chemichemi.

## Misitu

Msitu ni mahali penye miti mingi, mikubwa na midogo, vichaka na nyasi. Kuna misitu ya aina mbili, misitu ya asili na misitu ya kupandwa na binadamu. Misitu ya asili huota yenyewe, mfano wa baadhi ya misitu ya asili ni msitu wa Udzungwa, Zaraninge, Pugu-Kisarawe, Kazimzumbwi, Ruaha, Mikumi, Serengeti na Katavi. Baadhi ya misitu ya kupandwa na binadamu ni kama ile ya Sao Hill (Iringa), Msitu wa Kibena (Njombe) na Forest (Mbeya).

Misitu ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu, wanyama, ndege na viumbe hai wengine. Kwa binadamu, misitu hutoa vifaa vya ujenzi, kama vile mbao, miti, nguzo na kamba. Pia, hutoa kuni, mkaa na dawa za asili. Vilevile, hutumika kufanyia matambiko au ibada za asili, mfano mzuri ni msitu wa Nyumbanitu uliopo Njombe. Aidha, kwa viumbe wengine, misitu hutumika kama makazi ya wanyama pori, ndege na wadudu mbalimbali.



*Kielelezo namba 3: Msitu wa asili*



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 78 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maji

Maji ni kimiminika kisicho na rangi kinachotokana na mito, maziwa, bahari na mvua. Watu hutumia maji kwa kupikia, kunywa na kufanyia usafi. Maji yamegawanyika katika aina kuu mbili ambazo ni; maji ya chumvi ambayo yanapatikana baharini na maji yasiyo na chumvi ambayo hupatikana katika mito, maziwa, chemichemi na mabwawa. Maji ni kiini kikubwa cha uhai wa viumbe hai vyote duniani na karibu zaidi ya robo tatu ya eneo la dunia imezungukwa na maji.

Maji yana matumizi mengi nyumbani na katika shughuli za kiuchumi kama vile kilimo na viwanda. Nyumbani maji hutumika kunywa, kuoga, kufulia na kuoshea vyombo. Kwa viumbe hai wengine, mfano kenge, samaki, mamba, viboko, vyura na kaa, maji ni sehemu yao ya makazi. Nchini Tanzania, maji yametumika kuonesha mipaka ya nchi, mfano Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Mto Ruvuma. Vilevile, maji hutumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji na kunyweshea mifugo, mfano, kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga huko Kapunga na Mbarali, Mbeya. Maporomoko ya maji hutumika kuzalisha nishati ya umeme. Kwa mfano kituo cha umeme cha Kidatu hutumia maji yanayoporomoka kutoka mto Ruaha na mto Kilombero. Vilevile, hutumika kama njia ya usafirishaji wa watu na mizigo kwenye bahari, maziwa na mito mikubwa kwa kutumia meli, jahazi, mashua, boti na mitumbwi. Aidha, maji husaidia kurekebisha hali ya hewa na pia kulinda uoto wa asili. Kwa mfano, maji hutoa mvuke unaotengeneza mvua. Pia, maji hutumika kupoozea na kusafishia mitambo au mashine mbalimbali viwandani.



*Kielelezo namba 4: Baadhi ya matumizi ya maji*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mbuga za wanyama

Mbuga za wanyama ni eneo wanaloishi wanyama pori. Baadhi ya mbuga za wanyama zilizopo nchini kwetu ni Serengeti, Ngorongoro, Mikumi na Ruaha. Wanyama hao ni vivutio vya utalii na hutupatia fedha za kigeni.



*Kielelezo namba 5: Hifadhi ya wanyamapori*

## Milima na mabonde

Milima na mabonde huhifadhi na kulinda uoto wa asili. Pia, ni chanzo cha ardhi yenye rutuba na kivutio kwa watalii. Tanzania tunayo rasilimali kubwa ya milima baadhi ya milima hiyo ni Mlima Kilimanjaro, Kipengere, Meru, Usambara na Uluguru. Milima hutupatia malighafi za ujenzi, kama vile mawe, chokaa na mchanga. Pia, baadhi ya milima na mabonde ni chanzo cha maji, mfano mlima Matogoro uliopo Songea, ambao ni chanzo cha maji ya mto Ruvuma. Tuitunze na kuihifadhi milima na mabonde yetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

## Watu

Watu ni viumbe hai wenye akili na utashi. Kwa hiyo, ni rasilimali kubwa katika nchi yoyote ile kwa sababu ya matumizi yake ya akili na utashi. Kwa kutumia akili yao na utashi wao, watu huwa ni nguvukazi ya taifa lolote



URAIA NA MAADILI STD V .indd 80 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

lile ikiwemo Tanzania. Kwa kutumia juhudi na maarifa yao, watu huzalisha mali mashambani, migodini, viwandani na penginepo ili kukuza uchumi wa taifa. Pia, viongozi na watalaamu mbalimbali hutokana na rasilimali watu. Vilevile, watu ni soko la bidhaa mbalimbali za mashambani na viwandani zinazozalishwa ndani na nje ya nchi.



*Kielelezo namba 6: Watu wakishiriki kazi ya ushonaji*

## Matumizi mabaya ya rasilimali za taifa

Hii ni hali ya kuzitumia rasilimali za taifa ama kwa lengo lisilofaa, au uvunaji wa rasilimali hizo kwa njia zisizofaa.

## Tafakari matendo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

1. Mwanafunzi anaharibu kitabu cha shule na mwingine anaruka juu ya madawati.
2. Mwanafunzi anachora ukuta wa jengo la shule; mwingine anaharibu bomba la maji shuleni.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 81 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Wanafunzi wengi wenye hasira wanavunja vioo vya madarasa kwa kuyapiga mawe.
4. Wanafunzi wanatembea kwenye bustani ya shule mmoja anang'oa maua.
5. Mwanafunzi anajaladia kitabu cha shule.
6. Mwanafunzi anapalilia bustani ya maua shuleni.
7. Mwanafunzi anafunga bomba la maji yasimwagike.
8. Mwanafunzi anamwagilia miche ya miti.

## Zoezi la 2

1. Orodhesha matendo yanayostahili kukemewa kati ya matendo uliyosoma.
2. Je, wewe ungekemea matendo yapi kati ya hayo uliyotaja? Kwa nini?
3. Orodhesha vitu vilivyo shuleni kwako ambavyo ni rasilimali za umma.
4. Eleza namna rasilimali za shule yenu zinavyotunzwa.
5. Eleza matendo ambayo utaweza kuyafanya kuanzia sasa yanayoonesha kukemea matumizi mabaya ya mali za shule.
6. Orodhesha vitendo vingine vya uharibifu wa rasilimali za umma katika jamii inayokuzunguka. Je, utakemeaje vitendo hivyo?
7. Ni vyombo vipi ambavyo unaweza kutoa taarifa ya uharibifu wa rasilimali ya umma katika jamii unayoishi?

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu namna mnavyotumia rasilimali maji katika shughuli za maendeleo ya jamii.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 82 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Sehemu A**

**Andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku.**

1. Ipi kati ya hizi ni miongoni mwa rasilimali zilizopo Tanzania ?
   (a) misitu
   (b) mbao
   (c) mkaa

2. Ipi kati ya hizi ni faida ya misitu?
   (a) kutupatia madini
   (b) kutupatia mbao
   (c) kutupatia nafaka

3. Tunawezaje kuhifadhi misitu?
   (a) kwa kukata miti
   (b) kwa kuchoma misitu
   (c) kwa kupanda miti

4. Ni kitendo gani kati ya hivi huchangia kuharibu rasilimali maji?
   (a) kukata miti kwenye vyanzo vya maji
   (b) kutochoma moto misitu
   (c) kutotiririsha maji machafu

5. Ni kitendo gani kati ya hivi huchangia kuharibu rasilimali ardhi?
   (a) kulima matuta kwa kukinga mteremko
   (b) kuchoma misitu wakati wa kusafisha mashamba
   (c) kuweka mbolea ya samadi shambani

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 83 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sehemu B**

Andika **Kweli** au **Si Kweli** kwenye sentensi zifuatazo:

6. Madini hutegemewa sana katika kuongeza pato la taifa. _________
7. Kila mtu anawajibika kulinda rasilimali za nchi. _________
8. Wanaoharibu rasilimali wanalisaidia taifa. _________
9. Mvuvi anayevua kwa kutumia sumu na baruti ni mtunzaji wa rasilimali. _________
10. Kukata miti ni njia mojawapo ya kulinda rasilimali misitu. _________
11. Wananchi wote wana jukumu la kulinda rasilimali madini. _________

**Sehemu C**

Oanisha neno au sentensi kutoka **sehemu A** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kutoka **sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Rasilimali za taifa | A. kutumia sumu |
| 2. Uharibifu wa ardhi | B. hutumika kwa kilimo na makazi ya wanadamu na wanyama |
| 3. Uvuvi haramu | C. vyanzo vya maji |
| 4. Ardhi | D. makazi ya wanyama tu. |
| 5. Milima na mabonde | E. watu, misitu, madini, ardhi, maji, wanyamapori |
| 6. Ubadhirifu | F. kuchoma misitu moto |
| 7. Urembo na nakshi | G. uvuvi usiotumia sumu |
| | H. matumizi mabaya ya rasilimali za umma |
| | I. hutokana na madini |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 84 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Mali ya umma | kitu chochote chenye thamani kinachomilikiwa na watu wote katika nchi |
| Malighafi | vitu vinavyotumika kuzalishia au kutengenezea vitu vingine |
| Matambiko | sadaka maalumu ya kiasili ambayo hufanywa kwa malengo ya kutuliza mizimu, kuungana nao au kuomba baraka zao |
| Nakshi | urembo wa kuchora, kutarizi au kuchongwa |
| Rasilimali | vitu muhimu na vya thamani vinavyomilikiwa na mtu, shirika au nchi |
| Wanyamapori | ni wanyama wasiofugwa na hupendelea kuishi mahali penye miti mingi, vichaka na nyasi |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 85 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kusimamia majukumu

Katika sura hii, utajifunza utayari wa kupokea majukumu, umuhimu wa kusimamia majukumu hayo na kuyatekeleza kwa ufanisi. Utajifunza pia utawala bora na umuhimu wa kutii sheria ili kuimarisha utawala bora.

### Usimamizi wa majukumu

Majukumu ni shughuli ambazo mtu anapaswa kuzifanya. Usimamizi wa shughuli hizi na nyinginezo ni nguzo ya msingi katika kufanikisha majukumu yaliyopangwa. Usimamizi huu siyo wa kulazimisha bali ni tabia ya kila mmoja kujituma katika eneo la kazi. Usimamizi wa majukumu una sura mbili: utekelezaji wa majukumu binafsi na utekelezaji wa majukumu uliyopewa na jamii. Mifano ya majukumu binafsi ni kama vile; kufanya kazi unazoagizwa nje na ndani ya darasa (kufagia, kupiga deki, kufuta ubao, kufuta utando wa buibui, kufyeka nyasi, kupanda miti na kumwagilia viunga vya bustani) bila kushurutishwa. Pia, utekelezaji wa majukumu ya nyumbani, pasipo kusukumwa au kusimamiwa na usimamizi wa majukumu tuliyopewa na jamii. Mifano ya majukumu haya ni kuwa kiongozi wa darasa, kiongozi wa klabu, kiongozi wa idara, au kiongozi wa nchi kwa kuwajibika kuwasimamia wengine ili kutimiza majukumu yao ukiongozwa na sheria, kanuni na taratibu.

**Angalia picha hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**




*Kielelezo namba 1: Kutekeleza majukumu unayopewa shuleni*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 86
17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Umeona majukumu gani yanatekelezwa katika picha hii?
2. Orodhesha majukumu mengine zaidi yanayoweza kufanyika shuleni na nyumbani bila usimamizi wa walimu, wazazi, au walezi.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu namna bora ya kutekeleza majukumu yako ya kila siku nyumbani na shuleni. Andika muhtasari wa majadiliano hayo, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Utayari wa kupokea majukumu na ushauri

Utayari ni hali ya mtu kukubali au kuwa kamili kwa ajili ya kufanya jambo fulani. Vilevile, utayari ni kukubali kupokea maagizo au majukumu na kuyatekeleza kulingana na maelekezo. Pia, utayari unajumuisha mtu kujisimamia mwenyewe katika kutekeleza majukumu na kuhakikisha kuwa utekelezaji wake wa kazi unakidhi viwango. Mwanafunzi mwenye usikivu mzuri yupo tayari kuyapokea na kuyatekeleza majukumu anayopewa kwa hiari. Hategemei malipo wala sifa kama tuzo ya upokeaji wa hayo majukumu. Aidha, hujisikia vizuri kutokana na kazi nzuri aliyoifanya. Pia, mwanafunzi anayependa kujituma ni mtu mwenye bidii na uwezo wa kujisimamia mwenyewe. Mwanafunzi huyu ni mwepesi kukubali ushauri ili kuboresha utendaji wa kazi zake.

Utayari wa kupokea majukumu huenda sambamba na utayari wa kukubali upungufu wako na ari ya kutaka kujifunza zaidi kwa kutafuta na kupokea ushauri. Upungufu wa utendaji ni utendaji usiokidhi viwango vilivyowekwa ikiwa ni pamoja na muda wa kumaliza kazi. Usimamizi wa majukumu unahitaji kufanya tathmini ya mara kwa mara ya utendaji ili kubaini upungufu uliopo. Mtu anayejisimamia mwenyewe hujitathmini na akigundua ana upungufu huushughulikia. Pia, anaweza kutafuta ushauri ili kukamilisha vyema majukumu yake.

Utayari wa kupokea majukumu vilevile upo katika kufanya yale ambayo hayako kwenye ratiba yako ya kila siku lakini ni muhimu kwa jamii. Hii

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

inahusisha yale yote ambayo yako nje ya darasa. Shughuli za nje ya darasa ni shughuli ambazo mwanafunzi anazifanya nje ya taratibu rasmi za darasani tofauti na masomo. Shughuli hizo ni kama vile kushiriki katika michezo mbalimbali, klabu za masomo, shughuli za elimu ya kujitegemea, usafi wa mazingira na kutunza bustani za maua. Mwanafunzi aliye tayari kupokea majukumu huyatekeleza kwa kasi, juhudi na maarifa bila kusukumwa au kusimamiwa. Kwa hiyo, utayari wa kupokea majukumu unajumuisha pia utayari wa kuyasimamia katika utekelezaji wake.

## Kupokea majukumu na kuwa tayari kuyatekeleza

Kupokea majukumu na kuwa tayari kuyatekeleza ni kipengele muhimu cha kusimamia majukumu. Kusimamia majukumu ni kufanya yale mambo tunayopaswa au kutakiwa kuyafanya kulingana na nafasi zetu katika jamii. Tunasimamia majukumu ambapo tunasimamia utekelezaji wa hayo majukumu. Kwa mfano, kiongozi wa darasa husimamia majukumu ya kuwanyamazisha wanafunzi wenzake wasipige kelele darasani, kutoa taarifa kwa mwalimu pale ambapo mambo hayaendi vizuri darasani na kuhakikisha kuwa wanafunzi wenzake wanafanya maagizo yatakiwayo. Utayari wa kutekeleza majukumu hayo huwa ni kipimo kikubwa cha ukomavu wa utashi wa binadamu.

### Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata

*Katika shule ya msingi Itamba kuna utaratibu wa wanafunzi kufanya shughuli za nje ya darasa. Shughuli hizo ni pamoja na michezo, kazi za elimu ya kujitegemea na usafi wa mazingira. Siku moja baada ya kengele kugongwa, wanafunzi wote walikusanyika kusikiliza mgawanyo wa kazi kutoka kwa mwalimu wa zamu. Kwa mujibu wa taratibu za shule yao, siku ya Alhamisi kila baada ya masomo, darasa la tano hupangiwa kufanya usafi wa mazingira. Wanafunzi walipangiwa kusafisha vyoo vya shule ambapo wanafunzi sita wa kiume walipangiwa kusafisha vyoo vya wanafunzi wa kiume. Wanafunzi sita wa kike walitakiwa kusafisha vyoo vya wanafunzi wa kike. Wote walipewa vifaa vya kufanyia usafi, ikiwa ni pamoja na sabuni , fagio na dawa za vyoo.*

*Wanafunzi wa kike waliondoka haraka ili kutekeleza jukumu walilopewa. Walipofika kwenye vyoo hawakuona maji na ukuta ulikuwa na utando wa buibui. Hivyo, baadhi yao walikwenda kuchota maji na wengine walitumia fagio kuondoa utando wa buibui na takataka nyingine. Walisafisha kuta na*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 88 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*sakafu na kuondoa utando wa buibui wote kwenye paa. Kisha wakamwaga dawa ndani ya matundu ya vyoo ili kuua wadudu na kuondoa harufu. Kwa muda mfupi walikamilisha jukumu walilopewa na mwalimu na walikuwa tayari kwa ukaguzi. Mwalimu alipopita kukagua kazi, aliwakuta wanafunzi wamemaliza kazi yao vizuri. Vyoo vyote vilikuwa vinang'aa kwa usafi na havikutoa harufu mbaya. Mwalimu aliwapongeza wanafunzi hao kwa kufanya kazi yao vizuri.*

*Mwalimu aliendelea kukagua usafi. Alipofika kwenye vyoo vya wanafunzi wa kiume aliwakuta baadhi yao wanacheza mpira. Wengine walikuwa wanachezea maji. Alipoingia kwenye vyoo vyao alikuta utando wa buibui ukutani. Kuta za vyoo zilikuwa chafu kwa michoro, maji yamemwagika kwenye sakafu na vyoo vinatoa harufu mbaya. Mwalimu hakuridhika na kazi yao. Aliwasisitiza umuhimu wa kupokea majukumu na kuyatekeleza kwa ufanisi.*

**Zoezi la 2**

1. Ni matendo gani yanayodhihirisha kuwa wanafunzi wa kike walikuwa na utayari wa kutimiza majukumu yao?
2. Je, wanafunzi wa kiume walitimiza wajibu wao? Eleza.
3. Una ushauri gani kwa wanafunzi wa kiume wenye tabia kama iliyooneshwa katika kisa hiki?
4. Nini faida za kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako jinsi utakavyomshauri mwanafunzi mvivu wa kufanya kazi ya kikundi darasani. Andika kwenye daftari mawazo uliyopata kwenye mjadala, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Uwepo wa utawala bora shuleni

Je, nini maana ya utawala bora? Bila shaka una picha ya aina fulani akilini mwako. Hebu jaribu kutafakari, ungependa mama, baba na walimu wako wakuongoze vipi? Pale unapokosea wakusaidie namna gani? Bila shaka majibu yako yatakuwa wakulee na kukuongoza katika utaratibu



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mzuri. Hayo matarajio yako ndiyo utawala bora. Utawala bora ni uongozi unaofuata misingi ifuatayo: kuzingatia sheria, kanuni na taratibu, haki na utoaji wa huduma za jamii kwa kiwango, kwa wakati na bila ubaguzi wa aina yoyote. Ili usimamiaji wa majukumu uweze kukamilika na kuwa na matokeo yanayotarajiwa, utawala bora ni jambo la msingi sana.

Uwepo wa utawala bora shuleni hupimwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora tuliyoainisha hapo juu. Hivyo basi, shule yenye utawala bora ni shule ambayo inazingatia sheria, kanuni na taratibu ilizojiwekea ili kuendesha mambo yake. Vilevile, ni shule ambayo viongozi, walimu na wanafunzi wanazingatia sheria walizojiwekea na hakuna miongoni mwao aliye juu ya sheria. Msingi mwingine wa utawala bora shuleni ni pamoja na ushirikishwaji wa wadau wote wa shule kuanzia uongozi, walimu na wanafunzi katika maamuzi mbalimbali ya shule. Huu ni utawala wa kidemokrasia unaozingatia na kuheshimu maoni ya kila mmoja shuleni. Maoni haya yanaweza kutolewa kwa namna mbalimbali ikiwemo kwa kutumia sanduku la maoni ambapo watu hutoa maoni yao kwa siri.

Misingi ya utawala bora shuleni inasaidia utekelezaji wa majukumu na uendeshaji mzuri wa shughuli za shule. Pia, utawala bora unaofuata sheria na haki husaidia kuzuia kutokea kwa migogoro shuleni.

**Soma kwa makini kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Hapo zamani za kale, kulikuwa na mfalme ambaye alikuwa anatawala nchi ya Kijito. Mfalme huyo aliitwa Kazimoto. Mfalme huyo aliongoza wananchi wake kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi yake. Alitenda haki kwa watu wote. Alitunza mali za umma kwa maslahi ya wananchi. Nchi ikawa katika hali nzuri kiuchumi na kiusalama, watu wakawa wanaishi kwa furaha na upendo. Siku moja mfalme Kazimoto alipata ugonjwa wa ajabu wa kutetemeka miguu na kushindwa kutembea. Wananchi wote walijitolea kwa moyo kumsaidia kiongozi wao hadi akapona kabisa.*

**Zoezi la 3**

1. Mfalme Kazimoto alikuwa na utawala wa namna gani?
2. Mfalme Kazimoto alipata ugonjwa gani?
3. Wananchi wa Kijito walikuwa na maisha ya namna gani?
4. Unafikiri ni kwanini wananchi walijitolea kumsaidia mfalme Kazimoto?



URAIA NA MAADILI STD V .indd 90 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako mkimshirikisha mwalimu wa somo mpange safari ya kwenda kujifunza mambo ya utawala bora katika ofisi ya serikali ya kijiji au mtaa.

## Utii wa sheria

Utii wa sheria ni nidhamu au usikivu wa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Ni msingi muhimu wa utawala unaozingatia demokrasia. Kwa hiyo utii wa sheria hurahisisha usimamizi wa majukumu, hufanya mambo yaende kimpangilio na kwa ustaarabu. Hili ni jambo la muhimu sana kwa kuwa uzingatiaji wa sheria husababisha matokeo mazuri. Ukiwa shuleni ni muhimu kufuata sheria na kanuni ili kufanya mambo yaende vizuri kwa utaratibu unaofaa. Huu utaratibu utawezesha shule yako iweze kuongozwa vizuri na kukidhi matarajio au malengo ya shule yako. Kuna sheria za aina mbalimbali, kama vile sheria za nchi, sheria za shule, sheria za kijiji au sheria za bunge.

Ukiwa kama mwanafunzi unapaswa kutii sheria za shule yako. Baadhi ya sheria hizo ni:

1. Kuwahi shuleni na mahali popote unapohitajika.
2. Kuvaa sare safi ya shule.
3. Hairuhusiwi kuvaa mapambo uwapo shuleni.
4. Hairuhusiwi kupiga kelele darasani na mahali popote penye mkusanyiko.
5. Ni lazima kuzingatia usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
6. Kila mwanafunzi ni lazima awe na nidhamu njema, utii na heshima ndani na nje ya darasa au shule kwa watu wa rika zote.
7. Hutakiwi kuwa mwizi, mdokozi, tapeli na mgomvi.
8. Kutii kengele ya shule haraka pindi inapogongwa.
9. Ni lazima kumtaarifu mwalimu wa malezi, wa darasa au wa zamu iwapo una tatizo la afya.
10. Ni lazima kuwa darasani siku zote za shule, utoro ni mwiko.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 91 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

11. Ni marufuku kushiriki vitendo vya kihuni pamoja na lugha chafu ya matusi, kebehi, dharau, uuzaji na unywaji wa pombe. Pia, ni marufuku kuuza na kutumia dawa za kulevya na uvutaji wa sigara.
12. Unatakiwa kutunza, kulinda hadhi ya shule, usalama wa mali na mazingira ya shule.
13. Ni marufuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi katika mazingira ya ndani na nje ya shule.

**Soma majibizano haya kati ya John na Hamisi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Hamisi:** Unajua kuwa moja ya sheria za shule ni marufuku kutumia au kuwa na dawa za kulevya?

**John:** Wee! Hamisi acha bwana, kwani umeona nini?

**Hamisi:** Nimekuona na msokoto wa bangi!

**John:** Mimi! (*anainua mikono juu*) wewe unaota nini, umeona wapi huo msokoto?

**Hamisi:** Njoo hapa nikukague mfukoni!

**John:** Achana na mimi bwana!

**Hamisi:** Lakini unajua sheria za shule zinakataza kuwa na vileo au kutumia dawa za kulevya?

**John:** Hamisi bwana. Najua! Basi nikupe hapo kidogo na wewe uvute?

**Hamisi:** Aaah, wapi! Kwa hiyo unanishawishi na mimi kuvuta bangi? Sasa nakupeleka kwa mwalimu.

**John:** Siyo hivyo, hapelekwi mtu hapa kwa mwalimu!

**Hamisi:** Kwani wewe hujajifunza madhara ya kuvuta bangi?

**John:** (*Kimya*)

**Hamisi:** (*Anamshika John mkono*) Twende kwa mwalimu, hii ni kwa faida yako.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 92 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. John anaonesha kufuata sheria za shule? Kwa nini?
2. Ni madhara gani yanaweza kumpata John kwa tabia ya kuvuta bangi?
3. Kuna wanafunzi wanaojihusisha na dawa za kulevya shuleni kwenu?
4. Wewe ungetoa ushauri gani kwa John?
5. Kuna tofauti gani kati ya tabia ya John na tabia ya Hamisi?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu namna mnavyoweza kuwashauri wanafunzi wanaotumia dawa za kulevya ili waache tabia hiyo. Andika mapendekezo hayo kwenye daftari lako, kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kuzingatia sheria na kanuni

Kuzingatia sheria na kanuni ni ufuataji wa taratibu kulingana na malengo yaliyowekwa au yaliyokusudiwa. Huu ni utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia sheria. Hili ni jambo muhimu sana katika kufanikisha malengo. Vilevile, uzingatiaji huu wa sheria husaidia kuepusha migongano na maslahi binafsi, huepusha migogoro baina ya mtu mmoja na mwingine, viongozi na wanafunzi au taasisi na wafanyakazi walio ndani yake. Hali hiyo huleta maelewano na ufanisi wa kazi wenye tija kwa wote. Katika nafasi yoyote utakayopewa unawajibu wa kuzingatia sheria na kanuni katika utendaji wako. Hii itasaidia kulinda utaratibu na majukumu ya utoaji wa haki.

**Zoezi la 5**

1. Orodhesha sheria za shule yako unazozitambua.
2. Je, sheria ulizoorodhesha ni tofauti au zinafanana na orodha iliyo kwenye kitabu chako?



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 93 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Kwa nini ni lazima kuwa na sheria na kanuni za shule?
4. Unafikiri ni madhara gani yanaweza kutokea iwapo sheria za shule zitapuuzwa?
5. Utamshauri nini mwanafunzi anayepuuzia sheria za shule?

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu faida ya kuzingatia kanuni na sheria za shule. Andika faida hizo kwenye daftari lako, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Zoezi la 6

**Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku:**

1. Mtu kuwa na utayari wa kupokea majukumu hufuatana na:
   (a) kujitambua na kuwa na utayari wa kupokea ushauri
   (b) kushindana na wenzako
   (c) kukataa ushauri kutoka kwa mtu yeyote
2. Usimamizi wa majukumu shuleni hufanywa na:
   (a) walimu peke yao
   (b) wanafunzi wenyewe tu
   (c) walimu wakishirikiana na viongozi wa serikali ya wanafunzi
3. Viongozi wote wanapaswa kuzingatia:
   (a) maendeleo yao tu
   (b) misingi ya utawala bora
   (c) utawala wa kiimla
4. Utii wa sheria:
   (a) haubagui kiongozi au mwananchi
   (b) bila shuruti hauwezekani
   (c) unasababisha ucheleweshaji wa majukumu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Mwalimu mkuu ana majukumu ya:
   (a) kupokea fedha za ada na kuzitumia kwa matumizi yake binafsi
   (b) kuongoza na kusimamia mambo yote shuleni
   (c) kuadhibu wanafunzi kwa uonevu
6. Sanduku la maoni husaidia:
   (a) kutotunza siri za wanafunzi
   (b) kuwaficha walimu kinachoendelea shuleni
   (c) kuwasilisha maoni kwa siri
7. Kiongozi bora ni:
   (a) mtu anayependwa na watu wengi
   (b) mtu anayetawala kwa kufuata haki
   (c) mtu aliyechaguliwa kwa kura nyingi
8. Migogoro shuleni itakwisha endapo:
   (a) wanafunzi wote wakorofi hawatafukuzwa shule
   (b) walimu watashirikiana na baadhi ya wazazi
   (c) shuleni kutakuwa na uwazi na uongozi unaofuata sheria na haki

## Zoezi la 7

Katika sentensi zifuatazo andika neno **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na neno **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi.

1. Majukumu ni shughuli ambazo mtu anapaswa kuzitekeleza. _________
2. Usimamizi wa shughuli ni kazi ya kinyapara. _________
3. Ili kutimiza majukumu hapana budi kusukumwa na kusimamiwa. _________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Mwanafunzi mwenye usikivu mzuri yupo tayari kuyatimiza majukumu anayopewa kwa kushurutishwa.________
5. Kupokea ushauri ni kukubali mapungufu na ni njia ya kutaka kujifunza zaidi. ________
6. Utawala bora ni uongozi unaotumia sheria kwa maslahi ya watu wachache. ________
7. Utii wa sheria husaidia kufanya mambo yaende kwa mpangilio.________
8. Kutokuwa mtoro ni moja ya mfano wa sheria za shule.________
9. Usafi wa mazingira ya shule ni wajibu wa wanafunzi wachache. ________
10. Utawala bora huleta amani na kutatua migogoro katika jamii.________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Kidhi | kutosheleza mahitaji |
| Tafakuri | mawazo ya kina ya mtu kuhusu jambo fulani |
| Ufanisi | hali ya kutenda kazi kwa viwango vinavyotakiwa kwa kutumia muda uliopangwa |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kuwa mvumilivu

Katika sura hii, utajifunza vitendo vya uvumilivu katika kukuwezesha kukabiliana na changamoto za maisha ya kila siku. Vilevile, utajifunza kutumia uzoefu wa watu mbalimbali katika kushughulikia changamoto hizo. Aidha, utajifunza athari za kimwili, kiafya na kisaikolojia zinazotokana na kushindwa kutatua changamoto za maisha.

### Matendo ya uvumilivu

Uvumilivu ni hali ya ustahimilivu wa changamoto au shida mbalimbali za maisha. Katika kipengele hiki utajifunza matendo ya uvumilivu katika kutambua hisia hasi dhidi ya watu wenye asili tofauti na ya kwako kwa mfano rangi, kabila au imani. Ni vyema ukatambua kuwa kuna imani tofauti na kuziheshimu hata kama hazifanani na za kwako. Unatakiwa kukubali kuishi na watu wenye imani, itikadi na mitazamo tofauti na yako kwenye jamii unamoishi.

### Tafakari mambo yafuatayo:

(i) Unaposikia kengele ya kanisani inagogwa saa kumi na mbili alfajiri

(ii) Unaposikia sauti ya adhana inasomwa saa kumi na moja alfajiri

(iii) Katika kikundi chenu wanafunzi wenzako wanajadiliana kwa lugha ya kabila lao bila kukushirikisha wala kukujali

(iv) Mwanafunzi mwenzako anapiga kelele na kuwachokoza wenzake wakati wa muda wa kujisomea darasani

**Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Kadoda:** Habari gani Mwanalomi?

**Mwanalomi:** Nzuri Kadoda! Vipi hali?

**Kadoda:** Ni nzuri tu, habari za darasani kwenu?

**Mwanalomi:** Darasa lile ninalosoma siliwezi kabisa, ningekuwa na uwezo ningehama.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 97 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kadoda:** Kwa nini Mwanalomi? Mbona darasa lenu linasifika kwa kufanya vizuri?

**Mwanalomi:** Ahaa! Ni kweli, lakini pamoja na kuwa na wanafunzi wanaofanya vizuri wengine ni watundu na wachokozi sana.

**Kadoda:** Kumbe hilo tu, ndilo linakukosesha raha ?

**Mwanalomi:** Wewe huoni kama ni tatizo?

**Kadoda:** Hata darasani kwetu wapo, tunawahimiza kuacha tabia yao na kiongozi wa darasa anaposhindwa kuwashauri hutoa taarifa kwa mwalimu.

**Mwanalomi:** Kumbe! inawezekana kusoma darasani na wanafunzi wenye tabia tofauti?

**Kadoda:** Ndio, ni muhimu kuwashauri na bila kuwatenga, hatimaye watabadilika.

**Zoezi la 1**

1. Je, ni mambo gani yanayomuumiza Mwanalomi katika darasa lake?
2. Kadoda alimshauri nini Mwanalomi?
3. Umejifunza nini katika sura hii kuhusu matendo ya uvumilivu?

**Kazi ya Kufanya**

Jadili na mwalimu wako kuhusu namna ya kufanya matendo ya uvumilivu kwa wanafunzi wenzako darasani. Andika majibu yako kwenye daftari. Kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kutambua changamoto katika maisha ya kila siku

Changamoto za kimaisha ni mambo anayokabiliana nayo mtu katika maisha yake ya kila siku. Baadhi ya changamoto hizo ni kufiwa na watu unaowategemea kama vile wazazi au walezi. Changamoto nyingine ni pamoja na kutengana kwa wazazi au walezi, kufungwa kwa wazazi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 98 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

au walezi, wazazi au walezi kuacha kazi, wazazi au walezi kupatwa na ulemavu. Vilevile, changamoto inaweza kutokana na majanga mbalimbali ya kiasili kama vile mafuriko, tetemeko la ardhi au kimbunga. Changamoto nyingine hutokana na matukio kama kufanyiwa vitendo vya ukatili mfano, kulawitiwa au kubakwa, kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji kama vile kuambiwa maneno ya kejeli na kutukanwa. Aidha, matatizo ya afya kwa wazazi au walezi, matatizo ya afya kwa wanafunzi, kupata ujauzito, kufukuzwa shule, kutokukubalika au kutengwa na familia ni baadhi ya changamoto za kimaisha. Lakini lengo la uvumilivu si katika kuvumilia mateso bali uvumilivu huo utumike kutafuta njia sahihi za kutatua changamoto za maisha ya kila siku.

## Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Dilasi na Jefu ni marafiki wanaosoma darasa moja. Walianza urafiki wao baada ya kuona wote wanajitahidi darasani na walikuwa wanashindana kushika nafasi ya kwanza. Maendeleo ya Jefu kitaaluma yalishuka baada ya baba yake kusimamishwa kazi. Jefu alianza kutohudhuria shule. Alikuwa anaaga nyumbani kuwa anakwenda shuleni, lakini hafiki huko. Alijihusisha na makundi mabaya na kujifunza tabia za udokozi na uvutaji bangi. Rafiki yake Dilasi alikuwa akimshawishi aende shuleni, lakini alisita na kusema kuwa hana vifaa vya kutumia shuleni. Dilasi alisikitika sana na aliwaeleza wazazi wa Jefu. Wazazi wa Jefu walimsihi mtoto wao avumilie hiyo hali na arudi shuleni. Pia, walimsihi kuongeza bidii ili awe msaada wao hapo baadaye. Walimsisitiza kuwa akikata tamaa hatakuwa na maisha mazuri. Jefu aliona kama haiwezekani. Wazazi wa Jefu waliendelea kumsihi mtoto wao kwa kushirikiana na walimu wake.

Jefu aliafiki ushauri wa wazazi wake pamoja na walimu akarudi shuleni. Rafiki yake Dilasi alifurahi sana kwa Jefu kuendelea na masomo. Baada ya muda mfupi, Jefu alianza kufanya vizuri katika mitihani yake ya mihula na kushika nafasi ya kwanza pamoja na changamoto alizonazo.

### Zoezi la 2

1. Jefu alikutana na changamoto zipi?
2. Je, wewe ungekuwa Jefu ungefanya nini?



URAIA NA MAADILI STD V .indd 99 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Uamuzi wa Jefu katika kukabiliana na changamoto ulikuwa sahihi? Kwa nini?
4. Toa mifano ya matukio yaliyowatokea ndugu au marafiki zako yanayofanana na yale yaliyomtokea Jefu.
5. Orodhesha mambo utakayofanya kuwasaidia wanafunzi wenzako wenye changamoto mbalimbali.

**Kazi ya Kufanya**

Katika eneo lako ni changamoto gani ambayo rafiki yako aliwahi kukabiliana nayo? Ulichukua hatua gani katika kumsaidia? Andika katika daftari lako hatua ulizochukua, kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo

## Kupokea mabadiliko katika maisha

Ni muhimu kuamini kuwa kubadilisha maisha yako kupo ndani ya uwezo wako. Mabadiliko ya maisha yako yatatokana na wewe mwenyewe. Hivyo, jenga matumaini na tabia ya kujiamini. Jiamini kwamba unaweza kuhimili mabadiliko na kuyafanya kuwa sehemu ya maisha. Unapojiamini utajenga tabia ya uvumilivu na kupokea mabadiliko bila kukata tamaa.

**Soma shairi hili, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Hakika ninakwambia, maisha hubadilika,
   Japo yametukalia, lakini tutayashika,
   Maisha kama tabia, yanaweza badilika,
   Kuwa na matumaini, hili nalo litapita.

2. Tafadhali jiamini, maisha kuyakabili,
   Kuwa na matumaini, waweza kuyahimili,
   Mshirikishe Manani, tatizo kulikabili,
   Kuwa na matumaini, hili nalo litapita.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 100 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Ni vyema ukajirudi, ushirikishe mwenzako,
Mjipatie miradi, na mazao yenye soko,
Liwe joto au baridi, epukeni sokomoko,
Kuwa na matumaini, hili nalo litapita.

4. Kuwa na mawazo chanya, kuyaepuka majonzi,
Michezo waweza fanya, mwili upate ulinzi,
Mangapi umeshafanya, ukavivuka viunzi,
Kuwa na matumaini, hili nalo litapita.

**Zoezi la 3**

1. Ni mambo gani mtunzi anatushauri katika ubeti wa pili ili tuweze kupokea mabadiliko katika maisha?
2. Mtunzi anatuasa mambo gani ili kuyaepuka majonzi na mwili upate ulinzi wakati wa kupokea mabadiliko katika maisha?
3. Katika ubeti wa tatu, mtunzi anatushauri mambo gani ili kuweza kubadili changamoto za maisha kuwa fursa?

**Kazi ya Kufanya**

Andika kisa ambacho ni changamoto uliyowahi kabiliana nayo, uoneshe hatua ulizochukua na watu uliowashirikisha. Kisa hicho kisipungue maneno 100.

## Umuhimu wa kuwa mvumilivu

Kuna manufaa makubwa ya kuwa mvumilivu unapokuwa na changamoto. Manufaa hayo ni pamoja na kujenga ufanisi katika utendaji wako wa kila siku. Manufaa mengine ni kukua kitaaluma, kupata marafiki wanaofaa, kukua kifikra na kupevuka kimawazo na kiakili. Marafiki unaokuwa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 101 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nao bega kwa bega wakati wa changamoto ndiyo marafiki wa kweli. Wakati wa changamoto hakikisha unapata ushauri unaofaa kutoka kwa watu mbalimbali, kumbuka kuwa changamoto ni fursa ya kukuimarisha maishani.

**Soma shairi hili kwa makini, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Napenda kuwakumbusha, jamani mnisikie,
   Uvumilivu onesha, yalo mema jipatie,
   Malengo kuorodhesha, kwa bidii jifanyie,
   Changamoto upatazo, ni sehemu ya maisha.

2. Changamoto ulonazo, nyuma zisikurudishe,
   Epukeni matatizo, makundi  mjiepushe,
   Hakuna njia katizo, kufanikisha maisha,
   Changamoto upatazo, ni sehemu ya maisha.

3. Changamoto zakupata, kila mara kukutisha,
   Zisikuache kujuta,  maisha kuimarisha,
   Watu wengi wamepita, wameyashinda maisha,
   Changamoto upatazo, ni sehemu ya maisha.

4. Unapopata utata, wenzako kushirikisha,
   Epuka kuwa mtata, ahadi kukamilisha,
   Wahanga kuwafuata, misaada harakisha,
   Changamoto upatazo, ni sehemu ya maisha.

5. Fanya kazi ifaayo, ya halali kwa kipato,
   Kila kazi ufanyayo, haikosi changamoto,
   Ifanye kazi kwa moyo, kufikia zako ndoto,
   Changamoto upatazo, ni sehemu ya maisha.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd   102
17/08/2021   11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. Ni kwa jinsi gani unazitatua changamoto unazokabiliana nazo?
2. Kwa nini unafikiri changamoto ni kitu cha kukuimarisha kimaisha?
3. Orodhesha mambo ya kuzingatia unapopatwa na changamoto.
4. Unamshauri nini mwenzako anayepitia changamoto?
5. Ni mambo gani unaweza kufanya ili kukabiliana na changamoto unazopitia?

**Kazi ya Kufanya**

Orodhesha mambo matano utakayofanya kuanzia sasa ili kukabiliana na changamoto zako na za wanafunzi wengine. Wasilisha kazi kwa mwalimu wa somo.

## Athari zinazotokana na kushindwa kutatua changamoto: Kimwili, kiafya na kisaikolojia

Mtu anaposhindwa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha hupata athari za kimwili, kiafya na kisaikolojia. Athari za kimwili ni hali ya maumivu katika mwili ambayo yanaweza kusababisha majeraha, ulemavu na hata kupooza. Vilevile, hali hii inaweza kusababisha kupata magonjwa kama shinikizo la damu na vidonda vya tumbo hivyo, kumfanya mtu ashindwe kutimiza majukumu yake kikamilifu.

## Athari za kisaikolojia

Kutokana na kipengele kilichotangulia, umetambua kwamba changamoto zinapomkabili mtu humfanya kuwa njia panda na kushindwa kufanya uamuzi ulio sahihi. Hivyo, hujikuta anapata athari za kisaikolojia. Saikolojia ni sayansi ya kuchunguza tabia, mitazamo, imani walizonazo watu na namna inavyoathiri mambo wayatendayo. Baadhi ya athari za kisaikolojia ni kama vile, kuwa na hofu, kutojiamini na kupata mshituko. Hali hii isipodhibitiwa mapema, huweza hata kusababisha kifo.

Athari za kisaikolojia husababisha akili ya mtu kushindwa kuhimili matatizo yanapotokea. Pia, huweza kusababisha mtu kujiona dhaifu na kujenga

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hali ya kulalamikia wengine kuwa chanzo cha matatizo yake. Unyonge pia ni athari ya kisaikolojia na kwa upande wa mwanafunzi anaweza kushuka kitaaluma au kuacha shule kwa kuwa huona hana namna nyingine ya kukubaliana na changamoto zinazomkabili.

**Soma kwa makini kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Bupe ni msichana anayesoma darasa la tano katika Shule ya Msingi ya Songwe. Alikuwa anaishi maisha mazuri pamoja na wazazi wake. Baba alikuwa mkulima wa mazao ya chakula na biashara na mama yake alikuwa mfugaji wa kuku kwa njia ya kisasa. Wazazi wake walikuwa na kipato cha kutosheleza matumizi ya familia na kubakiwa na ziada. Kwa kuwa Bupe alikuwa ni mtoto wa pekee katika familia yake, alipewa malezi bora ya kuridhisha na wazazi wake walimpatia kila alichohitaji.*

*Siku moja walipanga safari ya kwenda kijiji cha Sange, kilichopo wilaya ya Ileje mkoani Songwe. Wakiwa safarini gurudumu la mbele la gari walilokuwa wakisafiria lilipasuka na hivyo kusababisha ajali mbaya sana. Ajali hiyo ilisababisha wazazi wote wawili wa Bupe kupoteza maisha papo hapo. Bupe alipata majeraha na kupelekwa hospitali kutibiwa. Baada ya mazishi ya wazazi wake, Bupe alikuwa mpweke mno. Hali hii ilimsababishia kushindwa kusoma vizuri. Katika mtihani wake wa kuhitimu darasa la saba, hakufanya vizuri. Hivyo alirudi kijijini kwao. Huko alilelewa na babu na bibi yake na hapo ikawa mwisho wa ndoto zake nyingi alizojiwekea.*

### Zoezi la 5

1. Ni mambo gani yalisababisha Bupe akate tamaa?
2. Wewe ungekuwa Bupe ungetumia mbinu gani kukabiliana na changamoto aliyopata?
3. Unamshauri nini mwenzako ambaye anapitia changamoto kama za Bupe?

### Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wenzako namna mtakavyoweza kumsaidia mwanafunzi mwenzenu mwenye matatizo ya kisaikolojia.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 104 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutumia uzoefu wa watu katika kushughulikia changamoto za maisha

Je, uliwahi kumwona mtaalamu wa ushauri nasaha na unasihi aliyepo shuleni kwako kupata ufumbuzi wa changamoto zako? Je, uliwahi kuomba ushauri kwa watu wazima wenye uzoefu wa maisha ili kutatua changamoto zako? Je, uliwahi kutafuta watu waliopitia changamoto kama zako ili uweze kutumia uzoefu wao kutatua changamoto zako za maisha?

Ni muhimu tutambue kuwa, changamoto ni sehemu ya maisha yetu. Pia, wewe siyo wa kwanza kukabiliwa na changamoto za kimaisha. Changamoto zisikufanye ukate tamaa. Kumbuka, inabidi maisha yaendelee baada ya changamoto iliyokupata. Kuna watu waliwahi kupitia changamoto hizo na wakapita salama. Hivyo, ni vyema kutumia uzoefu wao katika kutatua changamoto zako. Vilevile, katika jamii yako kuna watu wazima wenye uzoefu mkubwa zaidi yako kimaisha, inakupasa kuwatumia kwa kuomba ushauri. Hali kadhalika, shuleni kuna walimu ambao ni wataalamu waliobobea katika ushauri nasaha na unasihi. Ni muhimu kuwatumia ili kupata ufumbuzi wa changamoto zinazotokana na mabadiliko ya maisha yako. Fikiria ni kwa namna gani unashirikiana na wazazi au walezi wako katika kutatua changamoto zinazoikabili familia yenu?

**Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Roza:** Mama, mbona siku hizi hatupiki nyama na wala hutununulii nguo mpya?

**Mama:** Mwanangu Roza, siku hizi maisha yamebadilika. Hali ya uchumi wa familia imeyumba. Si unakumbuka duka letu liliungua moto?

**Roza:** Ndiyo mama!

**Mama:** Hapo ndipo changamoto zilipoanza. Maana kile ndicho kilichokuwa chanzo kikuu cha kipato chetu. Mali za dukani na fedha zote ziliungua.

**Roza:** Sasa tunafanyaje mama?

**Mama:** Hata mimi sijui, labda tushauriane cha kufanya.

**Roza:** Mimi nimepata wazo mama.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 105 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mama:** Ehee! Wazo gani mwanangu?

**Roza:** Mimi ninashauri tulime bustani ya mboga kama wanavyofanya wazazi wa rafiki yangu Monika. Mboga ni adimu kwa sasa hapa kijijini kwetu. Tutapata wateja wengi sana. Tukiuza mboga tutapata fedha ya kununulia nguo, mchele na vitoweo. Pia, tutapata mtaji wa kuanzisha duka lingine. Au mama unaonaje?

**Mama:** Wazo zuri sana mwanangu. Ngoja kesho tuanze kuandaa hiyo bustani.

**Roza:** Sawa mama.

## Zoezi la 6

1. Ni janga gani liliwapata familia ya Roza?
2. Je, wewe ungekuwa Roza, ungemshauri nini mama yako ili kuongeza kipato cha familia yenu?
3. Taja njia tatu mbadala unazoweza kutumia kutatua changamoto za kipato katika familia yenu.

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana katika vikundi kuhusu changamoto za kila mmoja wenu anazozipata akiwa nyumbani. Andika changamoto hizo kwenye daftari lako kisha eleza jinsi utakavyotatua changamoto hizo. Mkabidhi mwalimu wa somo daftari lako.

## Zoezi la 7

Andika **Kweli** au **Si Kweli** katika sentensi zifuatazo:

1. Uvumilivu unamfanya mtu astahimili changamoto. _________
2. Ni vizuri kuwaacha watu wenye imani au itikadi tofauti wakae peke yao ili kuepusha migogoro. _________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Ni jambo la busara kuwa mstahimilivu kwa watu wenye mitazamo tofauti. ________
4. Kuvumilia katika maisha ya kila siku ni pamoja na kukubali mabadiliko hasi. ________
5. Unapopata changamoto ni mwisho wa ndoto zako za maisha. ________
6. Wazazi wakishindwa kukupa mahitaji ya shule, lazima ushuke kimasomo. ________
7. Unapopatwa na changamoto usijiingize katika makundi mabaya. ________
8. Unaweza kugeuza changamoto ikawa fursa. ________
9. Huwezi kutumia ushauri wa watu kutatua changamoto zako. ________
10. Changamoto ikitumiwa vizuri humnoa mtu kimaisha. ________
11. Mtoto hawezi kumshauri mzazi inapotokea changamoto ya maisha katika familia. ________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Fursa | nafasi au mwanya wa kuweza kufanya jambo fulani |
| Taaluma | ujuzi au maarifa maalumu yanayopatikana kwa kusoma |
| Utata | hali isiyo na jibu la haraka |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Kufikia malengo

Darasa la nne ulijifunza kuwa na mtazamo chanya, fikra za kujitegemea na kujenga udadisi ili kufikia malengo. Katika sura hii, utajifunza kuhusu mikakati ya kufikia malengo, kutathmini utendaji na nidhamu binafsi. Pia, utajifunza namna ya kuchanganua mambo kiyakinifu na kufanya ulinganifu katika ujifunzaji ili kufikia malengo yako.

### Mikakati ya kufikia malengo

Je, neno malengo lina maana gani? Malengo ni mambo unayodhamiria kufikia au kutekeleza. Malengo hukupa mwongozo na mwelekeo katika kufanya jambo ili kupata matokeo unayotarajia. Vilevile, malengo hukuwezesha kuweka nia katika kile unachokilenga na kukufanya uelekeze nguvu zako kwenye kitu hicho, badala ya kushika hiki na kile. Malengo yanakuwezesha kufahamu unatakiwa kufanya nini, wakati gani na kwa nani. Baada ya kujiwekea malengo utaweza kubaini ni uamuzi gani unafaa na ni upi haufai kwa ajili ya kutimiza malengo hayo. Je, wewe umewekaje malengo na mikakati ya kuyafikia?

Ili uweze kufikia malengo yako, ni vyema ukazingatia mambo ya msingi kama vile kuainisha matarajio yako kwanza. Kwa mfano, ungependa kufikia kiwango gani cha elimu? Ungependa kufanya kazi gani? Hakikisha malengo yako yanapimika, muda wa utekelezaji unafahamika na yanatekelezeka. Ukiwa mwanafunzi, ni vyema kuangalia iwapo malengo yako yanalingana na uwezo wako. Malengo yako yasiwe ya juu sana na yasiwe ya chini sana. Andaa mpango kazi wako ambao utakusaidia kufikia malengo yako. Weka vigezo vya upimaji katika kutekeleza malengo yako. Kwa mfano, “Ili niweze kufikia lengo langu sitakiwi kupata chini ya alama 70 katika somo lolote.” Anza kutekeleza mpango wako wa kazi kwa umakini na zingatia vipaumbele. Tumia ujuzi sahihi, au omba ushauri wa kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza wakati wa kupanga njia bora za kufikia matarajio uliyojiwekea.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 108 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma kwa makini mazungumzo ya Baba na Jumbe, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Jumbe:** Shikamoo baba.

**Baba:** Marahaba Jumbe, habari za shule?

**Jumbe:** Nzuri tu baba.

**Baba:** Ungependa kufanya kazi gani utakapohitimu masomo yako?

**Jumbe:** Ningependa kuwa daktari wa kutibu binadamu pindi nitakapo hitimu masomo yangu.

**Baba:** Vizuri, je, umeweka malengo gani kufikia ndoto zako?

**Jumbe:** Ni kusoma kwa bidii ili kufikia elimu ya sekondari, kisha nitachagua masomo ya sayansi, ambayo yataniwezesha kufikia ndoto na malengo niliyojiwekea.

**Baba:** Vyema Jumbe, weka bidii katika masomo yako, huku ukiwa na nidhamu nzuri.

**Jumbe:** Asante baba nitafanya hivyo.

**Zoezi la 1**

1. Jumbe ana matarajio ya kufanya kazi gani pindi atakapohitimu masomo yake?
2. Je, Jumbe atatumia njia gani kufikia malengo yake?
3. Baba yake Jumbe alimshauri nini mwanawe?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kwamba ungependa kuwa nani na utatumia mikakati gani kufikia malengo hayo. Wasilisha mkakati wako kwa mwalimu wa somo.

## Tathmini ya utekelezaji wa malengo

Tathmini ya utekelezaji wa malengo hufanyika wakati na baada ya utekelezaji. Wakati wa utekelezaji unachunguza mbinu unazotumia ili kujua

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kama zinafaa ama la. Kwa mfano, wewe kama mwanafunzi unapaswa kutathmini maendeleo yako siku hadi siku, au wiki hadi wiki na hata mwezi hadi mwezi, au mwaka hadi mwaka. Hii itakusaidia kufikia malengo yako ambayo ni ufaulu mzuri. Tathmini hii unaweza kuifanya kwa kujiuliza: Je, muda ninaotumia kujifunza unatosha? Je, ratiba niliyojiwekea ninaifuata? Je, darasani ninamsikiliza mwalimu? Je, rafiki zangu wananisaidia au ni kikwazo? Je, ninajibu na kuuliza maswali darasani? Je, ninakamilisha kazi za darasani kwa wakati?

Ukigundua kuwa muda unaotumia kujifunza ni mdogo utauongeza, au ukigundua kuwa darasani unafanya mambo mengine badala ya kumsikiliza mwalimu utabadilika. Tathmini nyingine unaifanya baada ya utekelezaji wa malengo yako; kwa mfano, kama lengo lako lilikuwa kufaulu mtihani wa mwisho wa mwaka, utapima kama ulifikia kiwango kizuri cha ufaulu ulioutarajia. Unaweza kujiuliza maswali kama; Je, kiwango nilichofaulu kinatosha? Je, ni mambo gani yalichangia ufaulu wangu kuwa hivi? Je, nitaboresha wapi? Nifanye nini ili ufaulu wangu uwe mzuri zaidi?

Hata hivyo, unaweza kupata vikwazo mbalimbali wakati wa kutekeleza malengo yako. Vikwazo hivi ni changamoto za kawaida katika utendaji kazi wowote. Kwa mfano, inaweza ikatokea dharura nyumbani ikaingiliana na ratiba yako uliyojiwekea. Linapotokea jambo kama hili, unaweza kutafuta njia mbadala ili lengo lako liweze kufikiwa. Kwa mfano, unaweza kufidia muda uliopotea kwa kupunguza muda wa mazungumzo yasiyo ya lazima na michezo.

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Athumani na Neema ni wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Muungano. Walikuwa wakisoma kwa pamoja na wote wawili walijiwekea malengo ya kufanya vizuri katika mitihani yao ya kuhitimu darasa la saba. Neema ana majukumu aliyokuwa nayo ya kumsaidia mama yake kupika na kuosha vyombo. Hata hivyo, aliweka juhudi na kufuata ratiba binafsi ya kujisomea.*

*Athumani akiwa nyumbani alitumia muda mwingi kucheza na kwenda kwenye vibanda vinavyoonesha filamu. Alitumia muda mchache kujisomea na mara nyingine hakusoma kabisa. Matokeo ya darasa la saba yalipotangazwa, Athumani hakuchaguliwa wakati Neema alichaguliwa kwenda sekondari. Kitendo hicho kilimuumiza sana Athumani na alimwendea Neema na*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 110 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*kumwambia kwamba pamoja na kuweka malengo hajafaulu. Neema alimuelimisha Athumani kwamba kuweka malengo ni jambo moja na kuyatekeleza ni jambo jingine. Neema alimweleza Athumani kwamba yeye alipanga ratiba yake na kuitekeleza vizuri, licha ya kazi nyingi alizokuwa akizifanya nyumbani.*

*Athumani alitambua kosa alilolifanya, hivyo aliwaomba wazazi wampe nafasi tena ajiunge katika shule zisizo za serikali, ili aweze kupata elimu ya sekondari. Tangu hapo, Athumani alisoma kwa bidii na kwa kuzingatia mpango kazi wake aliojiwekea. Hatimaye, wote wawili Athumani na Neema walihitimu elimu ya sekondari na kufaulu vizuri kwa kupata daraja la kwanza.*

**Zoezi la 2**

1. Neema na Athumani walijiwekea malengo gani ya pamoja hapo awali?
2. Kwa nini Neema alifanikiwa katika malengo waliyojiwekea hapo awali?
3. Bainisha uzembe alioufanya Athumani na kusababisha kutofikia malengo yake ya awali.
4. Je, Athumani alipojiwekea mpango kazi kwa mara ya pili aliutekeleza?
5. Una ushauri gani kwa wanafunzi wenye tabia kama ya Athumani?
6. Orodhesha matendo utakayofanya kuanzia sasa kutokana na uliyojifunza kwenye kisa hiki.

**Kazi ya Kufanya**

Andaa malengo yako na namna utakavyoyatekeleza ndani ya mwaka mmoja, kisha wasilisha kwa mwalimu wako wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutatua changamoto katika utekelezaji wa malengo

Bila shaka katika kutekeleza malengo yako, umeweza kukabiliana na changamoto mbalimbali. Je, ulitumia njia gani kukabiliana na changamoto hizo?

**Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mwalimu** Juma, mbona huna furaha? Una tatizo gani?

**Juma** Nipo kawaida mwalimu. Nilikuwa nawaza matatizo ya kifamilia.

**Mwalimu** Ehee! Unaweza kuniambia ni matatizo gani hayo?

**Juma** Kila siku wazazi wangu, nikiwaomba fedha ya kununulia vifaa vya shule wanasema hawana. Maandalizi yangu ya masomo ni hafifu maana hata nyumbani hawanipi muda wa kujisomea. Naona kama hawanipendi na hawataki nifikie malengo yangu.

**Mwalimu** Pole sana Juma. Je, uliwahi kumshirikisha mtu yeyote juu ya changamoto hizo?

**Juma** Hapana mwalimu.

**Mwalimu** Sawa. Nitaongea na wazazi wako ili tupate ufumbuzi wa pamoja wa changamoto zinazokukabili. Vifaa vyako vya shule navyo vitapatikana. Usiwaze sana. Sawa Juma?

**Juma** Asante sana mwalimu.

**Mwalimu** Siku nyingine ukiwa na changamoto katika maisha, washirikishe watu unaowaamini. Watakupa ushauri unaofaa na kwa wakati. Usikae unawaza tu, unaweza kufikia maamuzi yasiyofaa. Sawa Juma?

**Juma** Sawa mwalimu, asante sana kwa ushauri wako.

### Zoezi la 3

1. Orodhesha changamoto zinazomkabili Juma.
2. Je, mwalimu amemsaidiaje Juma?
3. Unapokabiliwa na changamoto za maisha, unatakiwa ufanye nini?
4. Taja njia nyingine za ufumbuzi wa changamoto zinazoweza kutumika katika kufikia malengo yako.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 112 17/08/2021 11:19
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadili na mwenzako kuhusu changamoto zinazowakabili baadhi ya wanafunzi wenzenu wa darasa la tano, kisha muoneshe mikakati mtakayotumia kuwasaidia ili wafikie malengo yao. Andika mikakati hiyo katika daftari lako, kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kuwa na nidhamu

Kuwa na nidhamu ni moja ya mambo muhimu sana katika kufikia malengo yako. Nidhamu ni uwezo wa kujiongoza. Baadhi ya matendo yanayoonesha nidhamu ni kutenda jambo kwa ufanisi bila kusimamiwa. Mwanafunzi mwenye nidhamu anajituma kufanya kazi kwa bidii nje na ndani ya darasa. Anafuata kanuni na sheria za shule bila kusimamiwa. Mwanafunzi huyu hujiwekea malengo yake na anajituma kuyatekeleza bila kusimamiwa.

Je, unawezaje kujijengea na kuwajengea wengine nidhamu? Unaweza kujijengea nidhamu kwa kujijengea tabia ya kujiamini. Unapojiamini utaongeza bidii na kutafuta misaada mbalimbali ili uweze kufanya vizuri zaidi. Kujiamini ni motisha inayotoka ndani yako na nguvu ya pekee katika kufanikisha mambo. Hata motisha zinazotoka nje kama kusifiwa hazina nguvu kama kujiamini. Unaweza pia kuwajengea wenzako uwezo wa kujiamini. Kwa mfano, kutomkosoa mwenzako kwa njia isiyo ya kistaarabu. Kukosoa kusiko na ustaarabu kunaweza kudhoofisha uwezo wa mtu wa kutenda. Pia huzaa woga, chuki na hofu ya kutenda. Kamwe, usitumie lugha ya kumkatisha tamaa mwenzako. Lugha ya kukatisha tamaa hushusha morali na kuvunja nguvu. Hata wewe mwenyewe unatakiwa kuyakwepa mazingira ya kutendewa vitendo hivyo.

Je, umewahi kumuona mtu ambaye hufanya kazi bila usimamizi? Anakuwa mtu wa aina gani? Wewe umewahi kufanya kazi bila kusimamiwa? Ulijisikiaje pale ulipofanya hivyo? Mtu anayefanya kazi bila usimamizi huonesha ana nidhamu. Ana kiwango kikubwa cha kujiamini na kujitawala na hicho ndicho kipimo cha utu wake.

Watu wenye nidhamu ya kujituma, hufanya kazi kwa ari na moyo. Pia, hutumia vipaji vyao kwa kiwango cha juu sana. Vilevile, humiliki ubora wa kazi ambayo mara nyingi huwa ni matokeo ya kufanya kazi kwa kujituma.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 113 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kusimamiwa mara nyingi hujenga woga na hali ya kutojiamini jambo ambalo hupunguza ufanisi. Faida nyingine ni kuaminika na kukubalika. Mtu mwenye nidhamu huweza kukabidhiwa majukumu makubwa na kukubalika katika nafasi muhimu za uongozi.

**Zoezi la 4**

1. Nini maana ya nidhamu?
2. Orodhesha matendo ya mtu mwenye nidhamu?
3. Orodhesha matendo utakayoanza kufanya kuanzia sasa ili kujenga nidhamu?
4. Je, nidhamu itakusaidiaje kujiwekea malengo na kuyatekeleza?

**Kazi ya Kufanya**

Orodhesha vitendo vya wanafunzi ambao hawana nidhamu. Bainisha njia utakazotumia kuwashauri wabadilike, kisha andika kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu

Uyakinifu ni tabia ya kutaka kujua mambo kwa kina kwa njia ya kuhoji. Tabia ya uyakinifu humuwezesha mtu kuhoji mambo au matukio yanayotokea, kufanya ulinganifu juu ya anachokijua katika kujifunza, kutathmini utendaji wake na kuzingatia maadili wakati wa kutafuta maarifa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Sehemu hii, itakuwezesha kuchanganua mambo kiyakinifu kwa kuhoji na kufanya ulinganifu.

## Kuhoji mambo

Tabia ya kuhoji kabla ya kutenda au kulipokea jambo ni muhimu sana. Tabia kama hii inakupa nafasi ya kuelewa zaidi na kuimarisha kile unachokitenda. Pia, inakujengea stadi ya kujitambua, kuelewa matatizo ya watu wengine na kukuza vipaji vyako. Aidha, inakuza busara na kujenga ari ya unyenyekevu pale unapopata nafasi ya kujua yale ambayo huyajui. Katika ngazi ya darasani, tabia ya kuhoji ni njia muhimu ya ujifunzaji. Huongeza maarifa, hukuza ubunifu na pia kukuza moyo wa uwajibikaji.



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 114 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Soma habari hii kwa makini, kisha ujibu maswali yanayofuata.

Yusta na Amina waliingia darasa la tano katika shule ya bweni ya Iwawa. Ghafla, kila mmoja alipata rafiki wa darasa la saba. Rafiki wa Yusta aliitwa Mage na rafiki wa Amina aliitwa Anastazia. Baada ya wiki mbili, rafiki wa Yusta alianza kumpa nguo zake amfulie. Baada ya mwezi mmoja, Yusta alikuwa akifanya shughuli zote za Mage. Maeneo yote ya usafi wa shule aliyopangiwa Mage yalihudumiwa na Yusta. Hata kipande cha shamba cha Mage kililimwa na Yusta. Lakini kwa Amina mambo yalikuwa tofauti. Anastazia alipompa Amina nguo za kufua, Amina alihoji kwa nini afue nguo za mwanafunzi mwenzake. Pia, Amina alihoji sababu za urafiki huo. Je, yeye Anastazia alikuwa na shida gani? Hivyo, Anastazia hakumpa majukumu tena. Urafiki kati ya Amina na Anastazia ukavunjika.

Baada ya miezi mitatu maendeleo ya darasani yalikuwa chini kwa Yusta na ya juu kwa Amina. Amina alimshauri Yusta aachane na Mage kabisa. Baada ya ushauri huo Yusta aliacha kufanya shughuli alizopewa na Mage. Aliona haikuwa lazima yeye kuzifanya. Alianza kuhoji uhalali wa yeye kufanya shughuli hizo. Hatimaye, urafiki kati ya Yusta na Mage ulianza kudorora. Baada ya miezi sita maendeleo yao kimasomo kwa wote wawili, Yusta na Amina yalianza kuimarika na kuwa juu kuliko hapo awali.

### Zoezi la 5

1. Ni eneo lipi la habari linaloonesha tabia ya kuhoji?
2. Ni eneo lipi la habari linaloonesha tabia ya kutokuhoji?
3. Je, tabia ya kuhoji ilikuwa na manufaa gani kwa Amina?
4. Je, tabia ya kutohoji ilisababisha madhara gani kwa Yusta?
5. Unafikiri kwa nini Yusta alishuka kimasomo?
6. Orodhesha hasara zinazotokana na tabia ya kutokuhoji mambo kabla ya kuyatekeleza.

### Kazi ya Kufanya

Orodhesha matatizo yaliyo kwenye jamii inayokuzunguka yanayotokana na tabia ya kutokuhoji mambo kabla ya kutekeleza. Andika matatizo hayo kwenye daftari lako na liwasilishe kwa mwalimu wa somo.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 115 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Madhumuni ya kuhoji katika maisha ya kila siku

Kuhoji ni hali ya kudadisi kwa kutaka kujua mambo kwa kina. Madhumuni ya kuhoji ni kupata majibu sahihi kutoka kwa mtu anayehusika ili kuondoa utata wa jambo. Tunahitaji kuhoji ili kufanya uamuzi sahihi. Kwa mfano, mwanafunzi aliyefanya kosa shuleni, huitwa na kuhojiwa na mwalimu kwa ajili ya kupata ukweli wa makosa yake. Kabla ya mtuhumiwa kuhukumiwa mahakamani, huwa anahojiwa ili kuweza kubaini ukweli wa mambo. Kuhoji kunasaidia kutatua changamoto zinazojitokeza katika maisha ya kila siku. Kwa mfano, ukianza tabia ya kuchelewa kufika nyumbani utokapo shuleni, mzazi au mlezi wako atakuhoji ili kuweza kubaini jambo linalokucheleweshа na kisha kutafuta utatuzi wa jambo hilo.

Mwalimu anaweza kutumia mbinu ya kuhoji darasani ili kupata jibu la uhakika au kufikia jibu sahihi kutoka kwa wanafunzi wake. Njia zinazoweza kutumika katika kuhoji mambo mbalimbali ni kama vile maswali na majibu kwa mdomo. Haya hutumika kuhoji pale mwalimu anapotaka kupata ukweli au kupata majibu sahihi kutoka kwa mwanafunzi muda huohuo na wakiwa wanaonana.

## Kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine

Tabia ya kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine ni jambo muhimu sana katika maisha. Kuna namna nyingi za kujifunza katika maisha yetu. Unaweza kujifunza kutokana na matendo au maisha ya watu wengine. Mfano, mwanafunzi hujifunza kutoka kwa wanafunzi wenzake, walimu, wazazi, walezi au kutoka kwa jirani au jamii. Vilevile, watu wengi hujifunza kutoka kwa watu wengine. Hivyo, kila tukio katika maisha ya watu wengine linaweza kuwa ni funzo kwako ambalo litakusaidia kuwa na uelewa mpana wa maisha.

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Chakubanga ni mwanafunzi wa darasa la tano anayetoka kwenye familia yenye kipato cha juu. Mara nyingi huja shuleni kwa gari la kifahari na hurudishwa nyumbani kwa gari hilo mara tu vipindi vinapomalizika. Rafiki yake wa karibu sana ni Julius, ambaye naye anatoka kwenye familia yenye kipato kikubwa. Yeye pia huletwa na kurudishwa shuleni na gari. Wote, Chakubanga na Julius, walijiona ni bora sana na kujitenga na wanafunzi wengine akiwemo Mohamed. Mohamed ni mwanafunzi anayetokea*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 116 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*katika familia ya mzee Lazaro mwenye kipato duni kinachotokana na kilimo katika shamba lake dogo la nyanya.*

*Siku moja, katika runinga ilitangazwa kuwa baba yake Chakubanga alikuwa anachunguzwa kwa matumizi mabaya ya fedha za umma. Baada ya muda mfupi alikamatwa na kufungwa. Mali zake zote zikataifishwa na serikali. Maisha ya Chakubanga na familia yake yakawa magumu. Baada ya mkasa huo ulioikumba familia ya Chakubanga, Julius alianza kumtenga rafiki yake Chakubanga na kumuona hana maana kwake. Siku moja Chakubanga alikosa nauli ya kwenda shule. Mohamed, alimuonea huruma Chakubanga na kumpatia kiasi kidogo cha shilingi 300 ili zimsaidie kwa nauli ya kwenda shuleni. Julius alimkazia macho Mohamed na kumwambia, "Kwa nini unampatia pesa Chakubanga!" Mohamed alijibu, "Ni vyema kusaidiana bila kujali tofauti zetu."*

**Zoezi la 6**

1. Je, umejifunza nini kutokana na urafiki wa Chakubanga na Julius?
2. Umejifunza nini kutokana na tabia ya Mohamed?
3. Je, umejifunza nini kutokana na tabia aliyokuwa nayo Chakubanga?
4. Unafikiri kwa nini Julius alimkwepa Chakubanga?
5. Umepata funzo gani kutokana na kitendo cha Mohamed cha kumsaidia Chakubanga?
6. Umejifunza nini kutokana na tendo la kufilisiwa mali na hatimaye kufungwa kwa baba yake Chakubanga?
7. Bainisha watu wenye tabia kama ya Mohamed katika jamii yako.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu namna mtakavyosaidia kubadilisha tabia za wanafunzi wenzenu wenye tabia kama za Chakubanga na Julius.

## Kutathmini utendaji wako ili kuuboresha

Kutathmini ni hali ya kuangalia jambo kwa kina, kuangalia faida na hasara zake ili kuweza kutoa uamuzi sahihi wa busara na wenye ufanisi. Hivyo,



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 117 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

utendaji bora ni matokeo ya tathmini ya kina ya namna ya kufanya jambo kwa ufanisi.

**Namna ya kufanya tathmini ya utendaji shuleni na nyumbani**

Tathmini ya utendaji shuleni hufanyika pale ambapo mwanafunzi amepewa kazi ya kufanya baada ya kujifunza ili kupima uwezo wake wa kutenda kazi hiyo. Kwa mfano, mwanafunzi anapewa kazi ya kufanya baada ya kujifunza mada au umahiri fulani. Hufanyika pia kwa kuangalia matokeo ya utendaji wake shuleni, kwa kuangalia kadi za maendeleo ya taaluma na mwenendo ili kubaini tabia ya mwanafunzi kwa ujumla ikiwemo namna anavyoshirikiana na wenzake. Tathmini hii pia itabaininisha ushiriki wake katika kazi za nje ya darasa, mfano kushiriki kwenye michezo na shughuli za elimu ya kujitegemea shuleni, ni njia nyingine zinazowezesha kumfanyia tathmini.

**Angalia picha hii, inayoonesha wanafunzi wakifanyiwa tathmini ya utendaji shuleni.**



*Kielelezo namba 1: Wanafunzi wakifanya mtihani*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tathmini ya utendaji wa mtoto akiwa nyumbani hufanyika kwa kuangalia ushiriki wake katika kazi mbalimbali za nyumbani, kama vile kuosha vyombo au kufua nguo. Tunapima endapo mtoto ana uwezo wa kutenda kazi hizo kwa ufanisi. Vilevile, mtoto anavyoshiriki katika shughuli za uzalishaji mali akiwa nyumbani, kama vile kwenda shambani, kulisha mifugo au kulima bustani za mbogamboga.

## Umuhimu wa kutathmini utendaji wa nyumbani

Utendaji wa nyumbani ni muhimu sana kutathminiwa kwa kuwa utasaidia katika ustawi wa familia kama vile kumrekebisha mtoto na kumjengea tabia ya kujitegemea. Utendaji wa nyumbani ukitathminiwa humjengea pia mtoto udadisi kwani huweza kuhoji na kutafuta majibu ya changamoto zinazojitokeza katika familia. Humjengea mtoto ujasiri na uwezo wa kujiamini katika kufanya mambo yanayoleta maendeleo. Vilevile, utendaji bora nyumbani huakisiwa katika utendaji shuleni. Taarifa hizi husaidia wakati mwalimu na wazazi au walezi wanapokutana kwa lengo la kujadili tabia ya mwanafunzi ili kuinua utendaji wake shuleni na nyumbani.

### Zoezi la 7

1. Eleza namna tathmini inavyofanyika katika shule yako.
2. Njia zipi wazazi au walezi wako wanazitumia kufanya tathmini ya utendaji wako nyumbani?
3. Tathmini inasaidiaje kuboresha utendaji shuleni na nyumbani?
4. Je, ni madhara gani yanaweza kutokea kama tathmini za utendaji nyumbani na shuleni hazikufanyika?

### Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wenzako namna tathmini ya utendaji wenu inavyofanyika hapo shuleni. Andika tathmini hizo kwenye daftari, kisha liwasilishe kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 119 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

Oanisha maneno ya **sehemu A** na yale ya **sehemu B** ili kupata maana sahihi, kisha andika herufi ya jibu sahihi.

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Malengo | A. hali ya kuwa sawa au uwiano |
| 2. Utekelezaji wa malengo | B. uliza mtu maswali ili kupata ukweli wa mambo |
| 3. Kufanya jambo kiyakinifu | C. kazi kufanyika katika muda uliopangwa |
| 4. Njia ya kuhoji | D. tathmini ya utendaji shuleni |
| 5. Ulinganifu | E. namna ya kuangalia matokeo shuleni |
| 6. Matokeo ya mtihani | F. tabia ya kuhoji au kudadisi |
| 7. Uchapakazi wa shughuli za nyumbani | G. matarajio katika kufanya jambo |
| 8. Kufanya tathmini | H. tathmini ya utekelezaji |
| | I. tathmini ya utendaji nyumbani |
| | J. kuamua mambo kwa haki kutokana na ushahidi |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Kipato | mavuno au fedha anazopata mtu kutokana na kazi aliyoifanya au faida ya mauzo ya kitu. |
| Kipaumbele | jambo muhimu kuanza kutekelezwa |
| Kudorora | hali inayopunguza ukamilifu wa kitu |
| Morali | ari ya kufanya jambo kwa moyo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| Mpango kazi | utaratibu wa kufanya kazi kwa hatua ili kufikia lengo lililokusudiwa |
| Mtazamo chanya | mawazo au fikra za matumaini alizonazo mtu kuhusu suala fulani dhidi ya ukataji tamaa |
| Tathmini | kuangalia kitu kwa undani kisha kukadiria thamani yake au ubora wake |
| Unyenyekevu | hali ya kutambua uwezo na upungufu wako na kukubali kujifunza kutoka kwa watu wengine |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Kuwa mwadilifu

Katika sura ya tisa ulijifunza namna ya kufikia malengo. Katika sura hii, utajifunza dhana ya maadili, uadilifu, matendo ya uadilifu na namna ya kuwa mwadilifu. Je, maadili ni nini? Maadili ni mwenendo au utendaji unaokubalika katika jamii fulani. Pia, ni mfumo wa maisha unaokubalika katika jamii husika. Wakati mwingine maelekezo yanayotolewa ili kujenga tabia na mwenendo wa mtu au kikundi cha watu katika kazi au maisha pia huitwa maadili.

Je, uadilifu ni nini? Je, umewahi kutakiwa kuwa mwadilifu? Uadilifu ni kitendo cha mtu au jamii ya watu kutenda haki bila ya upendeleo kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa. Kwa kifupi, tunaweza kusema kuwa uadilifu ni kufanya matendo yaliyo mema na yanayokubalika katika jamii. Baadhi ya matendo hayo ni uaminifu katika jamii, kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia uwazi na ukweli na kusimamia haki.

### Kutumia mitandao kwa kufuata maadili ya Watanzania

Mtandao ni mfumo wa mawasiliano ya kiteknolojia unaotumiwa na watu kutafuta na kupeana taarifa kupitia vifaa mbalimbali kama vile simu na kompyuta. Taarifa, zipatikanazo kwenye mtandao hujenga fikra na mitazamo ya watu kuhusu mambo mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni. Taarifa hizo huweza pia kuathiri mitazamo ya kimaadili ya mtu au watu wa jamii husika kwa kuwaimarisha au kuwabomoa.

Kutokana na ongezeko la kasi la matumizi ya mitandao katika mawasiliano duniani, kunakuwa na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali. Taarifa nyingi zinazotumwa katika mitandao hiyo hubeba maudhui mbalimbali yanayofaa na yasiyofaa. Kwa hiyo, panahitajika utaratibu wa kuzichuja taarifa hizo ili kutenganisha taarifa zinazofaa na zisizofaa, zile zinazoendana na maadili ya watu husika na zisizoendana na maadili ya watu hao. Hivyo, ni muhimu kuzisoma na kuzichambua taarifa za mtandaoni kwa makini.

Mitandao huweza kutumika kwa kutupatia habari, kutuelimisha na kutuunganisha na wenzetu kote duniani. Lakini inaweza pia kuharibu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tamaduni za watu husika na kuwaingiza kwenye vitendo viovu kwa kupeana taarifa ambazo hazina uadilifu. Matumizi bora ya mitandao hulinda utu na heshima ya kila mwanajamii. Huepusha migogoro inayoweza kusababishwa na matumizi mabaya ya mtandao. Pia, husaidia jamii kupata manufaa ya kielimu na namna ya kuboresha utendaji wa shughuli za kila siku pamoja na kufahamu mambo yanayotokea ulimwenguni kwa wakati. Kwa mfano, kupitia mitandao watu wanaweza kujifunza mbinu bora za kilimo, uvuvi na ufugaji wa kisasa, ujasiriamali, ujenzi na hata mapishi. Hali kadhalika, jamii inaweza kujifunza tamaduni tofauti za jamii nyingine zinazofaa kuigwa.

**Soma kwa makini majibizano yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mama:** Christina mwanangu, unafanya nini?

**Christina:** Ninasoma mama.

**Mama:** Unasomaje hapa daftari na hapo simu!

**Christina:** Ninatumia simu kutafuta maarifa mengine halafu ninaandika daftarini.

**Mama:** Sawa mwanangu, lakini uwe makini. Usitumie simu kuangalia mambo yasiyofaa kama vile picha za ngono, majambazi, wizi na mauaji.

**Christina:** Ninazingatia hilo mama. Mwalimu wetu ametuelimisha namna ya kutumia mitandao na ametuasa kuwa makini na kuzingatia mambo yenye manufaa. Najua kuwa kwenye mitandao kuna mambo mengi mazuri na mengi mabaya, yasiyo na maadili.

**Mama:** Ni kweli mwanangu. Nimefurahi umetambua kwamba mitandaoni kuna mambo mazuri na yenye manufaa na pia yapo mambo mengi mabaya yasiyofaa. Kwa hiyo unapaswa kuwa mwangalifu na kuzingatia maelekezo uliyopewa na mwalimu wako.

**Christina:** Asante mama, nitazingatia yote.

**Mama:** Haya mwanangu masomo mema.

**Christina:** Asante mama.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Christina alikutwa na mama yake akifanya nini?
2. Mwalimu alimpa ushauri gani Christina kuhusu matumizi ya mitandao?
3. Mama yake Christina alimshauri nini mwanawe?
4. Ni mambo gani yenye faida huwa unayapata kwenye mitandao?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na rafiki zako katika kikundi kuhusu namna bora ya kutumia mitandao ya kijamii. Andika kwenye daftari lako namna mtakavyowashauri wanafunzi wenzenu wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Kuzingatia sheria na makubaliano

Je, umewahi kuambiwa "Fuata sheria?" ulipoambiwa hivyo ulielewa nini? Sheria inaweza kutafsiriwa kama ni kanuni zinazoongoza taratibu za uamuzi na utendaji wa jambo. Kila jamii ina taratibu ilizojiwekea ambazo zinatakiwa kufuatwa na kila mwanajamii kuanzia katika ngazi ya familia hadi kwenye ngazi ya taifa. Sheria, kama taratibu, zimewekwa ili kuhakikisha kuwa jamii zinaishi kwa amani, utulivu, furaha na maelewano. Vilevile, zinatumika kudhibiti usalama wa watu na mali zao. Athari za kutozingatia sheria ni kuishi maisha yasiyo na utaratibu. Hivyo kila mwanajamii anapaswa kuishi kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Makubaliano ni nguzo muhimu ya uzingatiaji wa sheria. Makubaliano ni maridhiano baina ya pande mbili katika kutekeleza jambo fulani. Makubaliano hayo yanaweza kuwa ya maandishi, ya mdomo au mkataba wa kisheria. Uzingatiaji wa makubaliano ni alama kubwa sana ya uadilifu na husaidia kuepusha migogoro katika jamii.

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Ali na Remi ni wanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Kibaya. Walipenda sana kutumia muda wao mwingi kucheza mpira wa miguu. Ingawa walikatazwa kucheza mpira karibu na madarasa na ofisi za shule,*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 124 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*wao hawakutii. Siku moja, wanafunzi wenzao waliporudi darasani kutoka mapumziko ya saa 4:00 asubuhi, wao walikuwa bado wanaendelea kucheza mpira karibu na madarasa na ofisi za shule. Remi alipiga mpira kwa nguvu ukagonga dirisha la ofisi ya mwalimu mkuu na hatimaye kuvunja kioo na kuingia ndani ya ofisi. Mwalimu mkuu alikasirika sana na kuwaamuru Ali na Remi kwenda kuwaita wazazi wao. Wazazi walipofika shuleni, mwalimu mkuu aliwaonesha uharibifu uliofanywa na walitakiwa kulipa gharama za matengenezo. Wazazi walikubali kulipa gharama. Ali na Remi walipewa adhabu mbele ya wenzao ya kupanda miti miwili kila mmoja na kuimwagilia maji hadi ikue. Huo ukawa mwanzo wa Ali na Remi kuzingatia taratibu na makubaliano yote shuleni.*

**Zoezi la 2**

1. Je, matendo ya Ali na Remi yameleta tatizo gani shuleni?
2. Orodhesha matendo utakayoanza kufanya kuanzia sasa ili kuimarisha uwezo wako wa kufanya uamuzi kwa kuzingatia sheria.
3. Ni makubaliano yapi ulishawahi kuyafanya na ukayatekeleza katika maisha yako?
4. Ni hasara zipi unazoweza kupata usipotekeleza makubaliano?

**Kazi ya Kufanya**

Andika kisa kinachoonesha kwamba uliwahi kuadhibiwa na mwalimu wako shuleni au mzazi/mlezi wako nyumbani, kisha wasilisha daftari kwa mwalimu wa somo.

## Kutekeleza maagizo na maelekezo

Katika sehemu hii utajifunza namna ya kuzingatia maagizo na maelekezo unayopewa unapokuwa shuleni na nyumbani. Kwani uadilifu hupimwa kwa kuangalia namna unavyotekeleza maagizo na maelezo unayopewa. Hivyo, ni muhimu kuzingatia maagizo yote mazuri unayopata ili kudumisha maelewano, amani na furaha.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 125 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma ngonjera hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Hodi hodi naingia, uwanjani kujitosa,
Kuna jambo lasumbua, wakubwa hata wadogo,
Ni nini kimetupata, na hasa sisi vijana?
Kutii maelekezo, tatizo kwetu vijana.

2. Asha pamoja na John, ubishi mwaendekeza,
Wazazi waagizapo, kiburi mwaendekeza,
Na shuleni mtumwapo, wazito kutekeleza,
Kutii maelekezo, tatizo kwetu vijana.

3. Tatizo ota mizizi, yatubidi tulipinge,
Tena tuelimishane, makini pasi pingana,
Maelekezo pokea, kufanya kwa ufanisi,
Kutii maelekezo, tatizo kwetu vijana.

4. Uwanjani naondoka, naomba nisikilizwe,
Wajibu wetu vijana, kuyatii maagizo,
Kwa walimu na wazazi, pia na jamii nzima,
Muhimu kuzingatia, maagizo tupewayo.

**Zoezi la 3**

1. Ni tatizo gani linawapata vijana katika kipindi hiki?
2. Njia gani zitumike kutatua tatizo hili?
3. Tatizo hili limeota mizizi katika mazingira gani?
4. Orodhesha matendo utakayofanya kuwarekebisha wenzako wasiozingatia maelekezo ya walimu na wazazi au walezi wao.
5. Orodhesha matatizo uliyowahi kushuhudia nyumbani na shuleni yaliyosababishwa na kutofuata maelekezo.
6. Taja vitendo utakavyofanya ili kuimarisha uwezo wako wa kuzingatia maelekezo ya walimu, wazazi au walezi wako.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 126 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadili na wenzako darasani kubaini vitendo vya wanafunzi wasiotii maagizo na maelekezo kisha ainisha ushauri utakaotoa kuwaelekeza umuhimu wa kutii maagizo na maelekezo. Andika kwenye daftari lako ushauri huo kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kutunza mali unayokabidhiwa

Kutunza ni kuweka kitu chini ya uangalizi mzuri ili kisiharibike, kisidhurike au kupotea. Kwa hiyo utunzaji wa mali ni uwekaji wa mali chini ya uangalizi mzuri ili isiharibike au kupotea. Utunzaji mali, ni tabia mojawapo nzuri sana ya uadilifu. Katika mazingira yako kama mwanafunzi una jukumu kubwa la kutunza mali za nyumbani na shuleni. Mali hizo ni kama vile madawati, vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia, vyombo vya nyumbani, vifaa vya usafi na vingine vyote utakavyokabidhiwa. Ni wajibu wako kama raia mwema na mwadilifu kulinda na kutunza mali ulizokabidhiwa kwa kuweka kumbukumbu ya mali hizo. Pia, kutunza mali ni pamoja na kutumia madawati kwa umakini bila kuyachorachora au kuyavunja kwa makusudi. Hali kadhalika, kujaladia madaftari na vitabu kwa majalada ni jambo linaloonesha utunzaji wa vitu. Vilevile, kutumia vyombo kwa uangalifu wakati wa chakula na kuvisafisha kwa makini ni alama ya utunzaji. Aidha, unawajibika kutunza mfuko au begi unalobebea madaftari, sare za shule na viatu vya shule ulivyonunuliwa na wazazi au walezi wako.

**Tafakari matendo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

(i) Ampokile amepongezwa kwa utunzaji bora wa mali za shule.

(ii) Mwasifa ameadhibiwa kwa kutotunza mali za shule.

(iii) Mdeka ameamuriwa kulipa jembe alilopoteza.

(iv) Ishimwe amekuwa akivunja vikombe na sahani za udongo za nyumbani.

(v) Sarafina amekuwa akivunja jiko la udongo kila mara na sasa anapikia jiko la kuni linaloeneza moshi mwingi ambao umesababisha macho yake kuwa mekundu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 127 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. Wewe unafanana na nani kwa tabia kati ya hawa waliotajwa hapo juu?
2. Una mpango gani wa kujirekebisha?
3. Eleza hasara za kutolinda na kutunza mali tunazokabidhiwa shuleni au nyumbani.
4. Taja faida za kutunza mali ulizokabidhiwa shuleni au nyumbani.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu namna mtakavyotunza mali mtakazokabidhiwa shuleni au nyumbani. Andika mikakati hiyo kwenye daftari lako kisha uliwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Mipango ya utekelezaji wa majukumu shuleni na nyumbani

Ni muhimu kutambua kuwa moja ya siri za mafanikio ya mtu au kikundi cha watu ni kuwa na mpango wa utekelezaji. Ili ufanikiwe katika majukumu ya shuleni na nyumbani huna budi kuainisha shughuli zote na kujiwekea ratiba ya kila siku na kuitekeleza ipasavyo. Pia, inakupasa kujiwekea malengo ya utekelezaji wa shughuli hizo na kutathmini utekelezaji wa malengo hayo kwa kuzingatia taratibu za shule na za nyumbani. Vilevile, unatakiwa kukemea na kutoa taarifa juu ya tabia zote zisizofaa na ushirikiane na wenzako kutoa msaada kwa wanafunzi au wanafamilia.

**Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mwandishi:** Habari gani?

**Yusto:** Nzuri, shikamoo.

**Mwandishi:** Marahaba. Hebu jitambulishe.

**Yusto:** Mimi naitwa Yusto, nasoma darasa la tano, Shule ya Msingi Mkongotema.

**Mwandishi:** Hongera sana Yusto kwa kupata ushindi wa mwandishi bora chipukizi wa mashairi nchini.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 128 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Yusto:** Asante sana, mwandishi.

**Mwandishi:** Unajisikiaje kwa ushindi huo?

**Yusto:** Ninajisikia vizuri sana kwa sababu ndoto yangu imetimia.

**Mwandishi:** Kumbe ulikuwa na ndoto? Hebu tueleze, ni ndoto gani hiyo?

**Yusto:** Mwalimu wetu wa somo la Kiswahili alipotufundisha ushairi alituhamasisha tujitahidi kuandika mashairi mazuri hadi tuwe mahiri kama Mathias Mnyampala.

**Mwandishi:** Ehee! Halafu ulichukua hatua gani?

**Yusto:** Kwanza alinihamasisha kupenda kusoma mashairi waliyoandika wengine vitabuni na magazetini.

**Mwandishi:** Kumbe! Na wewe uliwahi kuandika shairi lolote ukalipeleka gazetini?

**Yusto:** Ndiyo, nimewahi, tena mara nyingi tu. Kwa mfano, angalia hili hapa (*anamuonesha gazeti lenye shairi aliloandika*) na yapo mengine mengi.

**Mwandishi:** Kuna msaada wowote uliopata wa kusomewa kazi yako kabla ya kuipeleka gazetini?

**Yusto:** Kuna rafiki zangu niliokuwa ninashirikiana nao. Nikiwapa wanasoma kisha ninampelekea mwalimu kabla ya kupeleka gazetini.

**Mwandishi:** Hongera sana, wewe ni mwanafunzi makini mwenye malengo na mipango mizuri.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 5

1. Yusto alikuwa na ndoto gani?
2. Yusto alichukua hatua gani ili kuifikia ndoto yake?
3. Wewe una ndoto gani katika maisha yako?
4. Umepanga mikakati gani ili kukamilisha ndoto yako?
5. Ni watu gani wanaweza kukusaidia kukamilisha ndoto yako?



URAIA NA MAADILI STD V .indd 129 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu namna mtakavyotekeleza majukumu yenu ya nyumbani na shuleni kwa ufanisi. Andika kwenye daftari lako jinsi mtakavyotekeleza hayo majukumu kisha uwasilishe daftari kwa mwalimu wa somo.

## Matendo yasiyotiliwa shaka

Je, umewahi kutilia shaka jambo lolote lile? Kwa nini? Yumkini kuna sababu fulani ambayo ilikufanya utie shaka. Kutilia shaka jambo kunaweza kuwa na maana ya kuwa na wasiwasi juu ya ukweli, usahihi au uhalali wa jambo hilo. Kwa upande mwingine, matendo yasiyotiliwa shaka ni yale ambayo hayatoi wasiwasi juu ya ukweli wake, usahihi wake au uhalali wake. Utendaji wa matendo yasiyotiliwa shaka ni sehemu muhimu ya uadilifu. Uadilifu wa aina hii huvuta uaminifu na hali ya kukubalika katika jamii. Haya matendo huweza kutendwa shuleni au nyumbani. Baadhi ya matendo yanayotiliwa shaka kwa mwanafunzi ni usiri na ukimya uliopitiliza, muonekano tofauti wa baadhi ya viungo vya mwili wake kama vile macho kuwa mekundu kupita kiasi au kutembea huku akipepesuka. Matendo mengine ni kusinzia mara kwa mara darasani, kulia, kushindwa kabisa kujisomea, kuonekana akitokea kichochoroni, akiwa na pesa nyingi au akiwa na vitu vya thamani kubwa. Matendo yasiyotiliwa mashaka kwa mwanafunzi ambayo hutendwa shuleni na nyumbani ni kama vile kuwa mchangamfu na kushiriki vyema kazi za nyumbani na shuleni.

Matendo mengine ni uwazi ukiwa shuleni hata nyumbani kwa kueleza shida au matatizo yanayokukabili.

Unaposhirikiana na wenzako vizuri ukiwa shuleni na nyumbani katika michezo, unadhihirisha hali ya kutokuwa na tatizo. Kuwahi shuleni na kuwahi kurudi nyumbani ni matendo yasiyotiliwa shaka shuleni na nyumbani. Kulala mapema, kuwahi kuamka na kujiandaa vyema kwenda shuleni, humfanya mzazi au mlezi asiwe na shaka na wewe. Sasa, namna gani unaweza kuepuka matendo yanayotiliwa shaka?

Namna bora ya kuepuka matendo yanayotiliwa shaka shuleni na nyumbani ni kuwa na ushirikiano mzuri na wazazi, walezi, walimu na wanafunzi wenzako. Pia, unatakiwa uwatambulishe rafiki zako kwa wazazi au walezi wako, uwe makini katika masomo na kuwa msikivu.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 130 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 6**

1. Kwa nini ni muhimu kuchagua marafiki wenye tabia inayofaa?
2. Ni matendo gani yasiyotiliwa shaka uliyoyasoma katika habari hii?
3. Eleza namna utakavyomsaidia mwanafunzi mwenzako mwenye matendo yanayotiliwa shaka shuleni kwenu.

**Kazi ya Kufanya**

Chunguza matendo yanayofanyika shuleni na kisha bainisha matendo yale unayoyatilia shaka. Andika matendo uliyobaini katika daftari lako na uwasilishe daftari kwa mwalimu wa somo.

## Kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia uwazi na ukweli

Bila shaka umewahi kumsikia rafiki yako akisema "Wewe ni mwongo, sema ukweli." Na wakati mwingine umewahi kusikia watu wakisema, "Uwe muwazi." Uwazi na ukweli ni miongoni mwa nguzo muhimu sana za kuonesha uadilifu.

Uwazi ni hali au tabia ya kuzungumza kwa uhuru bila kuficha kitu. Ni dhana inayoakisi uhuru wa kutoa mawazo yanayokubalika bila kuvunja sheria. Uwazi pia ni dhana inayoashiria mipango au sera zinazoeleweka, zinazokubalika na kutengenezwa na watu wenyewe. Vilevile, uwazi ni hali au tabia ya kutenda matendo yanayokubalika na jamii bila kificho.

Je, unajisikiaje mtu anapokuambia ukweli? Unamwonaje yule ambaye hakuambii ukweli? Ni faida gani umewahi kuzipata kwa kuambiwa na kusema ukweli? Ukweli katika maisha ya kila siku una faida kubwa sana. Pamoja na faida zote zile ambazo unaweza kuzifikiria, bila shaka hazitatofautiana sana na hizi zifuatazo: ukweli unakupa nguvu na uhalali wa kukemea matendo maovu katika jamii. Mtu mkweli huvuta usikivu na uaminifu na huwa na uwezo mkubwa wa kukosoa na kukemea matendo maovu shuleni na katika jamii kwa ujumla. Baadhi ya vitendo visivyofaa shuleni ni uchochezi, kuongea uongo na kutokuwa muwazi. Hebu fikiri ni kwa kiasi gani kauli ya rafiki yako ambaye anasema ukweli ilikuwa



URAIA NA MAADILI STD V .indd 131 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na athari tofauti katika maisha yako kuliko ile kauli ya kukemea maovu iliyotoka kwa mtu mwongo.

Mtu anayesema ukweli mara zote huaminika kwa sababu hutoa taarifa kwa kutumia vyanzo vya kuaminika au vitu alivyoshuhudia. Taarifa itokayo kwa mtu mkweli na mwaminifu huwa na nguvu ya kufuatwa. Kwa mfano, taarifa itokayo kwa mzazi, mlezi au mwalimu anayeaminika huwa na nguvu au msukumo wa utekelezaji. Hali kadhalika, taarifa itokayo kwenye vyombo vya habari vinavyoaminika hupendwa na kuaminika na wengi. Taarifa hizo zinaweza kutoka kwenye radio, magazeti, runinga na mitandao ya kijamii. Mara nyingi taarifa ambazo haziaminiki hutoka katika mazungumzo ya mitaani. Hizi ni taarifa ambazo huwa hazijafanyiwa uchunguzi na mara nyingi ni taarifa ambazo hutoka kwa watu wasioaminiwa.

**Zoezi la 7**

1. Eleza faida ambazo unaweza kuzipata kwa kusema ukweli na kwa uwazi hapo shuleni kwako.
2. Utamsaidiaje mwenzako ambaye siyo mkweli?
3. Madhara gani ambayo umewahi kuyapata kwa kusema ukweli?

**Kazi ya Kufanya**

Jadilianeni katika vikundi namna mtakavyowasaidia wenzenu ambao sio wakweli hapo darasani kwenu. Andika mikakati mliyoweka katika daftari lako kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Athari za uongo katika maisha ya kila siku

Je, uliwahi kusema uongo? Je, kuwa mwongo ni sifa nzuri? Je, umekwisha kufikiria athari za kusema uongo? Uongo ni tabia ya kupotosha ukweli au uhalisia wa jambo, tukio au tendo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 132 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*Kaboga na Kajembe walikuwa marafiki na wote walisoma darasa moja. Marafiki hao walikuwa wachezaji mpira hodari, lakini walitofautiana katika uwezo wao wa kimasomo. Kajembe alikuwa anaongoza darasani kila muhula, lakini Kaboga alishika namba ya mwisho. Kaboga alimwonea wivu Kajembe na akaamua kufanya njama za kumharibia sifa ili afukuzwe shule.*

*Wakati wanafunzi wakiwa madarasani, Kaboga aliomba ruhusa kwenda kujisaidia. Badala ya kwenda chooni alikwenda bwenini. Akiwa bwenini akavunja sanduku la mwanafunzi mwingine aliyeitwa Kanene. Akachukua shati zuri la Kanene na kulificha chini ya godoro la kitanda cha Kajembe. Kanene alipogundua wizi uliofanyika alitoa taarifa kwa mwalimu wa zamu. Upekuzi ulipofanyika shati lilikutwa chini ya godoro la kitanda cha Kajembe. Kajembe alipohojiwa alikana kuhusika na wizi huo. Hata hivyo, kukataa kwake hakukumsaidia. Hatimaye, Kanene alikuta kitambulisho cha Kaboga kwenye sanduku lake lililovunjwa.*

*Kanene alipotoa taarifa kwa mwalimu kuhusu suala hilo, ikadhihirika wazi kuwa Kaboga ndiye aliyefanya uhalifu. Bila kutarajia, Kaboga akachukuliwa hatua kali za kinidhamu.*

**Zoezi la 8**

1. Unafikiri nini itakuwa hatima ya urafiki kati ya Kaboga na Kajembe?
2. Ni hatari gani ingemkabili Kajembe kama kitambulisho cha Kaboga kisingeonekana ndani ya sanduku la Kanene?
3. Licha ya uongo, Kaboga alikuwa na tabia gani nyingine mbaya?
4. Toa ushauri kwa wanafunzi wenye tabia za wivu na uongo kama tabia ya Kaboga.

**Kazi ya Kufanya**

Andika ngonjera beti mbili kuwaonya wanafunzi waongo na wenye wivu. Kisha, wasilisha kwa mwalimu wako wa somo.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 133 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Athari za tabia ya unafiki

Unafiki ni nini? Watu wanafiki wana tabia gani? Unafiki ni hali ya kusema uongo au kutoonesha uhalisia wa ukweli katika jambo fulani. Hii ni hali ya kuficha tabia yako halisi ambayo ni mbaya kwa lengo la kunufaika. Tabia ya unafiki ina athari mbaya kwako na kwa wenzako pia.

**Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Kasenene:** Haloo Kadege! Hujambo?

**Kadege:** Sijambo rafiki yangu!

**Kasenene:** Unatambua kuwa wewe ni rafiki yangu? Sina rafiki ninayemwamini kama wewe.

**Kadege:** Kweli Kasenene mimi si rafiki tu bali ni ndugu yako.

**Kasenene:** Leo nataka nikushirikishe kitu changu ili unisaidie.

**Kadege:** Haina shida, nieleze tu, nitakusaidia na sitakusaliti ndugu yangu.

**Kasenene:** Ee bwana ee! Leo nimefanikiwa kumpora mzee mmoja kiasi cha shilingi thelathini elfu. Naomba unitunzie kwa sababu ninahisi yule bwana atakuja tu kushtaki hapa shuleni.

**Kadege:** Hilo tu ondoa shaka, lete hizo fedha nikutunzie na nitakupa pindi utakapozihitaji.

**Mwalimu wa zamu:** (*Wanafunzi wakiwa mstarini*) Kati yenu ninyi wanafunzi kuna mmoja alimpora mzee huyu hapa fedha zake. Simameni kwenye mstari na mzee atapita kuangalia sura ya kila mmoja ili kumbaini mwizi. Asiondoke hata mmoja.

**Mzee:** (*Anapita kila mstari na alipomfikia Kasenene akasema*) “Ni huyu hapa aliyenipora fedha zangu”.

**Mwalimu wa zamu:** (*Wakiwa ofisini na mzee na Kasenene*). Kasenene, hebu rudisha fedha za Mzee huyu.

**Kasenene:** Mimi nakiri nilimpora mzee huyu kiasi cha shilingi elfu thelathini, lakini nilimpa zote rafiki yangu Kadege anihifadhie.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 134 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwalimu wa zamu:** (*Anaamuru Kadege aitwe*) Kadege, wewe umehifadhi fedha za wizi!

**Kadege:** Hapana mwalimu, mimi sijawahi kupokea fedha kwa Kasenene. Kasenene hajawahi kuwa rafiki yangu hata siku moja. Mimi sishirikiani na wezi.

**Mwalimu Mkuu:** (*Wakiwa kwenye ofisi ya Mwalimu Mkuu*) Kasenene, wewe umeonesha tabia mbaya sana na umeharibu sifa nzuri ya shule. Unasimamishwa shule kuanzia leo. Jumatatu ijayo uwalete wazazi wako wakiwa na fedha ya kulipa.

**Zoezi la 9**

1. Ni nani katika wahusika hawa ameonesha tabia ya unafiki?
2. Je, Kadege alifanya uamuzi sahihi kupokea fedha za wizi?
3. Kama Kadege angekuwa rafiki wa kweli angepaswa kufanya nini?
4. Ungetoa ushauri gani kwa Kasenene na Kadege?
5. Taja tabia nyingine zinazokuudhi shuleni kwako mbali na hizi ulizozibainisha katika kisa ulichokisoma.

**Kazi ya Kufanya**

Andika katika daftari lako hasara anazoweza kupata mtu mwenye tabia za unafiki, kisha wasilisha kazi yako kwa mwalimu wa somo.

## Kusimamia haki

Je, umewahi kulalamika kuwa hujatendewa haki? Je, umewahi kuambiwa na mtu utende haki? Kutenda haki ni kumpa mtu kile anachostahili kupewa. Kwa mfano, mtoto anastahili kupewa elimu, ulinzi, matibabu, lishe, malazi na kusikilizwa.

Jamii ambayo haitendi haki haina moyo wa kuheshimu hisia za wengine wala kujali yale ambayo yana manufaa kwa wengine. Huwa imejawa na ubinafsi pamoja na dhuluma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutetea haki zako na za wengine bila ubaguzi

Kwa ujumla, haki inaweza kutafsiriwa kuwa ni ile hali ya kumtendea mwingine kile ambacho anapaswa kutendewa kwa mujibu wa sheria. Hizi ni zile stahili zinazomfanya binadamu aishi kama binadamu au aweze kutekeleza majukumu yake kama binadamu. Kwa mfano, wewe kama mwanafunzi una haki ya kupata elimu, haki ya kulindwa, haki ya kutoa mawazo, haki ya kushirikishwa, haki ya kuishi, haki ya kutobaguliwa na haki ya kusikilizwa. Haki hizi anastahili kila mtoto japo kuna baadhi ya watoto wenzako ambao hawazipati haki zao. Hivyo unatakiwa pia kuwatetea ili nao wapate haki zao stahiki.

Ikumbukwe kuwa haki huenda pamoja na wajibu na kila penye haki kuna wajibu. Kwa hiyo, kwa kila haki unayoistahili unao wajibu wa kutimiza. Kwa mfano, kama unayo haki ya kupata elimu, unao wajibu wa kusoma kwa juhudi na maarifa. Kwa kuwa sheria za shule hulenga kulinda haki ya kila mwanafunzi, unao pia wajibu wa kutii sheria za shule na kutunza vifaa vya shule. Kwa upande mwingine, kwa kuwa unayo haki ya kusikilizwa, wazazi, walezi, walimu na watu wengine wana wajibu wa kukusikiliza. Nawe pia, unao wajibu wa kuwasikiliza wengine.

## Kutoa taarifa ya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa mamlaka husika

Kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki za binadamu kwa mamlaka husika ni jambo la msingi sana katika kuhakikisha haki inatendeka. Ili kufanikisha hilo inakupasa kuwa na ushahidi wa kutosha kwa kutunza kumbukumbu ya matukio kwa kuyaandika au kuyarekodi yale yote ambayo ni ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Pia, kuwa na vielelezo vya ukiukwaji wa haki za binadamu ili vitumike kama ushahidi.

**Zoezi la 10**

1 Eleza namna utakavyoshiriki kutetea haki zako na za wengine shuleni.

2. Orodhesha haki ambazo ungependa wazazi, walezi na walimu wako wazipe kipaumbele.

3. Wewe una wajibu upi kwa kila haki uliyoitaja katika swali la 2?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu haki za msingi zinazokiukwa hapo shuleni kwenu. Andika mikakati mtakayotumia kudai haki hizo kisha uwasilishe daftari lako kwa mwalimu wa somo.

**Zoezi la 11**

**Sehemu A**

Jibu **Kweli** au **Si Kweli** katika sentensi hizi.

1. Taarifa zote za mitandaoni zinazingatia maadili. ________
2. Ukitumia vizuri mitandao unaweza kujenga ujuzi na maarifa. ________
3. Ukitumia vibaya mitandao unaweza kushtakiwa kwa mujibu wa sheria. ________
4. Sheria ni kanuni au utaratibu uliotungwa na chombo chenye mamlaka ili kutosimamia taratibu za mahali fulani. ________

**Sehemu B**

**Andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku.**

5. Kanuni zinazowekwa shuleni na nyumbani husaidia nini?
   (a) kufuata utaratibu na kudhibiti nidhamu
   (b) ukiukwaji wa haki za mtoto
   (c) ubabe wa wazazi au walezi
   (d) kuleta fujo

6. Lipi kati ya haya yaliyoorodheshwa ni tendo la kutetea haki zako na za watoto wenzako:
   (a) kukosekana utawala bora
   (b) kutii sheria na kutozitumia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) kusaidia kutoa taarifa kwenye mamlaka zinazohusika

(d) kulia kwa uchungu

7. Ipi kati ya tabia zilizoorodheshwa inaonesha uvunjifu wa sheria za shule?

(a) kuwahi sana shuleni

(b) kusoma kwa bidii

(c) utoro na kupigana

(d) kujisomea nyumbani baada ya masomo.

8. Unafiki ni nini?

(a) hali ya ukweli na uwazi

(b) kujenga hali ya uwajibikaji

(c) uongo na uzembe

(d) kujifanya rafiki wakati ni adui

9. Yafuatayo ni madhara ya kutokuwa muwazi:

(a) kusifiwa na kuharibu

(b) kuleta migongano

(c) uzembe na uhalifu

(d) mshikamano na uvivu

10. Kipi kati ya vifuatavyo ni chombo cha kisheria kinachohusika na kusimamia haki?

(a) polisi

(b) bunge

(c) shule

(d) mahakama

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

11. Ipi kati ya zifuatazo ni sababu za ongezeko la matendo ya ukiukwaji wa haki za binadamu?

(a) kulipa kodi stahiki

(b) watoto kutopelekwa shule za bweni

(c) watu kujichukulia sheria mkononi

(d) upendo kwa watu wenye mahitaji maalumu

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Teknolojia | maarifa ya sayansi yaliyowekwa katika matumizi |
| Mnafiki | mtu anayefanya mambo kinyume na anavyosema au anavyoahidi |
| Uwazi | hali au tabia ya kuzungumza bila kificho |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 139 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Demokrasia

Katika sura hii, utajifunza umuhimu wa demokrasia katika ustawi wa jamii, kazi za vyama vya siasa, umuhimu wa uvumilivu wa kisiasa na kutambua katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### Dhana ya demokrasia

Demokrasia ni aina ya utawala ambao unatokana na watu na kwa ajili ya watu. Ni mfumo wa kukubali uamuzi wa watu wengi katika kuongoza serikali kwa manufaa ya watu wote. Hata hivyo, watu wanaoongelewa katika demokrasia ni wale ambao wanakidhi matakwa ya kisheria, kwa mfano watu wenye umri wa miaka 18 au zaidi. Ikumbukwe kuwa watoto wadogo chini ya miaka 18 hawana haki ya kisheria ya kupiga kura. Makundi mengine yasiyo na haki ya kupiga kura ni wafungwa na watu wasio na akili timamu. Hawa hawaruhusiwi kisheria kushiriki katika shughuli za kupiga kura.

### Umuhimu wa demokrasia katika ustawi wa jamii

Demokrasia ni mfumo wenye manufaa lukuki katika ustawi wa jamii. Faida ya kwanza ni kwamba demokrasia imejengwa chini ya msingi wa haki za binadamu. Miongoni mwa misingi au nguzo ya demokrasia ni *ukweli na uwazi.* Utawala wa kidemokrasia hupanga mipango yake kwa uwazi na ukweli kwa kuwashirikisha wananchi kuhusu shughuli zinazofanyika. Msingi wa pili wa demokrasia ni *kutii na kuheshimu sheria.* Utawala wa kidemokrasia hutambulika kwa utii wa sheria za nchi. Wananchi na viongozi wao wana haki sawa chini ya sheria. Anayevunja sheria anapaswa kupelekwa mbele ya vyombo vya sheria, yaani mahakamani. Utawala wa kidemokrasia hauruhusu wananchi au mtu yeyote kuchukua sheria mkononi. Mathalani, kumpiga mtuhumiwa, kumuumiza na kumuua badala ya kumfikisha katika vyombo vya usalama kama vile polisi.

Faida nyingine za utawala wa kidemokrasia ni kuwa huru. Kuna aina nyingi za uhuru: uhuru wa kutoa mawazo, uhuru wa kuabudu, uhuru wa kushirikiana na watu wengine na uhuru wa kuishi mahali popote bila kuvunja sheria za nchi. Pia, hukuza hali ya *uwajibikaji.* Viongozi huwajibika

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 140 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa wananchi kwa kutoa huduma kulingana na nafasi na madaraka yao. Wananchi nao huwajibika kwa serikali yao kwa kulipa kodi stahiki na kushiriki katika shughuli za maendeleo. Aidha, kuwepo kwa *mgawanyo wa madaraka* katika mihimili ya dola (Bunge, Mahakama na Serikali) ni nguzo nyingine muhimu ya demokrasia. Mgawanyo huo huepusha kuingiliana katika kutekeleza majukumu yao. Hali kadhalika, nguzo nyingine muhimu ya demokrasia ni kuwepo kwa *uvumilivu wa kisiasa*. Uvumilivu wa kisiasa ni ile hali ya kuheshimu maoni ya wengine hata kama hatukubaliani nayo. Kanuni hii hujenga amani na utulivu katika nchi yoyote ile.

**Zoezi la 1**

1. Eleza umuhimu wa ukweli na uwazi katika utawala wa kidemokrasia.
2. Kwa nini uvumilivu wa kisiasa ni muhimu katika utawala wa kidemokrasia?
3. Eleza kwa nini utii wa sheria ni muhimu katika utawala wa kidemokrasia?
4. Nani anapaswa kuwajibika katika utawala wa kidemokrasia? Anawajibika vipi?
5. Taja faida za uhuru wa kujieleza katika utawala wa kidemokrasia.

**Kazi ya Kufanya**

Andika kwenye daftari lako jinsi misingi ya utawala wa kidemokrasia unavyotekelezwa shuleni kwako. Kisha, wasilisha daftari lako kwa mwalimu wa somo.

## Kazi za vyama vya siasa

Kabla ya kueleza kazi za vyama vya siasa ni vyema tukaanza na dhana ya vyama vya siasa. Vyama vya siasa ni mkusanyiko wa watu wenye itikadi moja yenye lengo la kushawishi na kushika dola au utawala. Vyama vya siasa vina kazi za kuelimisha na kushawishi watu kuhusu sera zao na malengo yao na kukosoa utendaji wa serikali iliyopo madarakani. Pia, ni jukumu la vyama vya siasa kuweka dira ya nchi au kuonesha njia mbadala za utatuzi wa changamoto zinazoikabili jamii katika kukuza na kudumisha



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 141 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

amani ya nchi. Jukumu lingine ni kukuza ushirikiano miongoni mwa vyama vya siasa na kuitisha mikutano ya ndani ya vyama vyao na ile ya hadhara. Pia, vyama hufanya kampeni wakati wa harakati za uchaguzi.

Ili kudumisha demokrasia ya nchi, vyama vya siasa hufanya mikutano ya kisiasa kwa lengo la kunadi sera zao na kuhakikisha serikali inatimiza wajibu wake kwa wananchi. Pia, huomba kura kwa wananchi wakati wa chaguzi mbalimbali na kujenga uhusiano mwema na vyama vingine vya siasa. Vyama hivyo vina wajibu wa kuhamasisha wananchi kushiriki shughuli za maendeleo na kutetea haki kwa kupinga aina yoyote ya unyonyaji na ukandamizaji. Hali kadhalika, vyama vya siasa vina wajibu wa kudumisha amani.

**Soma kwa makini mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mwenyekiti:** Ndugu wajumbe karibuni kwenye kikao.

**Wajumbe (wote):** Asante!

**Mwenyekiti:** Naomba nimkaribishe Katibu wetu asome muhtasari wa kikao kilichopita. Karibu!

**Katibu:** Asante Mwenyekiti! Kikao kilichopita tulijadili katiba ya chama chetu na namna bora ya kuimarisha chama. Pia, tulizungumzia namna bora ya kuongeza wanachama wapya ili wajiunge na chama chetu. Ajenda za leo ni mbili: kwanza, kujadili majina ya wanachama wapya; pili, kujadili wanachama wawili wanaoomba nafasi za uenyekiti ndani ya chama.

**Mwenyekiti:** Ndugu wajumbe naamini mmesikiliza kwa makini ajenda za kikao chetu cha leo. Karibuni kwa majadiliano kwa ajenda ya kwanza. *(Katibu anasoma majina ya wanachama wapya walioomba kujiunga na chama. Wajumbe wanajadiliana kwa pamoja na kufikia maamuzi ya kuyakubali majina yaliyoletwa mbele yao)*.

Katibu! Tuendelee na ajenda ya pili.

**Mjumbe 1:** Mwenyekiti hatuna haja ya kupoteza muda, naona tupitishe tu jina la kwanza.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 142 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mjumbe 2:** Mimi naona bora tupitishe jina la pili. Huyu atatufaa zaidi.

**Mwenyekiti:** Wajumbe, naamini kila mtu amesikia mawazo ya wajumbe wenzetu. Wajumbe wengine mnasemaje?

**Mjumbe 3:** Asante mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mawazo yangu. Mimi nadhani ni bora tungewapigia kura wote.

**Mwenyekiti:** Jamani wajumbe mnasemaje?

**Wajumbe (wote):** Ndiyo. Tupige kura! Tupige kura!

**Mwenyekiti:** Katibu! Naomba uandae karatasi za kupigia kura. Pia, kila mgombea amteue mtu atakayesimama kama 'Wakala' katika zoezi la kuhesabu kura. *(Katibu anasoma tena majina ya wagombea wa nafasi ya mwenyekiti mpya. Mwenyekiti anawapa nafasi ya kujieleza wagombea mbele ya wajumbe. Kisha anawapa nafasi wajumbe wawaulize wagombea maswali matatu kila mmoja. Wagombea wanapomaliza kujibu maswali, kura zinapigwa na kuhesabiwa kisha matokeo yanatangazwa na mwenyekiti mbele ya wajumbe).*

Ndugu wajumbe, katika ajenda zetu mbili tulizozijadili, kwanza napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha wanachama wapya katika umoja wetu. Pili, namtangaza mgombea namba mbili kuwa ndiye Mwenyekiti wetu mteule baada ya kupata kura nyingi zaidi ya mpinzani wake. Asanteni sana kwa kushiriki zoezi hili kwa uwazi.

*(Mwenyekiti anampa nafasi mwenyekiti mteule atoe neno la kuwashukuru wajumbe kwa niaba ya wajumbe wapya. Kikao kinaahirishwa).*

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 143 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

1. Wagombea wangapi waligombea nafasi ya uenyekiti wa chama?
2. Kwa nini walimkataa mgombea wa kwanza katika nafasi ya uongozi?
3. Ni vipengele vipi vinavyoonesha ukweli na uwazi katika uchaguzi huu?
4. Ukweli na uwazi umesaidiaje kwenye uchaguzi huu?
5. Vyama vya siasa vina manufaa yapi kwa wananchi?

**Kazi ya Kufanya**

Bainisha matendo ya kidemokrasia yanayofanyika hapo shuleni. Orodhesha kwenye daftari, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Umuhimu wa uvumilivu wa kisiasa

Uvumilivu wa kisiasa ni hali ya wananchi wenye imani au itikadi tofauti za kisiasa kukubali mawazo ya watu wengine wenye imani au itikadi tofauti na za kwao. Mfano mzuri wa uvumilivu wa kisiasa ni pale ambapo mikutano ya vyama vya siasa kufanywa bila kuingiliwa au kuvurugwa na wanachama wa vyama vingine. Katika hali hii, wanachama wa vyama tofauti vya siasa hukubali kukosoana na kushindana kwa misingi ya haki, ukweli na amani. Aidha, uvumilivu wa kisiasa huwezesha wanachama wa vyama vyote katika eneo husika kuishi na kufanya kazi pamoja bila kubaguana. Ni jambo jema wananchi kuheshimu maoni ya wengine hata kama hawakubaliani nayo.

Kuwa mvumilivu, humsaidia mtu kustahimili hoja zinazokinzana na mtu mwingine kisiasa. Huonesha ukomavu wa kisiasa. Uvumilivu wa kisiasa husaidia kuimarisha ukomavu katika siasa, kustahimili majibizano ya kisiasa na kutojichukulia sheria mkononi. Hata pale ambapo chama kimoja kimeshindwa katika uchaguzi wa kidemokrasia, ni jambo jema kukubali matokeo ili kudhihirisha uvumilivu wa kisiasa.

Nchini Tanzania kuna vyama vya siasa kadhaa ambavyo vimeanzishwa na kupata usajili wa kudumu kwa mujibu wa sheria. Usajili huu hufanywa na ofisi ya msajili wa vyama vya siasa. Tanzania imekuwa chini ya mfumo wa vyama vingi kabla ya uhuru mwaka 1961 (ikijulikana kama Tanganyika)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hadi mwaka 1965. Baada ya hapo mfumo huu ulibadilishwa na kuingizwa mfumo mwingine wa chama kimoja cha siasa hadi mwaka 1992, ambapo mfumo wa vyama vingi ulirejeshwa tena nchini. Tangu kurejeshwa kwa mfumo huu kumekuwepo na ongezeko kubwa la idadi ya vyama vingi vya siasa. Vifupisho vya majina ya vyama hivyo na virefu vyake ni kama ifuatavyo:

| Na. | Jina la chama cha siasa | Kirefu chake |
|---|---|---|
| 1. | ACT-Wazalendo | Alliance for Change and Transparency - Wazalendo |
| 2. | ADC | Alliance for Democratic Change |
| 3. | CCK | Chama cha Kijamii |
| 4. | CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| 5. | CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| 6. | CHAUMA | Chama cha Ukombozi wa Umma |
| 7. | CUF | The Civic United Front |
| 8. | DEMOKRASIA MAKINI | Demokrasia Makini |
| 9. | DP | Democratic Party |
| 10. | NCCR-Mageuzi | National Convention for Construction and Reform – Mageuzi |
| 11. | NLD | National League for Democracy |
| 12. | NRA | National Construction Alliance |
| 13. | SAU | Sauti ya Umma |
| 14. | TADEA | Tanzania Democratic Alliance |
| 15. | TLP | Tanzania Labour Party |
| 16. | UDP | United Democratic Party |
| 17. | UMD | Union for Multiparty Democracy |
| 18. | UPDP | United People's Democratic Party |

*Jedwali namba 1: Majina ya vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu nchini Tanzania*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha hii, kisha tafakari moja ya misingi ya kidemokrasia kipindi cha uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani.**




*Kielelezo namba 1: Wananchi wakishiriki kupiga kura*

## Wajibu wa vyama vya siasa katika ushindani wa kidemokrasia

Vyama vya siasa vipo kisheria na vinapaswa kufanya shughuli zake kwa kufuata sheria ya vyama vya siasa. Vinawajibika kwa msajili wa vyama vya siasa. Wajibu wa viongozi ni kufanya mikutano ya kisiasa, kunadi sera zao na kushawishi wananchi ili wakubaliane na sera za vyama vyao. Aidha, vinawajibika kujenga uhusiano mwema na vyama vingine, kujenga demokrasia na kudumisha utamaduni wa umoja. Pia, kuandaa na kufanya uchaguzi ndani ya vyama vyao ili kuweza kupata viongozi. Hivyo, ni vyema vyama vya siasa vikaongozwa kwa mujibu wa katiba za vyama vyao.

Viongozi wa chama wana wajibu wa kuhamasisha wanachama na wananchi wengine kushiriki shughuli za maendeleo. Aidha, wanao wajibu wa kuandaa na kusimamia kampeni wakati wa chaguzi mbalimbali na kuhakikisha chama chao kinashika dola. Wanachama nao wana wajibu wa kutekeleza sera za vyama vyao kwa kufuata ilani za vyama vyao. Pia, wanao wajibu wa kushiriki katika mikutano ya kisiasa na kunadi sera za vyama vyao. Aidha, wanatakiwa kujenga mshikamano miongoni mwa wanachama wenzao na wananchi wengine bila kujali itikadi za vyama vyao pale ambapo maslahi ya nchi yanahitajika kulindwa. Vilevile, wanatakiwa kuheshimu bendera na sare za vyama vingine na kufuata sheria na taratibu za nchi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 146 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

1. Kwa nini ni muhimu kwa vyama vya siasa kuheshimu mikutano ya kisiasa ya vyama vingine?
2. Uvumilivu wa kisiasa una faida zipi?
3. Vyama vya siasa vinawezaje kujenga umoja wa Watanzania?
4. Viongozi wa vyama vya siasa wana wajibu gani?
5. Ni vitendo vipi vya wanachama na vyama vya siasa vinavyoonesha ukomavu wa kisiasa na kuheshimu itikadi za vyama vingine?
6. Kuna umuhimu gani wa vyama vya siasa kufuata sheria na taratibu za nchi ?

**Kazi ya Kufanya**

Andika majina ya wenyeviti wa vyama vya siasa na vyama vyao vyenye usajili wa kudumu nchini Tanzania. Kisha, wasilisha kwa mwalimu wa somo.

### Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Katiba ni sheria, kanuni na taratibu za nchi zinazotumika kuendesha shughuli za nchi, shirika, chama au kikundi cha watu wenye malengo yanayofanana.

Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina jumla ya sura kumi. Kila sura ina vipengele kadhaa kama zilivyofafanuliwa hapa chini:

**Sura ya kwanza:** Inahusu Jamhuri ya Muungano, vyama vya siasa na itikadi ya ujamaa na kujitegemea. Sura hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: Jamhuri ya Muungano na watu, malengo muhimu na misingi ya mwelekeo wa shughuli za serikali, haki na wajibu muhimu. Katika sehemu ya haki na wajibu umuhimu umewekwa katika kuzingatia haki ya usawa, haki ya kuishi, haki ya uhuru wa mawazo, haki ya kufanyakazi, wajibu wa jamii na madaraka ya pekee ya mamlaka ya nchi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 147 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya pili:** Inaelezea serikali ya Jamhuri ya Muungano na mgawanyiko wake. Sehemu ya kwanza inahusu Rais wa Jamhuri ya Muungano, kazi na mamlaka yake. Sehemu ya pili inahusu Makamu wa rais, kazi na mamlaka yake na sehemu ya tatu, Waziri mkuu, Baraza la Mawaziri na Serikali.

**Sura ya tatu:** Inahusu Bunge la Jamhuri ya Muungano. Mambo yaliyomo katika sura hii ni kuhusu Bunge lenyewe, Wabunge, Wilaya za uchaguzi na Uchaguzi wa wabunge, Utaratibu, Madaraka na Haki za Bunge.

**Sura ya nne:** Inahusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na pia Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**Sura ya tano:** Inahusika na utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano. Mambo yanayohusika katika sehemu hii ni Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, Tume ya Kuajiri ya Mahakama ya Tanzania Bara, Mahakama Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Sura hii ina sehemu saba zinazohusu utoaji haki katika Jamhuri ya Muuungano.

**Sura ya sita:** Imezungumzia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Sura hii ina vipengele viwili muhimu: Haki za Binadamu na Utawala Bora na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Sura ya saba:** Inahusu masharti kuhusu mchango wa serikali na mambo mengine ya fedha zinazoingia katika hazina ya serikali ya Jamhuri ya Muungano. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni Mchango na Mgawanyo wa Mapato ya Jamhuri ya Muungano pamoja na mfuko mkuu wa Hazina na fedha za Jamhuri ya Muungano.

**Sura ya nane:** Inahusu Madaraka ya Umma katika serikali za mitaa na kazi za serikali za mitaa.

**Sura ya tisa:** Inahusu majeshi ya Ulinzi na Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu.

**Sura ya kumi:** Inahusu mengineyo. Mfano, jina la katiba, tarehe ya kuanza kutumika katiba hiyo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mwananchi wa 1:** Habari za leo?

**Mwananchi wa 2:** Nzuri, leo ni siku yetu muhimu ya kufanya uchaguzi wa wenyeviti wa kamati za mitaa.

**Mwananchi wa 3:** Ni kweli, tena ni jukumu letu kikatiba.

**Mwananchi wa 1:** Jukumu la kikatiba kivipi?

**Mwananchi wa 3:** Kwa kuwa katiba ni sheria mama inayoongoza namna ya kuendesha shughuli katika nchi. Hivyo, hata haki ya kuchagua au kuchaguliwa imeainishwa katika katiba.

**Mwananchi wa 1:** Asante, maana umenielimisha.

**Mwananchi wa 2:** Kweli kabisa, katiba yetu imeainisha wajibu wetu kama raia kutii sheria za nchi.

**Mwananchi wa 3:** Sawa, basi twendeni tukatimize haki yetu ya kikatiba kwa kuchagua viongozi watakaotufaa.

**Mwananchi wa 1:** Ni kweli, twendeni.

## Zoezi la 4

1. Eleza maana ya katiba.
2. Je, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina sura ngapi?
3. Je, kuna faida gani za kujua katiba ya nchi yako?
4. Je, ni haki zipi zimeainishwa katika sura ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?
5. Mwananchi wa 3 amewaelimisha wenzake kuhusu nini?

## Kazi ya Kufanya

Azima Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwalimu wako, kisha jadiliana na wenzako kuhusu kazi ya katiba na baini haki za binadamu zilizoainishwa katika katiba.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 149 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Aina, sifa na wajibu wa raia wa Tanzania

Uraia ni hali ya mtu kutambulika chini ya sheria kama mwananchi mwenye haki zote katika nchi fulani. Nchini Tanzania uraia umeainishwa kuwa ni wa aina tatu. *Aina hizo ni uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia wa kujiandikisha.* Uraia wa kuzaliwa ni ule ambao mtu anakuwa nao kwa haki ya kuzaliwa Tanzania. Uraia wa kurithi ni ule unaomuhusu mtoto aliyezaliwa nje ya nchi kupewa uraia wa Tanzania kwa kigezo cha mzazi mmojawapo au wazazi wote wawili kuwa ni raia wa Tanzania. Aina nyingine ni uraia wa kujiandikisha: hii ni aina ya uraia ambayo raia wa nchi nyingine anaweza akapewa uraia wa Tanzania kwa kuomba katika ofisi za uhamiaji nchini.

**Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Chezo:** Shikamoo Mjomba!

**Mjomba:** Marahaba Chezo. Habari za shule?

**Chezo:** Nzuri mjomba, kila siku nakuona unakwenda kazini, kwani mjomba unafanya kazi wapi?

**Mjomba:** Nafanya kazi Dar es Salaam katika ofisi za uhamiaji.

**Chezo:** Ahaa! Ninyi ndio mnaotoa uraia na hati za kusafiria nje ya nchi?

**Mjomba:** Ndiyo!

**Chezo:** Kwani raia wa Tanzania anatakiwa awe na sifa gani mjomba?

**Mjomba:** Anatakiwa awe amezaliwa hapa Tanzania, wazazi wake, babu na bibi zake nao wawe wamezaliwa Tanzania. Kwa anayeomba uraia ni lazima kwanza aukane uraia wa taifa lake kwa maandishi ndipo aandikishwe kuwa raia wa Tanzania. Raia wa Tanzania anatakiwa asiwe na uraia wa nchi nyingine. Pia, kila raia wa Tanzania anatakiwa awe mzalendo.

**Chezo:** Ahaa! Je, anayeomba uraia anatakiwa awe na sifa zipi?

**Mjomba:** Kwa mujibu wa Sheria ya Uraia namba 6 ya mwaka 1995

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 150 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kanuni zake za mwaka 1997, mgeni anayeomba uraia wa Tanzania anatakiwa awe na umri wa miaka 18 au zaidi, mwenye akili timamu na uwezo wa kufanya maamuzi. Pia, anatakiwa ajaze fomu za maombi zinazopatikana katika ofisi zote za uhamiaji hapa nchini na maombi hayo yatangazwe katika vyombo vya habari vya serikali. Vilevile, awe hajawahi kukutwa na kosa lolote la jinai tokea alipoingia hapa Tanzania. Pia, anatakiwa aukane kwa maandishi uraia wa nchi yake aliyozaliwa au anayotoka. Vilevile, awe ameishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miezi 12 mfululizo kabla ya kuwasilisha ombi lake na katika kipindi cha miaka 10 awe ameishi Tanzania kwa kipindi kisichopungua miaka 7.

**Chezo:** Sasa nimeelewa. Kumbe mimi ni raia wa kuzaliwa, maana nimezaliwa hapa nchini. Baba na mama yangu, babu pamoja na bibi wote wamezaliwa hapa nchini Tanzania.

**Mjomba:** Nashukuru kama umenielewa.

**Chezo:** Asante sana mjomba.

## Zoezi la 5

1. Taja aina tatu za uraia nchini Tanzania.
2. Idara gani ina mamlaka ya kutoa uraia nchini Tanzania?
3. Raia wa Tanzania anatakiwa awe na sifa gani?
4. Uraia wako ni wa aina ipi? Kwa nini?
5. Unathibitishaje kuwa wewe ni raia wa Tanzania?
6. Orodhesha masharti ya kupewa uraia wa Tanzania kama wewe si mzaliwa wa Tanzania.

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu hatua za kuchukua unapohisi kuna watu wanaoishi nchini ambao si raia na hawana vibali vya kuishi nchini. Orodhesha hatua hizo kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Wajibu wa raia

Kila raia ana wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wajibu ni mambo ambayo kila raia anatakiwa kuyatimiza kwa mujibu wa sheria za nchi. Je, raia wa Tanzania ana wajibu gani?

Kama raia una wajibu wa kushiriki kwa kujituma kufanya kazi halali za uzalishaji mali. Unatakiwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa jamii na uchumi wa nchi. Pia, unatakiwa kufuata sheria za nchi kwa mujibu wa katiba yetu na kuwafichua wanaokiuka sheria za nchi. Hali kadhalika, unatakiwa kupiga vita aina zote za ubadhirifu na uharibifu wa mali za umma. Unatakiwa kulinda mipaka ya nchi yetu na kuwafichua maadui wa nchi yetu. Vilevile, unatakiwa kuheshimu mali ya mtu mwingine na kulinda mali zetu wenyewe na maliasili za nchi. Aidha, unatakiwa kulinda, kudumisha na kuhifadhi uhuru, mamlaka na umoja wa taifa.

### Zoezi la 6

1. Je, unafahamu wajibu wako wa msingi kama raia wa Tanzania?
2. Ni wajibu upi ambao umewahi kuutekeleza kama raia wa nchi?
3. Ni wajibu upi ambao hujawahi kuutekeleza na kwa nini?

### Kazi ya Kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako namna mtakavyoelimisha jamii kuhusu wajibu wa raia wa Tanzania. Andika mapendekezo hayo kwenye daftari lako na wasilisha kwa mwalimu wako wa somo.

### Zoezi la 7

**Sehemu A**

Andika **Kweli** au **Si Kweli** katika sentensi hizi:

1. Misingi ya demokrasia inazingatia haki za binadamu. ________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Utawala wa demokrasia unatambulika kwa kutii sheria za nchi pekee. ________

3. Katika mfumo wa kidemokrasia wananchi ni wapokeaji tu, hawawajibiki kwa lolote. ________

4. Wanawake hawana haki sawa na wanaume katika mfumo wa demokrasia. ________

5. Kazi mojawapo ya vyama vya upinzani hapa nchini si kukosoa utendaji wa serikali ya chama tawala. ________

6. Uvumilivu wa kisiasa kwa vyama vyote hudumisha amani. ________

7. Mikutano ya vyama vya siasa ikivurugwa na wanachama wa vyama vingine inaonesha ukomavu wa kisiasa. ________

**Sehemu B**

**Andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku**

8. Wajibu mojawapo wa raia wa Tanzania ni:
   (a) kujitangaza kwenye vyombo vya habari ili watu wote wakufahamu
   (b) kutumia mali za umma kadri unavyoweza
   (c) kulinda, kudumisha na kuhifadhi uhuru, mamlaka na umoja wa taifa

9. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina sura ngapi?
   (a) 9
   (b) 10
   (c) 11

10. Kazi ya vyama vya siasa nchini ni pamoja na:
   (a) kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo
   (b) kuitisha mikutano ya hadhara na kuhamasisha maandamano ya uvunjifu wa amani nchini
   (c) kuomba kura kwa wananchi wakati wa uchaguzi tu

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 153 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

11. Kuwa na uhuru wa kutoa maoni ni moja ya nguzo za:
    (a) kutii sheria
    (b) uwajibikaji
    (c) demokrasia
12. Mgawanyo wa madaraka husaidia:
    (a) kuepusha kuingiliana katika kutekeleza majukumu
    (b) kupunguza kazi na kupinga unyonyaji
    (c) mtu mwenye madaraka kunyenyekewa
13. Wanachama wa vyama tofauti vya siasa wanapokosoana na kushindana kwa misingi ya haki, ukweli na amani, hali hii tunaweza kuiita:
    (a) utulivu wa kisiasa
    (b) uvumilivu wa kisiasa
    (c) changamoto za kisiasa
14. Mtu anapata uraia wa Tanzania kwa kuzaliwa, kurithi na:
    (a) kuwatembelea wazazi wanaoishi Tanzania
    (b) kutumia kitambulisho cha mpiga kura
    (c) kujiandikisha
15. Sifa mojawapo ya mtu anayeomba uraia wa Tanzania:
    (a) aukubali uraia wa nchi alikotoka kwa maandishi
    (b) sio lazima kutangaza kwenye vyombo vya habari
    (c) awe hajawahi kukutwa na kosa lolote la jinai toka aingie nchini

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Lukuki | nyingi au idadi kubwa sana |
| Kinzana | pingana au bishana kwa hoja |
| Wakala | mwakilishi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Kudumisha amani

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza kuheshimu tofauti za kitamaduni na kuishi na watu wenye asili tofauti. Maudhui ya sura hii yatakuwezesha kufahamu umuhimu wa kuchangamana na watu wenye asili tofauti na kukemea ubaguzi ili kudumisha amani. Pia, utajifunza kuheshimu haki ya uhuru wa kuishi, utu na kujihadhari na wageni. Aidha, utajifunza kuheshimu mitazamo miongoni mwa watu wa jamii mbalimbali na kujenga urafiki mwema na mataifa mengine. Je, amani ni nini? Je, amani inatokana na nini? Tanzania ni nchi mojawapo inayosifika kwa kuwa na amani na utulivu. Hivyo basi, amani ni hali ya usalama isiyokuwa na fujo au vita. Kwa nini Tanzania inasifika kwa amani? Sifa hii ni matokeo ya upendo, mshikamano, ushirikiano, kujaliana, kuheshimiana na utu uliopo miongoni mwa Watanzania.

### Kuchangamana na watu wenye asili tofauti

Kuchangamana ni hali ya kuwa pamoja na kushirikiana na watu katika shughuli mbalimbali bila kujali tofauti za kisiasa, kidini, rangi, asili, jinsi hali ya mtu au hadhi yake. Je, darasani kwako kuna wanafunzi wenye asili tofauti?

**Chunguza picha hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**



*Kielelezo namba 1: Kuchangamana na watu wa asili tofauti*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Unaona nini katika picha hii?
2. Je, umewahi kuishi na watu wenye asili tofauti?
3. Je, ni rahisi kwako kushirikiana na watu wenye asili tofauti? Eleza ni kwanini.
4. Kwa nini ni vizuri kuchangamana na watu wenye asili tofauti?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako njia mtakazotumia kuchangamana na watu wenye asili tofauti. Kisha, andika katika daftari lako njia mlizojadili na wasilisha kwa mwalimu wako wa somo.

## Faida za kuchangamana na watu wa asili tofauti

Kuna faida gani kuchangamana na watu wenye asili tofauti? Bila shaka katika zoezi lililopita umejifunza faida za kuchangamana na watu wenye asili tofauti. Ni vyema ukatambua kuwa katika jamii zetu na hata shuleni, tunaishi na watu wenye asili tofauti. Hivyo, yatupasa kuheshimu tofauti hizo na kukemea jambo lolote linaloondoa au kudhoofisha huo mchangamano.

## Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Dadi ni mvulana anayesoma darasa la tano katika shule ya msingi Kandete, iliyopo katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma. Dadi ana rafiki anayeitwa Raja mwenye asili ya Kihindi. Raja anasoma shule ya msingi Hansanga iliyopo mkoani Arusha. Raja alikuwa na kawaida ya kwenda Songea kumtembelea shangazi yake wakati wa likizo na ndipo walipofahamiana na Dadi. Siku moja Dadi alipokuwa anarudi nyumbani akitoka uwanjani alikutana na rafiki yake Yusufu. Dadi alimwambia Yusufu kuwa ana rafiki mwenye asili ya kihindi aitwaye Raja na anataka kujifunza ngoma ya mganda ambayo huchezwa mkoani Ruvuma. Yusufu akamshauri Dadi kuwa ampeleke Raja Mbamba Bay ambako kuna mashindano ya mganda. Dadi akapokea ushauri na akamshirikisha rafiki yake Raja. Raja akakubali na wakapanga safari kesho yake.*



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 156 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Muda ulipowadia, Dadi na Raja wakapanda gari kuelekea Mbamba Bay (Nyasa) ambako kulikuwa na mashindano ya ngoma ya mganda. Wakiwa Mbamba Bay, katikati ya mchezo huo, Raja aliingia na kuanza kucheza. Rafiki yake Dadi na wachezaji wengine wa mganda walifurahi sana kuona Raja akicheza ngoma ya mganda. Japo haikuwa asili yake, Raja alijifunza haraka na aliweza kucheza ngoma ya mganda vizuri.*

**Zoezi la 2**

1. Umejifunza nini kutokana na vitendo alivyovifanya Dadi?
2. Ni vitendo gani vinafaa kuigwa? Kwa nini?
3. Umejifunza nini kutoka kwa Raja?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako juu ya umuhimu wa kuchangamana kama walivyofanya Raja na Dadi. Kisha, andika matokeo ya majadiliano hayo kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wako wa somo.

## Kukemea ubaguzi

Ubaguzi ni mfumo wa kijamii wa kutoa vitu au huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsi au kabila. Ubaguzi wa aina yoyote si jambo jema na linapaswa kukemewa kwa nguvu zote. Watanzania hatuna desturi ya kubagua watu wengine kwa misingi ya dini, jinsi, rangi, hadhi ya mtu au ulemavu.

**Soma ngonjera hii kwa makini, kisha jibu maswali yanayofuata.**

***Mpitanjia:*** Hodi hodi uwanjani, niseme yalo moyoni,
Mtu kwao maskani, ingiliana kwa nini?
Kufaidi vya nyumbani, pasipokuja wageni,
Niambie nielewe, kunitoa mashakani.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 157 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mtakaamani:** Ubaguzi jambo baya, kwetu sisi binadamu,
Naongea bila haya, hakuna asofahamu,
Sio kwamba nimepwaya, nimejaa ufahamu,
Nakemea ubaguzi, haufai asilani.

**Mpitanjia:** Tutapoteza asili, muwe makini jamani,
Tusifanye tunajali, kukumbatia wageni,
Hao watokao mbali, kamwe wasije nchini,
Niambie nielewe, kunitoa mashakani.

**Mtakaamani:** Nyerere ni wetu baba, pumzika kwa amani,
Mazuri yake si haba, jamani tuyaenzini,
Ubaguzi si mahaba, hakika tuepukeni,
Nakemea ubaguzi, haufai asilani.

**Mpitanjia:** Unanifumbua macho, lakini sijatosheka,
Hicho kitu usemacho, akilini nakiweka,
Japo naona kificho, sema nipate ridhika,
Niambie nielewe, kunitoa mashakani.

**Mtakaamani:** Hiyo dhambi kuienzi, inatafuna hakika,
Huo mwanzo wa kitanzi, Ulaya na Afrika,
Tudumu enzi na enzi, Tanzania kusifika,
Nakemea ubaguzi, haufai asilani.

**Mpitanjia:** Polepole naelewa, haijanitoka homa,
Sio kama nimelewa, naona umenisoma,
Sema nipate elewa, nami nipate kusema,
Niambie nielewe, kunitoa mashakani.

**Mtakaamani:** Kwa rangi kubaguana, taifa hadi kabila,
Kwa dini tutagombana, ibilisi zake hila,
Binadamu twafanana, twarejea wetu mola,
Nakemea ubaguzi, haufai asilani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Mpitanjia:*** Nami napata elewa, kukemea ubaguzi,
Ubaguzi kupokewa, ni kufuru kwa Mwenyezi,
Amani kuondolewa, hauhitaji chunguzi,
Nakemea ubaguzi, haufai asilani.

***Wote:*** Upendo tudumisheni, udugu pia amani,
Biashara tufanyeni, inua pato nchini,
Mataifa na nyumbani, Tanzania tangazeni,
Tukemee ubaguzi, haufai asilani

**Zoezi la 3**

1. Umejifunza nini katika ngonjera uliyoisoma?
2. Mtakaamani alikuwa anakemea nini?
3. Ni mambo gani yanaweza kusababishwa na ubaguzi?
4. Wewe ungekuwa Mtakaamani ungemwambia nini Mpitanjia?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako darasani mambo mtakayoyafanya kukomesha ubaguzi shuleni kwenu. Andika katika daftari lako mambo hayo, kisha wasilisha daftari kwa mwalimu wa somo.

## Kuchangamana na watu wenye tamaduni tofauti

Katika sehemu hii, tutaongelea kuchangamana na watu wenye tamaduni tofauti. Katika shule yako umewahi kumuuliza rafiki yako kuhusu asili ya utamaduni wake? Katika kipengele ambacho umekisoma, umeshajifunza namna ya kuchangamana na watu wengine na kukemea ubaguzi. Sasa utajifunza namna ya kuchangamana na watu wengine katika nyanja ya utamaduni. Utaendelea kujifunza tamaduni zao kwa kuangalia mambo mbalimbali yanayofanana au kutofautiana. Utamaduni wa taifa moja na mengine huongeza tofauti au kufanana katika mavazi, chakula, lugha, sanaa, michezo, mila na desturi zao pamoja na njia za kuabudu na ufundi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 159 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza picha hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**



*Kielelezo namba 2: Mavazi ya tamaduni tofauti*

**Zoezi la 4**

1. Katika picha hii umeona nini?
2. Kuna tofauti gani ya kimavazi kati ya picha hiyo?
3. Ni mambo gani yanafanana katika mavazi ya picha hii?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako kubaini tofauti za kiutamaduni zilizopo katika eneo unaloishi. Andika katika daftari lako tofauti hizo na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Mipaka ya ushirikiano na watu wenye asili tofauti

Kila jamii ina utamaduni wake katika kuonesha uhai wa jamii hiyo katika maisha yao ya kila siku. Utamaduni huo huunganisha na kutambulisha

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

jamii inayohusika. Huo utambulisho huunda tofauti kati ya jamii moja na nyingine. Hali hii huweka mipaka ya jamii moja dhidi ya jamii nyingine. Hivyo, kila jamii ina mipaka yake ya ushirikiano na jamii nyingine. Mipaka hii imetokana na tamaduni zao. Je, katika jamii unayoishi ni mipaka gani iliyowekwa ya namna ya kushirikiana na watu wenye asili tofauti?

**Soma mazungumzo haya kwa makini, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mgeni:** Hujambo!

**Farijala:** Sijambo, hali yako?

**Mgeni:** Nzuri. (*huku akiendelea kupiga picha*)

**Farijala:** Unafanya nini?

**Mgeni:** Nachukua picha kwani nimependa mazingira haya.

**Farijala:** Je, umewasiliana na uongozi wa mamlaka husika? Maana hapa kwetu maeneo kama vile Ikulu, mahakama, madaraja makubwa au hospitali hayaruhusiwi kufanyika shughuli yoyote ikiwa ni pamoja na kuchukua picha ya mazingira hayo bila idhini ya viongozi wa mamlaka husika.

**Mgeni:** Hapana! Nilikuwa sijui bwana. Mimi nimependa mandhari ya eneo hili la mahakama nikavutiwa kuchukua picha hapa.

**Farijala:** Ni vema nikupeleke kwanza kwenye ofisi ya mamlaka husika ili uweze kujitambulisha na kuomba kibali kabla ya kuendelea na kazi zako.

**Mgeni:** Sawa, twende.

**Farijala:** Haya, twende!

### Zoezi la 5

1. Unafikiri Mgeni alifanya kosa gani?
2. Farijala alimsaidiaje Mgeni?
3. Ungekuwa wewe ndiye Farijala ungefanya nini?
4. Ni mambo gani mengine yanayobainisha mipaka ya ushirikiano na watu wengine wa tamaduni tofauti?



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA NA MAADILI STD V .indd 161 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako katika vikundi namna ya kumsaidia mgeni anayekuja katika eneo unaloishi kwa kufuata mipaka ya ushirikiano iliyowekwa ya kushirikiana na watu wenye asili tofauti. Andika majadiliano hayo kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kufanya kazi pamoja na watu wenye asili na tamaduni tofauti

Katika kipengele kilichopita umejifunza kutambua mipaka ya ushiriki wa watu wenye asili tofauti katika shughuli za kijamii. Katika sehemu hii utaendelea kutambua namna unavyoweza kufanya kazi pamoja na watu wenye asili tofauti waishio Tanzania. Hii itakuwezesha kubadilishana uzoefu, kujifunza ushirikiano bila ya kutoa siri za nchi na viongozi, kuchuja mambo ya kuzungumza na kulinda utaifa wetu. Je, katika eneo lako umewahi kufanya kazi gani na watu wenye asili tofauti?

**Zoezi la 6**

1. Orodhesha baadhi ya kazi ambazo tunafanya pamoja na watu wenye asili tofauti waishio Tanzania.
2. Kuna umuhimu gani wa kushirikiana kufanya kazi na watu wenye asili tofauti?

**Kazi ya Kufanya**

Bainisha kazi unazoziona zinafanywa pamoja na watu wenye asili tofauti kwenye eneo unaloishi. Orodhesha kazi hizo kwenye daftari lako kisha wasilisha kwa mwalimu wako wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Siku moja Asia alipokuwa darasani akimsikiliza mwalimu wa somo la Uraia na Maadili, ghafla alianza kuumwa tumbo. Mwalimu wake aliwaita wenzake wamsaidie kumpeleka zahanati ya kijiji. Baada ya kumchunguza, alionekana kuwa na tatizo kubwa, hivyo walimpeleka hospitali ya wilaya.

Walipofika huko waliwakuta wauguzi na madaktari wenye asili tofauti. Asia aliogopa sana, alihofia uhai wake. Muuguzi wa kiume mwenye asili ya Kichina alimtia moyo Asia na kumsihi asiwe na hofu. Kisha, alimpeleka haraka wodini na alianza kumchunguza na kumpima vipimo vyote. Vipimo vilionesha kuwa Asia alikuwa na uvimbe tumboni. Hivyo, alitakiwa kufanyiwa upasuaji. Asia alikubali na madaktari waliendelea na maandalizi ya upasuaji.

Asia alipofikishwa chumba cha upasuaji, aliwaona wauguzi wawili wa Kijapani na dakitari mmoja wa Kiafrika. Baada ya upasuaji hali ya Asia iliendelea vizuri. Asia alifurahi sana kwa kupona na kuhudumiwa na watu wenye asili tofauti kwa upendo. Madaktari walifanya kazi kwa ushirikiano kuhakikisha wanaokoa maisha yake.

## Zoezi la 7

1. Wahudumu waliomhudumia Asia ni watu wa asili gani?
2. Unafikiri ni kwa nini alihofu kuhudumiwa na watu wenye asili tofauti?
3. Taja faida za ushirikiano kati ya watu wenye asili tofauti katika kuleta maendeleo au kutoa huduma.

## Kazi ya Kufanya

Jadiliana na mwenzako kuonesha baadhi ya maeneo ambayo unadhani ni muhimu ushirikiano katika kufanya kazi udumishwe bila kujali tofauti za asili au utamaduni. Andika majadiliano hayo kwenye daftari lako, kisha uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 163 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuheshimu tofauti za kiutamaduni

Kuheshimu tofauti ni moja ya nguzo muhimu ya kudumisha amani. Amani haiwezi kudumishwa bila ya kukubali uwepo wa tofauti za kiutamaduni na kimitazamo. Katika kipengele hiki cha kuheshimu tofauti za kiutamaduni, utajifunza kuelezea utamaduni wa kabila lako na kutambua tofauti za kiutamaduni katika jamii.

## Asili ya utamaduni wa kabila lako

Bila shaka unatambua kuwa kila mmoja wetu ana kabila lake. Kila kabila lina asili yake na utamaduni wake. Je, unajua kabila lako? Je, unafahamu utamaduni wa kabila lako? Je, unaweza kueleza asili na utamaduni wa kabila lako? Je, unajivunia asili ya kabila lako?

Kila kabila lina namna ya kuenzi na kudumisha utamaduni wao kwa kurithisha lugha yao ya asili kwa watoto ili kuidumisha lugha hiyo. Pia, hurithisha ufundi kama vile uchongaji, uhunzi na ususi. Makabila mengi yanadumisha asili yao kwa kuendeleza vyakula vyao, ngoma za asili, salamu, mavazi, mila na desturi.

**Imba wimbo huu unaoitwa *Jieleze mwenzangu*, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Jieleze x 6
   Najieleza dada!
   Mimi hapa Nyemo Mazengo
   Kabila langu ni Mgogo,
   Asili yangu ni Dodoma,
   Najieleza dada!
   Chakula chetu ugali mlenda,
   Lugha yetu ni Kigogo,
   Nguo zetu ni kaniki.
   Najieleza dada!

2. Jieleze x 6
   Najieleza kaka!
   Mimi hapa Said Komba,
   Kabila langu ni Mngoni,
   Asili yangu ni Songea,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Najieleza kaka!
Chakula chetu ugali maharage,
Lugha yetu ni Kingoni,
Nguo zetu mgolole mwekundu
Ngoma yetu Lizombe

**Zoezi la 8**

1. Ni mambo gani yanayotambulisha asili ya kabila lolote?
2. Taja mambo yanayoelezea kabila lako.
3. Taja njia zinazofanywa na kabila lako kudumisha utamaduni.

**Kazi ya Kufanya**

Jadili na wenzako kuhusu asili ya kabila la kila mmoja wenu kwa kutaja mambo yanayowatambulisha. Andika mambo hayo katika daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Tofauti za kiutamaduni katika jamii

Bila shaka umeshatambua kuwa katika jamii kuna tamaduni tofautitofauti. Tofauti hizi za tamaduni zinatokana na kutofautiana katika mila na desturi za jamii husika. Je, nini maana ya mila na desturi? Nini tofauti ya mila na desturi?

Mila ni utaratibu wa maisha ya watu au jamii ambao umekuwa ukiendelea kwa siku nyingi. Desturi ni mambo yanayotendwa kila siku kadiri ya matakwa ya jamii husika. Mila na desturi huchangia kujenga tabia za watu katika jamii husika. Kuna mila na desturi zinazofaa na zisizofaa. Mila na desturi zinazofaa hupaswa kudumishwa, kuendelezwa na kufuatwa na kila jamii. Mfano wa mila zinazofaa ni jando na unyago, kuoana, kuzikana na kusalimiana. Hata hivyo, desturi hubadilikabadilika kwa sababu uwepo wake hutegemea vilevile mazingira yaliyopo na upeo wa watu wanaohusika. Unaweza kusema desturi ni vipengele vidogovidogo vya mila. Kwa mfano, katika mila ya kusalimiana, kuna wengine wana desturi ya kushikana mikono, wengine wanakumbatiana, wengine wanapiga magoti na wengine hawashikani mikono. Wote hawa wanasalimiana, ila namna ya kusalimiana inatofautiana. Hata hivyo, hali hii huweza kubadilika kulingana na wakati na upeo wa jamii inayohusika.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mila na desturi ni mambo yanayowaunganisha wanajamii na kujiona wamoja. Watanzania pia wana mila na desturi zinazowaunganisha. Mfano, lugha ya Kiswahli inaunganisha Watanzania wengi. Pia, tuna desturi ya upendo, mshikamano na ushirikiano katika shughuli mbalimbali za kijamii.

## Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Asha ni mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Boma iliyopo mjini Morogoro. Tangu alipozaliwa, hajawahi kutambulishwa asili ya utamaduni wa wazazi wake. Hii inatokana na wazazi wake kutopenda kuenzi asili ya tamaduni zao. Hii inamfanya Asha asione thamani ya asili ya utamaduni wake. Wazazi wa Asha hawapendi vyakula vya asili. Pia, wanatumia vitu na mavazi yenye asili ya ughaibuni. Vilevile, hawaongei lugha ya asili ya kabila lao. Hii imemfanya Asha kutojua lugha ya asili ya kabila lake. Japo yeye anapenda lakini, imemlazimu kuwa hivyo. Hata michezo na ngoma za asili ya kabila lake hazijui. Amekuwa ni mtoto wa mjini. Asha amejaribu kuwaelekeza wazazi wake umuhimu wa kuenzi na kupenda utamaduni wao. Wazazi wake wameanza kuelewa na kuenzi utamaduni wao.

### Zoezi la 9

1. Orodhesha vitendo ambavyo vinadumaza asili ya utamaduni wetu vinavyofanywa na wazazi wa Asha.
2. Je, tabia gani zingine zinazofifisha utamaduni wetu?
3. Taja manufaa matatu ya kuenzi utamaduni wako.

### Kazi ya Kufanya

Jadili na wenzako kuhusu matendo yasiyoendana na utamaduni yanayojitokeza katika shule yako. Toa ushauri wa namna ya kuenzi na kuendeleza utamaduni wenu. Andika ushauri huo kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 166 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuheshimu haki ya uhuru wa makazi

Bila shaka umeshatambua unapaswa kukemea na kutokomeza ubaguzi ili kudumisha haki ya uhuru wa kuishi kwa raia yeyote yule nchini. Kipengele kingine cha msingi katika kudumisha amani ni kuheshimu haki ya uhuru wa makazi. Hii inahusisha uhuru wa mtu kuishi mahali atakaporidhika kuwa atakidhi mahitaji yake bila kujali asili yake, rangi yake, dini, kabila, kanda na utaifa, au nasaba. Uhuru uliopo Tanzania unamwezesha kila raia asijione mnyonge awapo ndani ya nchi hii.

Je, umewahi kufikiri kuwa unaweza kuishi sehemu yoyote nchini Tanzania bila kubughudhiwa na mtu yeyote?

## Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata

Ikupaeli ni msichana mwenye asili ya Mkoa wa Kilimanjaro. Alimaliza darasa la saba miaka miwili iliyopita katika shule ya msingi iliyopo Rombo, mkoani Kilimanjaro. Mara baada ya kuhitimu elimu yake ya msingi, aliahidi kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili awe mfanyabiashara maarufu. Alianza biashara kwa mtaji mdogo wa kutembeza matunda. Kila alipopata faida aliongeza mtaji na baadaye mtaji ulikua akabadili biashara. Alifungua duka la nguo lakini biashara haikuwa nzuri sana. Kwa kuwa alikuwa mfanyabiashara mkubwa, alipata marafiki wafanyabiashara Waafrika na Wahindi. Hawa walimshauri ahamie sehemu nyingine, lakini alikuwa anakataa kwa kuwa alishazoea mazingira ya Rombo.

Siku moja alipoweka bidhaa dukani, zilikaa muda mrefu zaidi ya vile alivyozoea. Rafiki zake walimsihi ajaribu kutafuta eneo jingine. Ikupaeli alikubali alimua kuhamia Mtwara kama alivyoshauriwa na alipokelewa vizuri na wenyeji wa huko. Pia, walimpa ushirikiano mzuri.

Ikupaeli alijitahidi kuonesha bidii japo kulikuwa na changamoto. Hata hivyo, alijitahidi kukabiliana nazo hadi akafanikiwa na hatimaye biashara yake ilikua na mtaji ukaongezeka mara dufu. Kwa sasa ana maduka makubwa katika mikoa ya Arusha, Mtwara, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Iringa.

### Zoezi la 10

1. Unafikiri kwa nini Ikupaeli aliondoka Rombo na kwenda Mtwara?
2. Ikupaeli alipofika Mtwara wenyeji wake walimpokeaje?
3. Kama wewe ungekuwa Ikupaeli ungekubali kuondoka katika eneo la asili yako?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Shirikiana na wanafunzi wenzako kufanya uchunguzi katika eneo mnaloishi ili kubaini watu wenye asili tofauti na yenu wanaoishi kwenye eneo hilo. Chora chati inayoonesha asili ya watu hao kwenye daftari lako na kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Kutoa maamuzi yasiyo ya kibaguzi

Je, umewahi kusikia mtu akilalamika kwa mwenzake kuwa anabaguliwa? Ulielewa nini? Je, umewahi kutoa uamuzi wa kibaguzi? Bila shaka una uelewa au una ufahamu wa aina fulani wa dhana ya ubaguzi. Pamoja na uelewa ulionao, ubaguzi unaweza kutafsiriwa kuwa ni hali ya kuwatenga wengine kwa misingi ya rangi, utaifa, dini, kabila, au jinsi zao.

## Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Siku moja baba yake Lungo alimwambia mwanaye Lungo waende matembezini mjini. Lungo alifurahi kuongozana na baba yake. Hivyo, alijiandaa haraka, kisha akamwambia baba yake kuwa yuko tayari. Kwa kuwa kijiji chao kilikuwa mbali, walipaswa kupanda basi. Walipofika mjini walitembelea maduka mengi kwa kuwa baba yake Lungo alitaka kumnunulia baiskeli mwanaye. Waliingia karibu maduka manne ili kujiridhisha na bei ambayo angeweza kumudu kununua baiskeli ya mwanaye. Katika maduka hayo manne, mawili yalikuwa ya watu wenye asili ya Kihindi, moja la Mtanzania na moja la Mchina. Baadaye alifanya uamuzi wa kununua baiskeli katika duka la Mhindi kwa kuwa bei yake aliimudu.

Walipokuwa njiani wakirudi nyumbani, Lungo alimweleza baba yake kwamba walipokuwa mjini ameshangaa kuona maduka ya watu wenye asili tofauti wakiendelea na shughuli zao kama kawaida bila hofu. Baba yake alimjibu mwanaye kwamba tangu nchi yetu ipate uhuru, ilidhamiria kuwajali raia wote bila kujali dini, rangi, asili, au nasaba zao. Hicho ulichokiona kinadhihirisha wazi kuwa nchi yetu haina ubaguzi na inawapa raia wake wote haki na fursa sawa.

Lungo alimshukuru sana baba yake kwa zawadi na kwa kujifunza mambo mengi yakiwemo ya kuishi na watu wenye asili tofauti. Lakini alibaki anashangaa kwamba mtu mwenye asili tofauti kuwa raia wa Tanzania.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 168 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baba yake alimweleza kwamba raia ni mtu yeyote mwenye haki kisheria kwa sababu ya kuzaliwa au kujiandikisha katika taifa fulani na ana haki ya kushiriki katika shughuli za taifa hilo.

**Zoezi la 11**

1. Lungo alipofika mjini alishangaa nini?
2. Umeelewa nini kuhusu maana ya neno uraia?
3. Lungo alijifunza nini katika matembezi na baba yake huko mjini?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kwa nini watu wenye asili tofauti hufanya shughuli zao bila hofu nchini Tanzania? Andika sababu mlizozijadili kwenye daftari lako na uwasilishe kwa mwalimu wa somo.

## Kudumisha uhusiano na watu wengine

Uhusiano ni maafikiano baina ya watu ndani ya nchi na kati ya nchi na nchi. Uhusiano huo unaweza kuwa wa kiutamaduni, kibiashara na kimichezo. Uhusiano na mataifa mbalimbali ni wa muhimu sana na unafaa kudumishwa kwa sababu hukuza mshikamano, upendo na uelewano. Kudumisha uhusiano wa biashara, utamaduni na michezo kwa watu wenye asili tofauti ni moja ya nguzo imara katika kudumisha amani. Uhusiano wa aina hiyo hujenga upendo na mshikamano. Pia, huvunja mipaka ya mawasiliano ya kujifunza tamaduni za mataifa au makabila mengine. Hali kadhalika, hutupa nafasi ya kubadilishana ujuzi na uzoefu, kupata fursa ya kubadilika na kuondokana na taratibu zisizofaa. Vilevile, hutuwezesha kufaidi vipaji vya wengine na kudumisha udugu na urafiki.

Uhusiano wa kibiashara huhusisha nchi moja au taifa moja kwenda kufanya biashara kwa kuingiza bidhaa za nchi moja kwenye nchi nyingine. Uhusiano huu huweza kuingiza pato la taifa na kupanua uwanja wa kibiashara. Kwa upande mwingine, uhusiano wa kimichezo ni uhusiano ambao mataifa huweza kushirikiana katika michezo. Ushirikiano huo unaweza kuwa katika muundo au mfumo wa ama kutoa mchezaji wa nchi moja kwenda kushiriki michezo katika nchi nyingine, au wachezaji

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wa nchi moja kubadilishana uzoefu kimichezo. Kitendo hiki hukuza vipaji vya wachezaji na kuitangaza nchi inayohusika kwa nchi nyingine. Vilevile, uhusiano wa kiutamaduni ni ule ambao taifa moja huruhusu tamaduni zake kuweza kutumika na mataifa mengine. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili huweza kuzungumzwa na baadhi ya Wachina, Wazungu na mataifa mengine ambayo asili yake siyo Tanzania. Uhusiano huu husaidia kukuza utamaduni wa Kitanzania.

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1.



2.




*Kielelezo namba 4: Kudumisha uhusiano wa kibiashara na wa kiutamaduni na watu wa mataifa mengine*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 170
17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 12**

1. Je, wewe unashiriki vipi kudumisha uhusiano na watu wenye asili tofauti?
2. Mambo gani unajifunza unapokuwa na uhusiano wa kibiashara na kiutamaduni na watu wenye asili tofauti?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu njia mtakazotumia kudumisha uhusiano na watu wengine wenye asili tofauti. Andika kwenye daftari lako mbinu mlizojadili, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Kuthamini utu wa mtu

Kuthamini utu wa mtu ni kipengele muhimu sana cha kudumisha amani. Je, utu ni nini? Utu ni ile hali au imani kwamba kila mtu anastahili kuthaminiwa, kukubaliwa, kupendwa, kusikilizwa, kutobughudhiwa, kutambulika na hisia zake kuheshimiwa kwa sababu ni binadamu. Msingi wake uko kwenye imani kuwa kila binadamu ana haki sawa na mwingine. Kuwathamini wengine huhusisha kuthamini mitindo yao ya maisha pamoja na hali zao za kiuchumi na kuwapa yale ambayo ni stahili yao kama binadamu. Hivyo, ili uweze kuishi na watu wenye asili tofauti unapaswa kuwathamini kwa kuwakubali, kuwapenda, kuwasikiliza, kutowabughudhi, kutowatenga, kuwaheshimu, kuheshimu hisia zao na kutowabagua.

**Zoezi la 13**

1. Taja mambo utakayoyafanya yenye kuonesha unathamini utu wa wenzako.
2. Orodhesha matendo ya kuthamini utu unayoyajua.
3. Eleza matendo uliyowahi kufanya kwa watu wenye asili tofauti yenye kuonesha kuthamini utu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 171 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wanafunzi wenzako muweze kubaini matendo yasiyo thamini utu wanayofanyiwa wanafunzi katika shule yenu. Andika matendo hayo katika daftari lako kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

## Njia mbalimbali za kupata taarifa juu ya watu wenye asili tofauti waishio Tanzania

Katika sehemu hii, tutaendelea kujifunza njia mbalimbali za kupata taarifa juu ya watu wenye asili tofauti waishio Tanzania ili kuweza kujifunza kama sehemu ya kudumisha amani.

Hebu jaribu kujiuliza, katika eneo unaloishi ulipataje taarifa zozote zinazomhusu rafiki yako? Ni muhimu kupata taarifa juu ya watu wenye asili tofauti kwa ajili ya usalama wa nchi yetu. Unaweza kuwauliza wahusika wenyewe, kuwauliza watu walio karibu nao, kuuliza kwenye taasisi wanazofanyia kazi, kutembelea ofisi za uhamiaji na vyombo vingine ili kupata taarifa hizo. Njia nyingine inaweza kuwa kuwaomba wahusika vitambulisho vyao, kusikiliza simulizi zao na kusoma magazeti na vitabu na kusikiliza vyombo vya habari ili kupata taarifa zao. Unafikiri kwa nini ni muhimu kupata taarifa zao?

### Tafakari matendo haya

1. Kijana mmoja wa kiume mwenye asili tofauti na jamii anamoishi alikuwa ameanzisha kikundi cha mafunzo ya karate kwa vijana bila viongozi wanaohusika kujua. Vijana walipofuzu mafunzo hayo walianza kuwa vibaka.
2. Mwalimu mwenye asili ya kigeni alikuwa ameanzisha shule yake bila kufuata taratibu zinazohusika, wanafunzi na wazazi walianza kulalamika.
3. Katika kijiji cha Mpakani kuna vijana waliingia kwa siri kuja kulima na kufanya kazi za vibarua. Siku moja walimpiga mtu wa kijiji hicho na kutokomea.

Je, umegundua nini katika matendo hayo?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Siku moja viongozi wa Kijiji cha Mtakuja waliitisha mkutano wa wananchi wote ili kuelimishana na kupeana taarifa juu ya usalama wa eneo lao. Mwenyekiti alipofungua mkutano, aliomba wananchi waseme kero zilizopo katika maeneo yao. Wananchi wengi walisema kero mbalimbali ikiwemo ya kuongezeka kwa watu wasiowatambua pamoja na ongezeko la uhalifu katika maeneo yao. Walisema yawezekana kuwa hali hii ndiyo inayosababisha ongezeko la vitendo vya udokozi na uhalifu mwingine.

Mwenyekiti aliwashukuru wananchi hao kwa taarifa hiyo. Aliwaomba wananchi wote kuwa waangalifu na wageni wowote hasa wale wanaowatilia shaka. Pia, aliwaagiza wale wanaopangisha nyumba wahakikishe mikataba ina picha za wapangaji wao. Pia, wahakikishe wanawasiliana na serikali ya kijiji kabla ya kuingia mikataba ya upangishaji nyumba kwa ajili ya ushauri zaidi. Alisema, "Hata kama ni mgeni amekuja kuwatembelea hakikisheni viongozi wenu wanajua."

## Zoezi la 14

1. Unafikiri kwa nini ni muhimu kutaarifu viongozi au mamlaka zinazohusika pindi tunapoona wageni tunaowatilia shaka au tusiowafahamu?
2. Kama ungeshiriki kwenye mkutano kama huo ungeweza kuwataja watu wenye asili tofauti kama alivyofanya mwananchi huyo?
3. Katika jamii unayoishi mnafanya nini ili kupata taarifa za watu wanaoingia katika eneo lenu?

## Kazi ya Kufanya

Mkiongozwa na mwalimu, fanyeni uchunguzi kwenye Mtaa au Kijiji chenu na kubainisha njia zinazotumika kupata taarifa za wageni wanaoingia katika maeneo yenu. Kila mmoja aandike njia hizo katika daftari lake kisha awasilishe kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 173 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 15

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku.**

1. Ipi kati ya zifuatazo ni faida ya kuchangamana na watu wa asili tofauti?:
   (a) upendo na kuheshimiana
   (b) ubaguzi
   (c) kuwa na moyo wa kutokuthamini utu

2. Kubaguana kwa misingi ya rangi, kabila au imani kuna matokeo gani?
   (a) kunaleta kuheshimu watu wengine
   (b) kunaleta maendeleo ya kila kundi
   (c) kunakuza chuki na mafarakano katika jamii

3. Unapoona mtu mwenye asili ya China anaongea Kiswahili inamaanisha nini?
   (a) hajui lugha yake ya Kichina
   (b) anakipenda Kiswahili kuliko Kichina
   (c) anaimarisha uhusiano wa kiutamaduni na nchi yetu

4. Uhuru wa mtu kuishi mahali popote nchini ni mfano wa nini?
   (a) haki za binadamu
   (b) njia za kupata maadui wengi
   (c) mbinu za kuzuia uzururaji

5. Tunaonesha kuthamini utu wa mtu tukifanya matendo gani?
   (a) tunapoangalia mwonekano wake
   (b) tunapoonesha kumjali bila kumbagua
   (c) tunapoangalia mavazi na sura yake

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Nasaba | uhusiano wa kiukoo |
| Utu | hali ya kuwa na tabia zinazojali hadhi ya mtu |
| Ughaibuni | nchi za mbali |
| Maradufu | mara mbili ya kitu kingine |
| Tokomea | kwenda mahali kusiko julikana bila taarifa |
| Dhamiria | kusudia kufanya jambo |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 174 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Kushirikiana na mataifa mengine

Ulipokuwa darasa la nne ulijifunza njia za kuboresha uhusiano mwema na watu wenye asili tofauti, yakiwemo matendo ya ukarimu na misingi ya urafiki mwema na dhana ya utandawazi. Katika sura hii, utajifunza ushirikiano baina ya mataifa, uhusiano wa kibalozi na jumuiya za kimataifa. Pia, utajifunza faida na hasara za utandawazi.

### Manufaa ya ushirikiano baina ya mataifa

Ushirikiano wa kimataifa ni nini? Ushirikiano wa kimataifa ni hali ya mataifa kukubaliana na kufanya jambo kwa pamoja. Mataifa mengi duniani hushirikiana kukusanya nguvu kwa manufaa ya pande zote. Ushirikiano huu huwezesha kubadilishana uzoefu na ujuzi. Pia, hujenga urafiki, kwa mfano, kwa njia ya utamaduni, biashara, siasa na uchumi. Uhusiano mzuri wa kimataifa huboresha usalama na amani. Uhusiano mwema ni muhimu sana hasa kwa nchi jirani. Kupitia ushirikiano wa kimataifa, Tanzania hunufaika kwenye mambo mengi kama masoko ya bidhaa zake, mikopo, wataalamu na nafasi za masomo.

### Sera ya Tanzania ya uhusiano wa kimataifa

Sera ya Tanzania ya uhusiano wa kimataifa ya mwaka 2015 ndiyo dira ya nchi inayoelekeza juu ya uhusiano huo. Sera hiyo ina mambo makuu yafuatayo: kulinda uhuru na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuimarisha umoja wa mataifa na kushiriki kuboresha maendeleo, amani na usalama ulimwenguni. Mambo mengine ni kupigania uboreshaji wa umoja wa kimataifa na mashirika ya fedha ulimwenguni na kushirikiana na nchi yoyote yenye nia njema na Tanzania. Vilevile, sera inahimiza kukuza ushirikiano baina ya nchi zinazoendelea; kupigania mfumo mpya wa uchumi duniani na kudumisha umoja wa Afrika.

### Faida za uhusiano wa kimataifa

Tanzania inashirikiana na mataifa mengine katika nyanja mbalimbali ikiwemo siasa, uchumi, diplomasia na utamaduni. Ushirikiano wa kiuchumi ni muhimu kwani hakuna nchi duniani inayojitosheleza kiuchumi. Biashara ya kimataifa inawezekana pale tu penye ushirikiano wa kiuchumi. Balozi



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

zetu mbalimbali zipo ili kuimarisha uhusiano wa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kati ya Tanzania na nchi za nje. Ushirikiano wa kiutamaduni unachochewa na ushirikiano wa kisiasa na kiuchumi. Faida nyingine za ushirikiano wa kimatiafa ni kuimarisha ulinzi na usalama na kudumisha ujirani mwema. Kwa mfano, uhusiano baina ya Tanzania na jirani zake kama vile Kenya, Uganda, Zambia, Rwanda, Msumbiji na Burundi unadumisha ujirani mwema.

Ushirikiano wa kimataifa hudumisha amani, huchochea maendeleo na pia husaidia kubadilishana uzoefu. Aidha, ushirikiano huo huimarisha biashara hususan pale ambapo nchi zinaamua kuwa na sarafu moja. Hali kadhalika, ushirikiano wa kimataifa unasaidia kubadilishana teknolojia baina ya nchi washirika. Vilevile, ushirikiano hurahisisha uhuru wa kusafiri kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine.

## Changamoto za Ushirikiano wa Kimataifa

Kuna changamoto mbalimbali za ushirikiano wa kimataifa. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na nchi wanachama kutoheshimu mikataba, kutokuaminiana, tofauti za kiitikadi na kitamaduni. Changamoto nyingine ni migogoro ya mipaka, migogoro ya kibiashara na mabadiliko ya kiutawala. Pia, zinaweza kutokea tofauti za kiuchumi na maendeleo ya taifa moja kujiona lina nguvu kuliko taifa jingine. Aidha, vita vya wenyewe kwa wenyewe ndani ya nchi na ugaidi ni miongoni mwa changamoto za ushirikiano wa kimataifa.

**Chunguza picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1.



FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 176 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



*Kielelezo namba 1: Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine*

**Zoezi la 1**

1. Unaona nini kwenye picha za kielelezo namba 1?
2. Taja faida zinazoweza kupatikana kutokana na shughuli inayofanyika katika picha namba 2.
3. Ni nchi zipi hupakana na Tanzania ?
4. Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine unaongozwa na sera ya mwaka gani?

**Kazi ya Kufanya**

Katika makundi, jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu faida za uhusiano kati ya Tanzania na mataifa mengine kiuchumi na kisiasa. Andika faida hizo katika daftari lako, kisha wasilisha kwa mwalimu wako wa somo.

## Jumuiya za Kimataifa

Jumuiya za Kimataifa zimeundwa na nchi mbalimbali. Baadhi ya jumuiya hizo ni: Jumuiya ya Madola, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Jumuiya hizi zimeundwa kwa malengo na kazi mbalimbali za kimataifa.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 177 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Jumuiya ya Madola

Jumuiya ya madola ni umoja wa mataifa huru yaliyokuwa makoloni ya Uingereza, ikiwemo Uingereza yenyewe. Ilianzishwa mwaka 1949. Baadhi ya malengo ya Jumuiya ya Madola ni: kujenga umoja, ushirikiano, urafiki na udugu kati ya nchi zilizowahi kuwa chini ya ukoloni wa Uingereza. Malengo mengine ni kutatua migogoro ya kisiasa katika nchi ambazo ni wanachama na kuhimiza amani na usalama. Pia, jumuiya hii ina malengo ya kujenga haki na usawa duniani, kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kuhimiza uhuru, usawa, haki,na heshima ya binadamu. Jumuiya ya Madola hutathmini utekelezaji wa malengo hayo kwa kukutana mara moja kila baada ya miaka miwili.

Tanzania hupata faida zifuatazo kwa kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Madola. Nchi maskini zinapokuwa na uhusiano na dola kubwa kunakuwepo na ushawishi wa kusimamia maslahi yao. Hii ni faida kubwa kidiplomasia kwani nchi hizo zinapata fursa ya kusikilizwa na madola makubwa. Pia, kuna faida za kiuchumi. Kwa mfano, Uingereza hutoa soko kwa bidhaa za nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola.

Faida nyingine ni kiutamaduni, kielimu na kiuchumi. Uingereza hutoa nafasi za masomo kwa nchi wanachama. Jumuiya ya Madola pia huandaa michezo mbalimbali inayojumuisha nchi wanachama. Vilevile, nchi tajiri kwa mfano Uingereza, Kanada na Australia, hutoa misaada na mikopo kwa nchi maskini ambazo ni wanachama.

## Umoja wa Mataifa

Umoja wa mataifa ni nini? Umoja wa mataifa ni jumuiya ya nchi huru duniani. Umoja wa mataifa ulianzishwa mwaka 1945 baada ya vita kuu ya pili ya dunia.

## Madhumuni ya Umoja wa Mataifa

(i) Kudumisha amani na Usalama wa Mataifa

(ii) Kutatua migogoro ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kisheria.

## Mafanikio ya Umoja wa Mataifa

Baadhi ya mafanikio ya umoja wa mataifa ni:

(i) Kuepusha vita nyingine ya dunia.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 178 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Kupunguza kasi ya utengenezaji wa silaha hatarishi, kama vile silaha za nyukilia.

(iii) Kusimamia michakato ya upatikanaji wa uhuru wa nchi mbalimbali barani Afrika kama vile : Tanzania, Zimbabwe, Namibia, Kenya, Uganda na nchi nyingine nyingi za Afrika.

(iv) Usuluhishi wa migogoro kati ya nchi na nchi na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

(v) Kutoa ulinzi wa kijeshi na misaada katika nchi zenye vita.

(vi) Kuanzisha mashirika mbalimbali ya maendeleo ya jamii, uchumi, elimu na kazi. Mfano, wa mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Kazi Duniani, Shirika la Maendeleo ya Watoto, Shirika la Maendeleo ya watu na Shirika la Wakimbizi.

(vii) Kuondoa ubaguzi wa rangi na ukoloni mkongwe.

## Changamoto za Umoja wa Mataifa

Umoja huu una changamoto nyingi zikiwemo mgawanyiko wa mataifa tajiri na maskini duniani, migogoro ya vita vya kikabila na majimbo mfano, Nigeria, Burundi, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.




*Kielelezo namba 2: Wakimbizi wakiwa katika kambi ya shirika la Umoja wa Mataifa*



URAIA NA MAADILI STD V .indd 179 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Umoja wa Afrika

Umoja wa Afrika ulianzishwa mwaka 2002 kwa madhumuni yafuatayo: kuleta umoja na mshikamano miongoni mwa nchi za Afrika na kulinda uhuru na uadilifu miongoni mwa nchi wanachama. Kusisitiza ushirikiano wa kimataifa na kuzingatia haki za binadamu. Pia, Umoja wa Afrika hukuza amani, ulinzi na usalama wa bara la Afrika. Vilevile, hukuza misingi ya demokrasia na utawala bora miongoni mwa wanachama. Pia, umoja huu hukuza maendeleo endelevu ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na kuchochea maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nchi wanachama.

## Mafanikio

Kupitia umoja huu, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Baadhi ya mafanikio hayo ni kuendelea kudumisha ushirikiano wa kanda za kiuchumi kama vile: Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Soko Nafuu la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika na Ushirikiano wa Kiuchumi wa Nchi za Afrika ya Magharibi.

Madhumuni makuu ya jumuiya hizi ni kupambana na umaskini na magonjwa katika nchi wanachama, pamoja na kudumisha amani na umoja miongoni mwa nchi wanachama. Mafanikio mengine ni kujengwa kwa miundombinu ya kuunganisha nchi za Kiafrika ili kurahisisha biashara na usafiri. Mfano, barabara inayounganisha nchi za Afrika inayotoka Cape Town nchini Afrika Kusini hadi Kairo, Misri kupitia Dodoma na Manyara nchini Tanzania.

## Changamoto

Changamoto kubwa ni umasikini miongoni mwa wanachama na vita vya makundi mbalimbali. Mfano, vita ya wenyewe kwa wenyewe nchini Sudan Kusini.

## Jumuiya ya Afrika Mashariki

Ushirikiano kati ya nchi za Afrika Mashariki ulianza tangu mwaka 1947 na ulihusisha nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zikiwa makoloni ya Uingereza. Wakati huo ushirikiano ulihusu huduma za jamii tu. Magavana wa kikoloni wa nchi hizi ndio waliokuwa na mamlaka ya mwisho kwenye ushirikiano huu. Baada ya uhuru wa nchi hizo, umoja huu uliendelezwa. Chini ya jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoundwa mwaka 1967, mashirika ya huduma mbalimbali yalianzishwa. Mashirika hayo ni: shirika la reli, bandari, fedha, posta na simu na baraza la mitihani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jumuiya hii ilivunjika mwaka 1977 kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutofautiana kwa siasa za nchi wanachama ambapo Kenya ilikuwa nchi ya kibepari lakini Tanzania ilikuwa nchi ya kijamaa, Uganda iliingia katika kipindi cha udikteta wa Idi Amin aliyeharibu uhusiano na majirani alipoanza kudai mkoa wa Kagera nchini Tanzania ni sehemu ya Uganda. Pia, kulikuwa na madai ya Kenya kuwa na viti vingi zaidi kuliko Uganda na Tanzania katika kamati ya maamuzi ya jumuiya hiyo. Mwaka 1993 viongozi wa Afrika Mashariki, Rais Daniel Arap Moi wa Kenya, Rais Ali Hassan Mwinyi wa Tanzania na Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda walianza kufanya mazungumzo ya kufufua ushirikiano wa nchi zao na tarehe 7/7/2000 Jumuiya mpya ya Afrika ya Mashariki ilizaliwa katika makao yake makuu jijini Arusha. Baadaye, nchi wanachama ziliongezeka na kufikia nchi wanachama sita. Nchi za Burundi na Rwanda zilijiunga mwaka 2007 na Sudan Kusini ilijiunga katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 2016.

## Malengo

Malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na kukuza maendeleo endelevu, kukuza utawala bora na uwajibikaji, kuondoa vikwazo vya kibiashara, kutembeleana, pamoja na kudumisha umoja na mshikamano miongoni mwa nchi wanachama. Malengo mengine ni kuanzisha shirikisho la kisiasa na kufikia maendeleo ya kiuchumi na maisha bora kwa wananchi wa nchi wanachama.

Baadhi ya nyanja za ushirikiano zilikuwa kama ifuatavyo: Kuondoa vikwazo vya biashara kwa kuwa na ushuru wa pamoja wa forodha, kuanzisha soko la pamoja na kuwa na sera na mikakati ya pamoja ya maendeleo ya viwanda. Pia, Jumuiya inakusudia kuwa na mfumo mmoja wa fedha na uhifadhi wa mazingira.

## Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Tanzania ni moja ya wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Jumuiya hii ilianzishwa mwaka 1980 na inahusisha nchi zilizopo kusini mwa Afrika.

Makao yake makuu yapo Lusaka nchini Zambia. Jumuiya hii ina jumla ya nchi wanachama 15 ambazo ni Afrika Kusini, Angola, Botswana, eSwatini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lesotho, Madagaska, Malawi, Morisi, Msumbiji, Namibia, visiwa vya Shelisheli, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.



URAIA NA MAADILI STD V .indd 181 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Malengo

Malengo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika yanajumuisha kudumisha ulinzi, mshikamano na usalama, kuendeleza miundombinu ya mawasiliano na kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nchi zilizoendelea. Pia, Jumuiya hii ina lengo la kuunda umoja wa kibiashara na kutatua changamoto za kiuchumi, kijamii na kisiasa katika nchi wanachama. Vilevile, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ina lengo la kuendeleza kilimo na viwanda katika nchi wanachama.

### Zoezi la 2

1. Orodhesha jumuiya mbalimbali za kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama.
2. Orodhesha faida ambazo Tanzania inapata kwa kuwa mwanachama wa jumuiya za kimataifa.
3. Umoja wa Mataifa ni nini?
4. Nini madhumuni ya Umoja wa Mataifa?
5. Orodhesha madhumuni na faida ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.
6. Taja majina ya marais wa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### Kazi ya Kufanya

Kwa kusaidiana na mwalimu wa somo, jadiliana na wenzako katika vikundi, faida mbalimbali za Tanzania kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## Viashiria na athari za utandawazi nchini Tanzania

Je, utandawazi ni nini? Utandawazi ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali, kama vile biashara, uchumi, siasa, jamii na utamaduni. Mfumo huu wa uhusiano unawezeshwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Teknolojia hii inayafanya mataifa na jamii kuwasiliana kwa urahisi kwa kutumia

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA NA MAADILI STD V .indd 182 17/08/2021 11:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kompyuta au simu. Mfumo huu, umefanya mataifa kuwa na mwingiliano na ushirikiano mkubwa katika nyanja mbalimbali zilizotajwa hapo juu. Hivyo, katika sehemu hii utajifunza athari za utandawazi zikiwemo faida na hasara zake. Vilevile, utajifunza jinsi ya kupambana na athari za utandawazi nchini Tanzania.

Viashiria vya utandawazi ni pamoja na uhuru wa uwekezaji wa mitaji na fedha wa kimataifa, uchumi wa soko huria, uhuru wa watu, mali na teknolojia kusafirishwa duniani. Pia, huhusisha uzingatiaji wa demokrasia na utawala bora. Viashiria vingine vya utandawazi ni kusambaa kwa mashirika ya kimataifa, kama vile mabenki ya kimataifa na makampuni ya kibiashara. Viashiria vingine ni kama vile, baadhi ya serikali kujitoa kwenye mfumo wa biashara za kimataifa, kuongezeka kwa teknolojia ya habari na mawasiliano duniani, hasa vyombo vya habari vya kimataifa na matumizi ya mitandao ya kijamii.

**Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Zena:** Babu, hivi enzi zenu kulikuwa na utandawazi?

**Babu:** Utandawazi! Ndiyo nini?

**Zena:** Utandawazi ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali kama vile biashara, uchumi, siasa, jamii na utamaduni.

**Babu:** Ahaa! Sasa mnapata manufaa gani katika huo utandawazi?

**Zena:** Utandawazi una manufaa mengi. Utandawazi umepunguza vikwazo vya mipaka ya nchi ya kufanya biashara na kufanya kazi. Umeleta ajira, tunabadilishana utamaduni unaofaa na kuongeza uwekezaji. Vilevile, kupitia uwekezaji tunakuza teknolojia.

Hivyo, utandawazi unasaidia kuboresha huduma za jamii kama afya, maji, elimu na usafiri.

**Babu:** Umetaja manufaa tu, mbona husemi hasara za huo utandawazi wenu?

**Zena:** Ni kweli babu, kila chenye faida, kina hasara pia. Utandawazi umepunguza uhuru wa serikali kujiongoza. Unasababisha kupitishwa kwa vitu haramu kama vile dawa za kulevya na



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

silaha. Pia, umeathiri utamaduni wetu kwani tunaiga yasiyofaa kwa maadili ya jamii yetu. Vilevile, umeleta uhalifu wa kimataifa hasa wizi wa mtandaoni na ugaidi. Aidha, utandawazi unaongeza unyonyaji kwa nchi maskini.

**Babu:** Ndiyo maana, maadili yenu vijana sasa hivi yana poromoka! Sasa mnafanyaje ili kupambana na athari hizo za utandawazi?

**Zena:** Babu, inabidi tusaidiane wote kupambana kwani umoja ni nguvu. Tunatakiwa kuboresha elimu yetu ili isaidie kuchuja matokeo ya utandawazi yanayofaa na yasiyofaa. Tutumie vizuri rasilimali zetu ili tuondokane na misaada yenye masharti magumu. Vilevile, tuimarishe na kusimamia sera na sheria zetu.

**Babu:** Ni sawa mjukuu wangu. Halafu, inabidi kuzingatia maadili yetu ya Kitanzania. Tulinde na tudumishe utamaduni wetu. Tuache kuiga utamaduni wa ughaibuni bila kutafakari. Mimi nitakuwa nawacharaza bakora vijana wote watakaoiga utamaduni usiofaa katika jamii yetu.

**Zena:** Mimi najitambua, hunipati babu!

**Zoezi la 3**

1. Taja faida za utandawazi.
2. Nini madhara ya kuwepo kwa utandawazi?
3. Ainisha njia za kupambana na athari za utandawazi?

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na wenzako kuhusu vitendo vilivyopo katika jamii yako vinavyoonesha jamii inavyofaidika na utandawazi. Orodhesha vitendo hivyo, kisha wasilisha kwa mwalimu wa somo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

### Sehemu A

Oanisha maneno ya **sehemu A** na sentensi katika **sehemu B** ili kupata maana sahihi.

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Ushirikiano wa kimataifa | A. upotoshwaji wa maadili |
| 2. Jumuiya ambazo Tanzania ni mwanachama | B. nchi zote huru duniani ni wanachama wa hiari |
| 3. Kudumisha uhusiano wa kimataifa | C. kunakuza biashara |
| 4. Hasara za utandawazi | D. utengano |
| 5. Umoja wa Mataifa | E. ni uhusiano baina ya taifa moja na jingine |
| | F. Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Madola na Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| | G. Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Utandawazi na Teknolojia, Umoja wa Kibiashara, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Madola |

### Sehemu B

Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi.

6. Ni marufuku kwa nchi iliyo na uchumi wa chini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. __________
7. Mtanzania anatakiwa kufanya biashara zake hapa nchini tu. __________

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Uhusiano wa Tanzania na Kenya umesaidia kuboresha uchumi wa nchi hizo mbili. _________

9. Umoja wa Mataifa hutoa msaada wa kifedha kwa nchi wanachama kupitia jumuiya zake. _________

10. Tanzania hunufaika na uhusiano wa kibalozi na mataifa mengine kiutamaduni. _________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Asilani | kamwe, abadani, katu |
| Changamoto | hali au vikwazo vinavyomweka mtu katika majaribu au shida |
| Diplomasia | kanuni na taratibu za kuanzisha na kuendeleza uhusiano baina ya mataifa |
| Dola | chombo chenye mamlaka ya kuendesha utawala au siasa ya nchi, serikali, taifa |
| Jumuiya | mkusanyiko au mkutano wa watu |
| Kuenzi | kuonesha heshima au kuweka mtu au kitu kwenye nafasi ya heshimu ya juu |
| Manani | Mungu |
| Sera | utaratibu au mwongozo wa kuendesha mambo ya serikali. |
| Ubaguzi | ni hali ya kutoa vitu au huduma kwa upendeleo |
| Ubalozi | uwakilishi wa nchi katika nchi nyingine |
| Ugaidi | vitendo vya kutisha, mauaji na mashambulizi kwa watu wasio na hatia yanayofanywa kwa ajili ya kufikia malengo fulani ya kisiasa au kidini |
| Utu | hali ya kuwa na tabia zinazolingana na hadhi ya mtu au binadamu |

FOR ONLINE USE ONLY

## Vitabu kutoka
## Taasisi ya Elimu Tanzania

### Darasa la Tano

























ISBN 978-9987-09-330-4